


# UNABII WA HABARI ZA BIBLIA

Ni nini kilizuka kule Fatima?



Pentekoste, Ndoto,  
**pamoja na Karama za Kiroho**

Maono, Historia,  
**pamoja na Kanisa la Mungu**

# HABARI ZA UNABII WA BIBLIA



3

24

31

33

## KATIKA TOLEO HILI:

- 3 Maono, Historia, pamoja na Kanisa la Mungu** Je, Mungu hutumia maono? Je, Shetani hutumia maono? Ni kwa namna ipi maono yameubadiri ulimwengu?
- 10 Ni nini kilizuka kule Fatima?** Ni nini kilizuka kule Fatima, Ureno mnamo 1917? Hili ni kwa sababu gani linaumuhimu kwa sasa? Je, Fatima inatoa dalili kuhusu Shetani na mpango wake?
- 14 Jisomee Kozi ya Biblia Somo la 2: Hapa tunakuletea habari njema . . . UJUMBE uliotumwa toka Mbinguni.** Hili ni somo la pili la Kozi ya kuwasaidia watu wajisomee na kielewaa vema Biblia.
- 24 Pentekoste, Ndoto, pamoja na Karama za Kiroho.** Aina mbalimbali za karama za kiroho zimetajwa katika Biblia. Je, zipo zozote mionganoni mwake ambazo ni dhahiri kwa sasa? Vipi kuhusu ndoto? Fasiri (fafanuzi), maarifa, utambuzi, na upendo ni nini?
- 31 Je, unavumilia hadi mwisho?** Baadhi katika Kanisa la Mungu wananaia "kung'ang'ana" hadi Kristo atakaporudi. Kimtazamo wao, "WANAVUMILIA" hadi mwisho (Math. 24:13) – lakini siyo kwa namna ambayo Kristo alitaka.
- 33 Evans Ochieng na Kanisa la Continuing Church of God:** Makala hii inatoa utambulisho juu ya Bwana Evans Ochieng, Mchungaji wa Kanisa la Continuing Church of God anayeishi nchini Kenya.

**Jarada la Nyuma: Internet na Radio.** Hili linaonyesha ni wapi watu wanaweza kuupata ujumbe kutoka Kanisa la Continuing Church of God.

**Kuhusu Jarada la Mbele:** Mlinganisho baina ya sanamu ya kuchonga iliyoko Fatima (photo na Joyce Thiel) pamoja na ile sanamu itokanayo na ufanuzi wa kile kinachodaiwa kuzuka na kuwatoka watu kule Fatima mwaka 1917 (sanaa na Brian Thiel pamoja na James Estoque). Kusema kweli 'Mama wa Fatima' alizuka akiwa kavaa siketi fupi!

Unabii wa Habari zaBiblia huchapishwa na Kanisa la Continuing Church of God, 1248 E. Grand Avenue, Suite A, Arroyo Grande, CA, 93420. <http://www.ccg.org>

©2014 Continuing Church of God. Limechapishwa katika U.S.A. Haki zote zimehifadhiwa.

Kunakiri makala yote ama sehemu yake pasipo ruhusa ya kimaandishi toka kwa mmiliki hairuhusiwi. Tunaheshimu haki zako hivyo hatutoi, kuuza ama kukodisha orodha ya mawasiliano yetu. Endapo haungependa kuendelea kupoakea gazeti hili, wasiliana na office yetu iliyoko Arroyo Grande. Maandiko yamenukuriwa toka New King James Version (©Thomas Nelson, Inc., Publishers, used by permission) Isipokuwa pale tu tumeelekeza vinginevyo.

Unabii wa Habari za Biblia-HUWEZESWA KWA MICHANGO YENU

Bible News Prophecy has no subscription or newsstand price. This magazine is provided free of charge by the Continuing Church of God. It is made possible by the voluntary, freely given tithes and offerings of the membership of the Church and others who have elected to support the work of the Church. Contributions are gratefully welcomed and are tax-deductible in the U.S. Those who wish to voluntarily aid and support this worldwide Work of God are gladly welcomed as co-workers in this major effort to preach and publish the gospel to all nations. Contributions should be sent to: Continuing Church of God, 1248 E. Grand Avenue, Suite A, Arroyo Grande, CA, 93420.

Mhariri Mkuu: Bob Thiel

Mpigachapa/Mhariri Msaidizi: Joyce Thiel


Masahihihisho na: Kayla Morgan

Maandalizi &Uchapaji: Burdine Printing

Picha: Picha zote zimetokana na familia ya Thiel ama na nyanzo ya mitandao ya kijamii kama vile Wikipedia (ikiwa chanzo hakikutajwa, itakuwa ni kwa sababu inaanikia kwamba chanzo husika kiliachia picha iwe kwa matumizi ya umma pasipo masharti yeoyote).

# KUTOKA KWA MHARIRI MKUU: BOB THIEL

## MAONO, HISTORIA, PAMOJA NA KANISA LA MUNGU



Anayedaiwa kuwa ni ‘Mama wa Guadalupe’, Mexico City  
(Photo na Jan Zatko)

Maono ni kitu gani? Je, maono yameubadiri ulimwengu? Je, maono ni swala linalokubaliwa na Biblia kuwa ni takatifu? Je, madai ya watu kutembelea maono ni swala la Wakatoliki pekee ama limeliathiri hata Kanisa la Mungu pia? Na kama ni hivyo, limeliathiri kwa namna gani?

Je, maono yataliathiri Kanisa la Mungu muda ujao?

### Maono yatokanayo na kuzukiwa na mtu mashuhuri wa kale (Apparition) ni kitu gani?

Hapa tunakuletea ufanuzi wa maana ya maono (Apparition), kulingana na Dictionary.com:

ap·pa·ri·tion [ap-uh-rishuhn] noun

1. Ni kutokea kimiujiza kwa mtu ama kitu...

Wengi mionganoni mwa Wakatoliki wanaamini kwamba mama wa Yesu aliyekwisha fariki, Maria, amekuwa akiwatokea watu kama maono kwa karne nyingi katika historia. Baadhi ya

maono yaliyodaiwa kutokea pamoja na miujiza yake yalihusika kwa kiasi kikubwa katika kuibuka kwa kanisa pamoja na baadhi ya makanisa mengine yaliyotokana nalo.

### Biblia na Maono

Je, maono yanakubalika katika Biblia kwa namna yoyote ile? Je, yanapaswa yaaminiwe? Ni kwa namna gani mtu atawea kutofautisha ikiwa yametoka kwa Mungu ama kwa Shetani?

Biblia iko wazi kwamba Mungu nyakati zingine huwatumia malaika kuwapelekea watu wake ujumbe, nyakati zingine kwa kuwatokea ama kupitia ndoto. Hili liko wazi hata nyakati za Agano la Kale (Mwanzo 16:7-12; 21:17-18; 22:11-18; 31:11; Hesabu 22:22-31; Waamuzi 2:1-4; 6:11-22; 13:3-21, n.k.) na pia nyakati za Agano Jipya (Mathayo 1:20-24; 2:13-20; 28:2-7; Luka 1:11-38; Ufunuo 5:2-3, n.k.). Kibiblia, maono (kutokewa) yanaweza kuwa yametoka kwa Mungu.

Biblia inaonyesha kwamba kuzukiwa na malaika kulitumika kutangaza kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji (Luka 11:1-20), kutungwa mimba kwa Yesu Kristo kwa uwezo wa Roho Takatifu kwa Maria (Luka 1:26-38), Kufufuka kwa Yesu Kristo (Mathayo 28:2-7), pamoja na mengine mengi.

Zaidi ya hayo, Agano Jipya linatoa taarifa muhimu kwamba kuzukiwa na malaika ilikuwa ni sehemu ya mwanzo wa historia ya Kanisa la Mungu (Mdo. 5:19-20; 10:3-7; 12:8-11; 27:23-26 ;).

Maono yaliyotokana na Mungu yameubadiri ulimwengu.

### Taarifa za Malaika Watatu

Biblia inaonyesha kwamba Mungu atatumia kutokea kwa malaika hapo baadaye.

Pamoja na maonyo yatokanayo na mashahidi wa Mungu wawili watakaofanya kazi kwa miaka  $3 \frac{1}{2}$  wakiwa na watu wa Mungu waliosalia, pia kukiwa na ishara mbalimbali na baragumu (parapanda au tarumbeta) kutoka kwa Mungu, Mungu atawatumia malaika watatu kutoa onyo la toba kwa ulimwengu. Hivyo, angalau kwa njia hii, maono yatakuwa ni sehemu ya hatua ya mwisho ya kazi ya Mungu:

6Kisha nikamwona malaika mwingine akiruka juu angani, naye alikuwa na Injili ya milele ya kuwatangazia wale waishio duniani, yaani, kwa kila taifa, kabilia, lugha na jamaa. 7Akasema kwa sauti kubwa, “Mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imewadnia. Mwabuduni Yeye aliyeziumba mbingu, dunia, bahari na chemchemi za maji.”

8Malaika wa pili akafuata akisema, “Ameanguka! Ameanguka Babeli aliye mkuu, yeye aliyeafanya mataifa yote kulewa kwa mvinyo wa ghadhabu ya usherati wake.”

9Malaika wa tatu akawafuata hao wawili akisema kwa sauti kubwa, "Kama mtu ye yote anamwabudu huyo mnyama na sanamu yake na kutiwa chapa yake kwenye kipaji chake cha uso au kwenye mkono wake, 10yeye naye, atakunywa mvinyo wa hasira kali ya Mungu ambayo imemiminwa katika kikombe cha ghadhabu yake pasipo kuchanganywa na maji. Naye atateswa kwa moto uwakao na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele za Mwana-Kondoo. 11Nao Moshi wa mateso yao hupanda juu milele na milele. Hakuna mapumziko, mchana wala usiku, kwa wale wamwabuduo huyo mnyama na sanamu yake, au kwa ye yote anayepokea chapa ya jina lake" (Ufunuo 14:6-11).

Sisi katika Kanisa la Continuing Church of God tunahitaji kutambua kwamba Mungu anahitaji watu watubu na atatumia malaika kuuhubiri ujumbe wa Injili yake. Kusema kweli, sababu ya udanganyifu (2 Wathesalonike 2:9-12) na kwa vile wengi wa wanadamu ulimwenguni watafanikiwa kimaisha katika kipindi hicho (ona: Ufunuo 18), basi watapuuzia kutokewa huko na malaika kutoka kwa Mungu. Pengine hiyo ndiyo sababu ni kwanini Biblia inafundisha kwamba "Siku ya Bwana yaja kama mwivi" (2 Petro 3:10).

## Biblia Inaonya Dhidi ya Maono

Pamoja na kwamba Mungu amekuwa akitumia na ataendelea kutumia "maono", wengi mionganoni mwa wanaodai kutokewa na maono kamwe hawakutokewa na maono toka kwa Mungu. Na moja mionganoni mwa maelezo ya 'maono' lililomaarufu sana ni lile ambapo Shetani alipotokea akiwa kama nyoka katika bustani ya Edeni (Mwanzo 3:1-4; Ezekiel 28:11-15; Ufunuo 20:2).

Maandiko yanaonya dhidi ya kuyafuata mafundisho ya mashetani, jambo ambalo siku nyingi linahusisha pia kutokewa na maono ya uongo:

1 Roho asema waziwazi kwamba katika siku za mwisho baadhi ya watu wataiacha imani na kufuata roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani. (1 Timotheo 4:1).

'Mafundisho kadhaa ya mashetani' ambayo yanaelezwa kuwa yanetufikia kuitia maono (ama yalithibitishwa na kutokewa na mapepo) ikiwemo swala la "Roho Mtakatifu", rozari, "roho zisizokufa", kuabudu sanamu, jukumu linalodaiwa kuwa Maria Mama wa Yesu analitenda kwa sasa katika wokovu, kile kinachoitwa kuwa ni "moyo mtakatifu wa Maria", na kuibuka kulikotabiliwa kwa "Mtawala Mkuu" (ambaye maandiko yaonekana ndiye yanatuonya dhidi yake yakieleza kuwa ndiye Mnyama wa mwisho atokaye katika bahari – Mfalme wa Kaskazini), Kutabiri juu ya kuibuka kwa "Kuhani wa Kimalaika" (ambaye maandiko yaonekana ndiye yanatuonya dhidi yake kuwa ndiye Mnyama wa mwisho atokaye kwenye nchi, Mpinga-Kristo wa mwisho, na ndiye Nabii wa Uongo). Pamoja na kwamba aina kama hizi za imani zilikuwepo nyakati za enzi za upagani, kukubaliwa na kupokelewa kwake na makanisa ya Ugiriki na Urumi kuliwezesha kutokewa na maono ya mashetani. Ulimwengu umeathiriwa sana kutokewa na haya maono ya kishetani.

Agano Jipyia pia linaonya kwamba Wakristo wanapaswa:

1Wapanzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho mwone kama zimetoka kwa Mungu, kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea ulimwenguni (1 Yohana 4:1).

Wakristo wanatakiwa "kuzijaribu (kuzipima) roho (maono)". Iwapo zote zingekuwa ni za kweli ama zote siyo za kweli kusingekuwa na sababu ya kutakiwa kuzipima.

Jionee njia mbili za kutathmini kuona iwapo roho ama mono yanayodaiwa kutokewa ni ya uongo:

8 Lakini hata ikiwa sisi au malaika atokaye mbinguni akihubiri injili nyingine tofauti na ile tuliyowahubiria sisi, basi huyo mtu na alaaniwe! 9 Kama vile tuliyokwisha kusema kabla, sasa nasema tena, ikiwa mtu ye yote atawahubiria injili kinyume na ile mliyoipokea na alaaniwe milele (Wagalatia 1:8-9).

1 "Kama nabii, au yule anayetabiri kwa njia ya ndoto, akitijiteza mionganoni mwenu na akwatangazia ishara ya miujiza na ajabu, 2ikiwa ishara au ajabu ya aliyozungumza ikatokea, naye akasema, "Na tufuate miungu mingine," (miungu ambayo hamuifahamu) na tuiabudu," 3kamwe msiyasikilize maneno ya nabii wala mwota ndoto huyo. BWANA Mungu wenu anawajaribu kuangalia kama mnampenda kwa moyo wenu wote na kwa roho yenu yote. 4Ni BWANA Mungu wenu ambaye mnapaswa kumfuata tena ni yeye mnapaswa kumheshimu. Shikeni maagizo yake na kumtii, mtumikieni na kushikamana naye. 5Huyo nabii au mwota ndoto lazima auawe, kwa sababu amehubiri uasi dhidi ya BWANA Mungu wenu, ambaye aliwatoa kutokewa nchi ya Misri na kuwakomboa kutokewa nchi ya utumwa, amejaribu kuwageuza kutokewa njia ambayo BWANA Mungu wenu aliwaagiza mfuate. Ni lazima mwondoe uovu mionganoni mwenu (Torati 13:1-5).

Hivyo, ujumbe wowote halali kutokewa kwa mwota ndoto ama nabii sharti uendane na injili ya kweli na pia sharti usiwe unapingana na amri za Mungu.

## Maswala ya kimitume

Kulingana na Agano Jipyia pamoja na baadhi ya makala za enzi za baada ya Agano Jipyia, Mitume walilazimika kupambana na angalao watu watatu ambao yaonekana walikuwa wametokewa na maono.

Mtume Paulo alilazimika kupinga na kufukuza pepo kutokewa kwa mwanamke ambaye yamkini alikuwa akitoa nabii kwa kutumia uwezo wa mapepo (Matendo 16:16-22). Paulo alipigwa na hata akafungwa kutokewa na swala hili alilolifanya (Matendo 16:23).

Mtume Petro alimkemea Simon Magus (Matendo 8:9-23), ambaye (kulingana na waandishi fulani wa taarifa za kidini wa karne ya 2) wanaelezea kuwa alikuwa akitokewa na malaika/mapepo/maono/na roho (Soma: Matendo 18:9-23). Inastaajabisha kuona kwamba hata wale kwa sasa wanaonekana kuwa ni waumini wa awali wa Kanisa la Roman Katholiki walimlaumu Simon pamoja na wafuasi wake kwa mafundisho kama vile imani ya kuabudu sanamu, kumtukuza mwanamke, fundisho la roho zisizokufa, ibada zenye maneno

ya kuita mapepo, mafumbo, makuhani wa kimafumbo, kujipa nyadhifa na majina ya kimungu kwa viongozi wao, kutoza pesa ili kutoa huduma za kidini, kupenda mila na imani za kufikirika badala ya maandiko matakatifu, Kuwa na kiongozi ambaye anachukuliwa kuwa sawa na Mungu/Kristo hapa duniani, na kujitenga na taratibu za kiKristo za Kibiblia kwa kuzichukulia kuwa ni za Kiyahudi.

Katika karne ya pili, Irenaeus aliandika juu ya tukio lililomhusisha Mtume Yohana na mtu mmoja mpotofu aliyeitwa Cerinthus, tukio ambalo laonekana lilitukia mwishoni mwa karne ya kwanza:

Wapo pia wale waliosikia kutoka kwake amba Yohana, mwanafunzi wa Bwana, alipokuwa akienda kuoga akiwa Efeso, alipomuona Cerinthus akiwepo katika bafu hilo, alitoka mbio kutoka katika nyumba hiyo ya kuogea bila hata kuoga, akipaaza sauti, "Tukimbieni zetu, isije hata nyumba ya kuogea ikaporomoka na kutuangukia, sababu Cerinthus, adui wa ukweli wa Mungu, yuko ndani yake" (Imetafsiriwa toka kitabu: Irenaeus. Adversus Haeres. Book III, Chapter 3, Verse 4).

Cerinthus kimsingi alikuwa akidai kupokea mafundisho yake kutoka kwa "malaika" akichanganya na mtazamo wake binafsi wa kibiblia. Cerinthus alifundisha kwamba kila swala lililomo katika Biblia ni la kimfano tu siyo halisi, alisisistiza kwamba jadi zisizo za kibiblia zilikuwa muhimu zaidi katika kuyafanya maandiko yaeleweke, akichanganya mafundisho ya ki-Gnostic pamoja na Biblia, akijitangaza kuwa yeche ni mtume, akafundisha na kuleta sikuu zisizo za kibiblia, na kudai kwamba malaika wa Mungu walikuwa wakimletea mafundisho na ujumbe mbalimbali. Pamoja na kwamba Wakatoliki walimkataa, bado baadhi ya mafundisho yake taratibu yalikumbatiwa na kuwa sehemu ya imani ya kanisa la Roma.

## Biblia Inaonya Juu ya 'Mama Bikira'

Kumekuwepo na taarifa nyingi juu ya kutokewa na 'maono ya mwanamke' kuanzia karne ya tatu B.K.

Je, Biblia yaweza kuwa na maonyo yoyote kuhusu kile kinachoaminiwa kuwa ni 'kutokewa na maono ya mwanamke'?

Bila ya shaka! Katika Agano la Kale, Biblia inatuonya juu ya "bikira" atumiaye uchawi ambaye pia anaitwa Malkia wa Falme:

1 "Shuka keti mavumbini, Ee Bikira Binti Babeli, keti chini pasipo na kiti cha enzi, Ee binti wa Wakaldayo. Hutaitwa tena mwororo wala wa kupendeza.

4Mkombozi wetu, BWANA Mwenye Nguvu ndilo jina lake, ndiye Yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli. 5 "Keti kimya, ingia gizani, Binti wa Wakaldayo, hutaitwa tena malkia wa falme. 6Niliwakasirikia watu wangu na kuaibisha urithi wangu, niliwatia mikononi mwako, nawe hukuwaonea huruma. Hata juu ya wazee uliweka nira nzito sana. 7Ukasema, 'Nitaendelea kuwa malkia milele!' Lakini hukutafakari mambo haya wala hukuwaza juu ya kile ambacho kingeweza kutokea.

11Maafa yatakuja, nawe hutaweza kuyaondoa kwa uagazi. Janga litakuangukia wala hutaweza kulikinga kwa fidia, msiba mkuu usioweza kuutabiri utakujia ghafula. 12 "Endelea basi na ulozi wako na wingi wa uchawi wako, amba umeutumikia tangu utoto wako, labda utafanikiwa, labda unaweza ukasababisha hofu kuu. 13Ushauri wote uliopokea umekuchosha bure! Wanajimu wako na waje mbele, wale watazamao nyota na watabirio mwezi baada ya mwezi, wao na wawaokoe na lile linalokuja juu yenu. (Isaya 47:1, 4-7, 11-13).

Cha kushangaza, hata ajabu la pili mionganii mwa maajabu saba ya ulimwengu wa kale limeitwa, "Babylon the Great, the Lady of the Kingdoms, the glory of the whole earth"— yaani, 'Babeli Mkuu, Malkia wa Falme, utukufu wa dunia yote!' Je, huoni kwamba kunawenza kuwepo na uhusiano baina ya Babeli ya kale na siri ya Babeli ya nyakati za mwisho iliyotajwa katika Ufunuo 17?

Biblia vilevile yaonekana kuunganisha maelezo ya ulozi wa Mama wa aya ya 7 na 8 za Isaya sura ya 47 na yule kahaba wa Ufunuo 17:1, 18; 18:7-8, 11 pamoja na mji wa Sefania 2:15.

Wengine watashangazwa kwa kuliona hili, lakini "mwanamke" huyu mwovu yaonekana anacheo cha "malkia" na pia "kahaba":

7 "Ukasema, 'Nitaendelea kuwa malkia milele!' .....  
8.....'Mimi ndiye, wala hakuna mwingine zaidi yangu. Kamwe sitakuwa mjane wala sitafiwa na watoto.' 9Haya yote mawili yatacupata kufumba na kufumbua, katika siku moja: kufiwa na watoto na ujane. Vyote hivyo vitakupata...." (Isaya 47:7, 8b, 9).

4 "Yote kwa sababu ya wingi wa tamaa ya ukahaba, anayeshawishi, bibi wa mambo ya uchawi, anayewafanya mataifa mateka kwa ukahaba wake na kuwafanya jamaa za watu mateka kwa ulozi wake" (Nahumu 3:4).

5 "BWANA Mwenyezi anasema, "Mimi ni kinyume na ninyi. Nitafunika uso wako kwa gauni lako. Nitaonyesha mataifa uchi wako na falme aibu yako" (Nahumu 3:5).

3 "Kwa maana mataifa yote yamekunywa mvinyo wa uasherati wake, nao wafalme wa dunia wamefanya uzinzi naye, nao wafanyi biashara wa dunia wametajirika kutokana na wingi wa utajiri wake" (Ufunuo 18:3).

17:1... "Njoo, nitakuonyesha adhabu ya yule kahaba mkuu, aketiye juu ya maji mengi....18:7 Mpatie mateso na huzuni nyingi sawa na utukufu na anasa alizojipatia. Kwa kuwa moyoni mwake hujivuna akisema, 'Mimi ninatawala kama malkia, mimi si mjane wala sitaona huzuni kamwe.' 8Kwa hiyo mapigo yatampata kwa siku moja: mauti, maombolezo na njaa. Naye atateketezwa kwa moto, kwa maana amhukumuye ni Bwana Mungu Mwenyezi..... mataifa yote yalidanganyika kwa uchawi wako (Ufunuo 17:1b, 18:7-8, 23).

Hivyo, elewa kwamba kile kitakachotokea kwa malkia/mama wa falme na pia kwa Babeli, kimeonywa tujiepushe nacho katika kitabu cha Ufunuo na sehemu nyingine. Lakini, "Malkia wa Falme" ndicho cheo ambacho Wakatholiki wamempa Maria.

Wapagani wa ki-Taoist wanamtukuza muungu mke, wamwitaye Tian Hou, ambaye ye ye pia cheo chake walichompa ni "Malkia wa Mbingu"! Makabila mbalimbali ya Wachina nao kadharika humtukuza mwanamke awatokeaye kimaono aliyepewa cheo kilekile (na hilo laonekana linauhusiano wa moja kwa moja na Shetani mwenyewe).

Kiukweli, siyo Biblia wala Mitume hawakuwahi kumtaja Maria Mama wa Yesu popote kwamba alikuwa malkia, mama wa wote, ama "Mama wa Ufalme".

Pamoja na hayo, kwa sababu za kuamini juu ya maono mbalimbali na maelezo ya wale wanaodai kutokewa na kuona maono ya Maria, Wakatholiki humchukulia Maria, mama wa Yesu, ni "Malkia wa Mbingu" na/ama ni "Mama wa Falme". Hili wameliamini kinyume na ukweli kwamba Biblia inaonya dhidi ya yule anayeitwa "Malkia wa Mbingu" (Yeremia 7:18-19; 44:17-25) na inakemea waziwazi dhidi ya yule aitwaye "Mama wa Falme".

Kwa kuwa Biblia inatuonya kwamba "malkia" atatokea katika nyakati za mwisho na atahusika na upotofu akitumia uchawi (Soma: Ufunuo 18:7, 23), hili linapatana na ukweli kwamba mzuka wa kitu kionekanacho kama mwanamke kitawatoka wengi na kuwahadaa wengi katika siku za mwisho.

Udanganyifu wa namna hii wa kutokewa na maono ya anayedaiwa kuwa ni Maria na pia aina nyingine za mizuka umekuwa ni tatizo katika historia ya kanisa.

## Maono yamesaidia Kuibuka Kwa Makanisa ya Kigiriki Na Kirumi

Wakati Wakristo wa kweli hawakubaliani na kwamba Maria Mama wa Yesu amekuwa akiwatokea watu mbalimbali, hili halimaanishi kwamba wale waliodai kutokewa naye ama na maono mengine ya uongo hawakuiathiri historia ya Kanisa la Mungu.

Kutokana na onyo lililoko katika Isaya 47:12, kwamba "Mama wa Falme" angetumia ulozi na uchawi tangia enzi za ubinti wake, nimejiuliza ni lini mzuka wa kwanza wa maono yaliyodaiwa kuwa ni ya Maria ultokea na ni kwa namna gani Kanisa la Mungu linaweza kuwa liliathiriwa na hili.

Miaka kadhaa iliyopita nilifanya utafiti na kukuta kwamba kadri ya mwaka 238-244 B.K. mtu aliyeitwa Gregory (alifariki kadri ya mwaka 270 B.K.) yaonekana ndiye aliyekuwa wa kwanza kudai kutokewa na mzuka wa Maria. Gregory alikuwa amefundishwa na mzushi wa kiallegori kutoka Alexandria, Misri aliyeitwa Oregen. Maono haya anadai yalimtokea kabla baadaye hajawa Askofu Gregory wa Neocaeseria (kwa sasa eneo hilo liko nchi ya Uturuki), na yawezekana swala hili lilichangia kumwezesha awe askofu. Gregory vilevile anajulikana katika historia kama "Gregory Mtenda Miujiza" au "Mtakatifu Gregory Thaumaturgus" (mtenda miujiza). Kuhusu Gregory, wanahistoria Roberts na Donaldson waliandika:

Aliaminika kuwa alikuwa amejaliwa uwezo wa kutenda miujiza, kitu ambacho alikuwa akikifanya mara kwa mara... mapepo yalimtii...aliweza kulipiga joho lake juu ya mtu, na mtu yule akafa...aliweza kuyaita mashetani yenyе uwezo na

kuyarudisha yakakae kwenye hekalu lao.

Haupo mfano wa mtumishi wa Mungu yeyote aliyekuwa akiua watu kwa namna sawa na alivyodaiwa Gregory kufanya, hivyo hili sharti litupe pitcha juu ya uwezo wa Gregori kwamba haukutoka kwa Mungu.

Lakini, kwa kuwa uwezo wa Gregory dhidi ya mapepo pamoja na "miujiza" yake kuwa vilikubaliwa na wengi, akafuatwa na wengi. Yaonekana kwamba ulozi wa Gregory na/au uchawi wake (soma: Isaya 47:5-12; Nahumu 3:4), vikiambatana na mteso kwa wakristo wa kweli yaliyoendeshwa na wafalme, vilisaidia sana kundi la kiimani potofu la Kigiriki na la Kirumi kuwaangamiza wakristo wa kweli wa Kanisa la Mungu kule Asia Ndogo. Gregory vile ndiye anahuksika na kuibuka kwa imani ya kumwabudu Maria iliyoanza katika kipindi chake (inayopatana kwa kila hali na muungu wa kipagani wa kike aitwaye Diana). Maandiko yake (Gregory) aliyozaacha yanafundisha namna ya kumsifu na kumtukuza mama aliyeuita "Bikra Mtakatifu", yakiambatana pia na mafundisho yenyе makufuru kwamba ni Maria (siyo Yesu) ndiye "alifuta dhambi" za Eva. Yeye pia ndiye aliyekuwa miongoni mwa watu wa kwanza waliodai Kristo alifundisha juu ya "Utatu Mtakatifu" pamoja na wazo la kipagani la kwamba wanadamu walikuwa na roho zisizokufa.

Wengi hawatambui kwamba yaonekana hadi kufikia mwanzoni mwa karne ya tatu, idadi ya Wakristo waliokuwa waumini wa Kanisa la Mungu yaonekana kuwa ilizidi ile ya wale waluojiita Wakristo waliokuwa chini ya makanisa yaliyokuwa yakiibuka kama makanisa ya Kigiriki na kirumi. Muona mizuka Gregory hapa ndiye alikuwa kichocheo cha kufanya wengi wajijunge na upotofu wa makanisa ya Kigiriki na Kirumi.

Hali kadharika, katika kipindi hiki ndipo "mwujiza wa ekaristi" yaonekana ndipo ulipoanza. Cyprian wa Carthage aliarifu kwamba, mtenda dhambi mmoja alipoenda kupokea ekaristi, hapohapo mkate huo wa ekaristi uligeuka na kuwa majivu mara tu ulipogusana naye. Kusambaa kwa taarifa za miujiza hiyo kuliwaathiri wengi (soma: Isaya 47:1-12). Pamoja na kwamba "miujiza ya ekaristi" siyo yenyе nguvu sawa na taarifa za maono, bado ni swala linalohusika na kile kilichoonywa kuwa ni ulozi na uchawi. Hadi leo, "miujiza ya ekaristi" inaathari kubwa sana kwa wale wanaokubaliana na imani ya Kanisa la Roma. Nyakati zingine, maono ya kutokewa na Maria pia yamedai kuhusika na kusisitiza matumizi ya hiki kinachoitwa "miujiza ya ekaristi".

## Maono yaliathiri Milki ya Roma

Mwandishi wa Kikatholiki, C.M. Mangan aliandika:

Mwaka 312, Mfalme wa Rumi, Emperor Constantine Mkuu wa1, alikuwa kuleTrier, Ujeruman; ambako alitokewa na mzuka asioutegemea wa msalaba ukionekana angani ukiwa na maandishi ya ajabu, "In hoc signum vinces" ("Katika ishara hii utashinda")! Mfalme alisisimuka kutokana na maono hayo na akawahimiza majeshi yake ya askari 20,000 yajitie moyo na kupambana na vikosi katili vya Mfalme Maxentius vyenye askari 100,000. Askari wa Mfalme Constantine, wengi wao wakiwa ni wapagani, wakachora alama ya msalaba kwenye ngao zao za vita.

"Msalaba" unaodaiwa kuonekana angani unasemekana ulikuwa ni mkuki wenyewe upanga uliokatisha kuunda msalaba. Wakati Yesu aliwaonya watu wake kwamba wasiwe sehemu ya vita vya kimwili vya dunia hii (Yohana 18:36) na kwamba hilo ndilo limekuwa msimamo wa Kanisa la Mungu kwa muda mrefu, lakini baada ya kushinda vita hiyo pamoja na upotofu wa makanisa ya Ukatholiki wa Kigiriki na Kirumi, Mfalme Constantine akiwa na mtazamo tofauti na ukweli wa Mungu akawa msaidizi mkuu wa kanisa la Kikatholiki na kuligeza liwe ni dini ipendayo kupigana vita kila mara.

Wanahistoria wanatambua kwamba haya yanayodaiwa kuwa ni maono, yakiambatana na ndoto ambapo Constantine alidai kutokewa na Yesu, vilibadiri historia ya ulimwengu. Mfalme Constantine, binafsi, aliyashukuru maono yake hayo na akaamini kwamba baadhi ya mambo ndani ya himaya yake walipaswa kubadirika.

Constantine akawa amesimika sheria ya kwanza ya kuabudu Siku ya Jumapili, akatangaza kupambana na yejote atakayekataa kuipokea dini yake, akawapa madaraka makubwa maaskofu wa makanisa ya Kigiriki na Kirumi, na akaongeza kwa kiwango kikubwa kuabudu sanamu pamoja na wakristo kujunga na jeshi. Vilevile alipokonya mali kadhaa za Kanisa la Mungu na akaagiza Wakristo wa Kanisa la Mungu walioko Yerusalem wauawe kwa kukataa kula nguruwe.

Wakatholiki wa Kirumi na Kiorthodoxi ya Mashariki walimpa jina la Constantine Mkuu kwa kuifanya dini yao iwe ndio pekee inayotambuliwa kisheria katika Milki yote ya Rumi. Upotofu mwengine wa mafundisho ya kiimani ultokea kupitia kwake na hata baada yake. Na elewa kuwa moja wapo ya upotofu huo ulikuwa ni kuamini maono. Ilielezwa pia kwamba kadri ya miaka miwili tu kabla, Constantine alitokewa na mzuka wa muungu jua aitwaye "Sol" alipokuwa kwenye msitu wa Apollo kule Ufaransa, mwaka 310 B.K. (imeandikwa katika makala ya: Rodgers, Barbara S. "Constantine's Pagan Vision,"*Byzantium*, vol. 50, 1980, pp. 259–78). Hili sharti litufanye tutafakari na kugundua kwamba, Constantine alikuwa na historia ya kuwa na mawasiliano na mapepo, japo wengi wamelipuuzia hili!

Hata baada ya kile kilichodaiwa kuwa ni kuongoka kwake katika kuingia kwenye aina yake mwenyewe ya imani ya Kikristo mnamo mwaka 312 B.K., (ikiwa aliwahi kubatizwa kabisa, basi itakuwa ni pale alipokuwa amelala kitandani akifariki mnamo mwaka 337 B.K., ingawa alijitangaza mwenyewe kuwa ni "Askofu wa Kikristo" aliye mlei, hapo mwaka 325 B.K.), Bado Mfalme Constantine alimeendelea kumuweka muungu wake jua "Sol" kwenye sarafu za fedha zake. Hapa jionee moja ya sarafu hizo ya mwaka 317:



Photo copyright 2008 Reid Goldsborough. Used with permission

Maeleo ya Kilatini: "SOLI INVI-C-TO COMITI", maana yake katika Kiswahili ni "Katika utukufu wa Jua (muungu) lisiloweza kutekwa". Ni wazi kwamba katika mwaka 317 B.K. (ambapo ni miaka mitano tangia adai "kuongoka"), Constantine bado alikuwa akiendelea kuliabudu jua—muungu wake "Sol" waziwazi, ambaye pia alijulikana kama Mithras (muungu—jua wa vita). Hili pia linapaswa liwe ni uthibitisho kwa wote kwamba, maono na mizuka yake hayakuwa yametoka kwa Mungu, bali pamoja na haya yote, bado wanaimani wake wangali wakimuita kuwa ni Constantine Mkuu.

Hili linawezekanaje?

Mtume Paulo aliasa kwamba Wakristo wa kweli "wangeenenda kwa imani, siyo kwa kuona" (2 Wakorintho 5:7), lakini wengine yaonekana hulipuzia hili na kupendelea kuamini uongo ambao wangeweza kabisa kuuthibisha kwamba si kweli (Soma: Ufunuo 22:15).

Katika Biblia inaonyesha kwamba wengi wangepokea ishara na maajabu mengi ya uongo (yakiwemo maono na mizuka, soma: Ufunuo 16:14) kwa sababu tu hawana "upendo wa ukweli" (2 Wathesalonike 2:9). Pamoja na kwamba Yesu alisema kuwa Neno la Mungu lilikuwa kweli (Yohana 17:17), wengi hupenda kuongozwa na fikra zao dhidi ya ukweli wa Biblia na wanaipokea injili ya uongo. Inasikitisha kwamba swala hili limekuwa likijirudiarudia na kuwa ndio mwelekeo katika historia nzima.

## **Maono ya Mizuka yameiathiri zaidi Historia: Urusi**

Madai ya kutokewa maono yamehusika katika upotofu katika enzi zote za Kanisa. Kadri muda ulivoyzidi kupita, madai ya kuona mizuka inayodaiwa kuwa ni Maria imezidi kuongezeka. Hili limeonekana kuwa ni swala lililosababisha wengi katika Ulaya na Afrika ya Kaskazini kuwafanya waipokee dini ya Kigiriki na Kirumi, badala ya imani ya kweli ya Kanisa la Mungu katika nyakati za enzi za karne za kati.

Lakini hata na maeneo mengine ya kijiografia nayo pia yaliathiriwa. Taasisi ya Kikatholiki ya Utafiti wa Maria (Catholic Marian Research Institute) imetoa taarifa kwamba kumekuwepo zaidi ya matukio 2,000 ya watu kuzukiwa na kinachoitwa Maria. Taasisi inaeleza kwamba kulikuwa na matukio karibia 800 enzi za karne ya 13 pekee—jambo linaloonyesha kwamba Ulaya ndio imekuwa na idadi kubwa zaidi ya hayo matukio, kitu kilichoifanya iathiriwe zaidi. Fafanuzi nyingi za Kikatholiki za kinabii zimetokana na maagizo ya mizuka iliyowatoka kupitia maono, hususani ile iliyodaiwa kuwa ni ya Maria, lakini hata kwa ile pia iliyodaiwa kuwa ni maono ya kutokewa na Yesu.

Kusema kweli, siyo Wakatholiki wa Rumi pekee ambao ndio wamedai kutokewa na mizuka hiyo ya maono. Wakati wa karne ya 14, Sergius wa Radonezh (Urusi) inataarifiwa kwamba alidai kuwa aliona maono ya kile kilichodaiwa kuwa ni Maria.

Pamoja na kwamba Urusi ilikuwa na aina za imani potofu juu ya Maria hata Kabla ya hapo, inaelezwa kwamba Sergius ndiye alikuwa "mwanaharakati mkuu" wa kuifanya Urusi ipokee imani ya Ukatholiki wa Kiorthodoxi na ni yeye pia "aliyesaidia kueneza katika Urusi yote" umaarufu na "matumizi" ya "michoro kwenye

majumba ya ibada—icon paintings”.

Lakini kuamini juu ya maeneo (icon) fulani kuwa ni matakatifu na kuyatkuza hapo awali haikuwa ni desturi ya kanisa, na aina hiyo ya michoro inasemekana hapo awali ilipingwa na watumishi wa Mungu. Hivyo, hakuna mantiki yoyote kuchukulia kwamba Sergius kweli alitokewa na Maria wa kweli wa kwenye Biblia. Sergius alikufa mwaka 1392.

Ulogaji (Ulozi)/uchawi pia yaonekana ulitumiwa na Sergius kwani “mzoga wake usioharibika” (sehemu ya maiti yake ambayo “haukuoza”) iligunduliu mwaka 1422 (baadhi ya Wakatholiki huamini kwamba, iwapo maiti haitaharibika kwa muda fulani baada ya kufariki kwa mtu, na mtu huyo alionyesha kuishi maisha kamili ya Kikatholiki, basi hilo ni ushahidi kuwa mtu huyo amefanyika “Mtakatifu”). Sergius anachukuliwa kuwa ni mmoja wa “Watakatifu” muhimu katika Kanisa la Kiorthodoxi la Urusi na hili pia lilitokana na kudaiwa kuwa maiti yake ilichelewa kuoza na uonaji wake wa maono.

## “Guadalupe” pamoja na Amerika ya Kusini

Moja wapo ya mizuka muhimu kudaiwa kuwa ni kutokea kwa Maria katika historia ni ule uliozuka kule Mexico wakati wa karne ya 16, ujulikanao kama “Mama Yetu wa Guadalupe”.

Taasisi ya Utafiti wa Maria iliandika:

Zama za Kati (Renaissance): Wakati wa karne ya kumi na sita, kulanza aina mpya ya kuzukiwa na maono. Mizuka hii ilikuwa na mwelekeo wa kutokea jamii na ilikusudiwa “kuifufua imani” na “kuyaongeza majanga ya ulimwengu”. (Laurentin 88) Tukio muhimu ni lile la Guadalupe (1531) ambalo “lilizaa kanisa jipya kwenye bara jipya” (Laurentin 88).

Gundua kwamba kulikuwa na mabadiriko katika aina ya maono katika nyakati za karne ya 16. Gundua pia madai kwamba mizuka wa “Guadalupe” unajulikana kuwa “ulizaa kanisa jipya kwenye bara jipya”.

Antonio Soccia iliandika:

Mzuka wa Guadalupe—kulingana na wanahistoria wengi wanavyokubaliana—ndicho kitu kilichowavuta Wahindi Wekundu kuingia kwenye Ukristo. Hivyo, ilikuwa ni Guadalupe yenyewe ambayo ilipelekeaa kuanzhishwa kwa Ukristo wa Amerika ya Kusini. (Imenukuriwa toka: Soccia A. The Fourth Secret of Fatima. Loreto Publications, English Translation 2009, p. 143).

Dr. Jeanette Rodríguez, Msomi wa Kikatholiki iliandika:

Juan Diego...alisema, “Anajiita ‘Tlecuauhltacupeuh’”. Kwa Waspaniola hili lilisikika kama “Guadalupe”... Lakini lugha ya Wahindi Wekundu ya Nahuatl huwa haina herufi “d” wala “g”; hivyo jina la mama yetu lisingeliweza kuwa “Guadalupe”... Uelewa wa wa-Nahuatl wa “Tlecuauhltacupeuh” ni La que viene volando de la luz como el águila de fuego (mama ajaye akiruka kama jeshi

la mwanga, kama tai wa moto, Echeagaray 1981:21). Jeshi la mwanga ndilo lilolokuwa mahali pa kuishi pa miungu ya Wahindi Wekundu waitwao Aztec, na tai alikuwa ndiyo ishara itokayo kwa miungu. (Imenukuriwa toka: Rodriguez J. ‘Our Lady of Guadalupe: faith and empowerment among Mexican-American women’. University of Texas Press, 1994, pp. 45-46).

Hivyo, mzuka huo waonekana kwa kiasi kikubwa kuwa ni kama muungu mke wa Wa-Aztec. Fuatilia pia kifuatacho:

Bikira wa Guadalupe alitokea kule ambako kwa sasa ni Jiji la Mexico City kwenye kilima kiitwacho Tepeyac, kilichokuwa kimewekwa wakfu kwa Tonantzin, muungu Mama wa Nchi wa Wa-Aztec. Hiyo ndiyo sababu kubwa iliyomfanya askofu asimwamini Juan Diego. Yamkini aliwaza: “Tunamjua siku zote ni nani hutokea kwenye kilima hicho naye siyo Bikira Maria bali ni muungu wa kipagani!” Kusema kweli, hata wenyeji wa Kimexico ndicho walichofikiri: “Tunamjua atutokeaye kwenye hicho kilima: ni Tonantzin!” Na ndipo wakamuita huyo tumuitaye ‘Bikira wa Guadalupe’ kuwa ‘Tonantzin’ kwa zaidi ya karne nzima. Hadi kufikia leo, wa-Mexico wanajua na humuita huyo Bikira wa Guadalupe kuwa siyo aina nyingine ya Mama Maria, bali ni yule yule Malkia wao wa Mbingu wa Ki-mexico. (Kutoka: Rozett E. Mother Mary and the Goddess. [http://www.interfaithmary.com/pages/mary\\_goddess.html](http://www.interfaithmary.com/pages/mary_goddess.html) viewed 04/07/2011).

Imekuwa ikidaiwa kwamba “Tonantzin, muungu mke wa wa-Aztec, kuanzia hapo alichukua muonekano wa Bikira Maria. Hivyo Tonantzin alibadirishwa awe...kwa ajili ya umuhimu wa kuwaongoa watu wa Amerika ya Kusini waliokuwa chini ya mamlaka mpya ya kisiasa waingie kwenye dini ya Ukatholiki”. (Toka: Breaux JJ. Intransigence & Indifference: Essays Concerning Religion and Spirituality. Lulu.com, 2008, p. 85).

Si kwamba tu mzuka huo ulikuwa ni upagani na wala siyo maono ya Maria (mama wa Yesu), bali pia awali ulikataliwa na kупингва na askofu wa eneo hilo kisha baadaye ukapokelewa!

Wengi hudai kwamba kuibuka kwa maono ya mzuka huu kulipelekea wengi katika Amerika ya Kusini waupokee Ukatholiki wa Rumi, ambao hadi leo wengi huko Amerika ya kusini bado wameukumbatia. Mzuka huu umefanywa mashuhuri zaidi na Papa Francis ambaye ameubariki mwaka 2013. Papa Francis kadharika hivi karibuni ameubariki aina nyingine za mizuka iliyobuka na kudai kuwa ni maono ya Maria, pale alipoitembelea hivi karibuni nchi kubwa zaidi katika Amerika ya Kusini ya Brazil, mwaka 2013.

## Maonyo kutoka Kanisa la Kiorthodoxi ya Mashariki

Ifuatayo ni taarifa ilioandikwa na kiongozi mmoja wa Kanisa la Kiorthodoxi akiwaonya watu dhidi ya mizuka kwamba maono ya uongo yakidai kuwa ni ya Maria yatawapeleka watu kwa MpangaKristo:

“Miungu wa kike” walioaminiwa na kujulikana enzi za

ulimwengu wa kale hawakuwa wanapatikana katika maeneo ya Mashariki ya Kati na Mediterrania pekee bali imani hiyo ilitapakaa kila mahali. Wahindi Wekundu wa kabilia la Kogi, ambao mionganoni mwao tulishi huko Columbia, waliiabudu roho ilipoitwa Nabuba, yaani "Mama wa Kale". Pale wamisionari wa Roman Katholiki walipajaribu kuwahubiri injili hawa Wakogi enzi za karne iliyopita, hawakutumia mbinu isiyo ya kawaida kwao katika kuwavuta wapagani wajiunge na umoja wa kanisa la Roma: badala ya kuwaelezea tofauti iliyopo baina ya imani za kijadi ya upagani na ukweli wa Ukristo, walitafuta "mifanano", chochote kilichokuwepo katika imani za wapagani hao kikalinganishwa na kuwa kiwakilishi cha Kristo, katika mtazamo huu wa imani ya ajabu, mifanano na "Kogi Sejukukui" (muungu mjuzi wa mazingaombwe ambaye hata alidanganya kwamba amekufa kumbe amejificha katika pango), wakati Nabuba anasemwa ndiye Bikira Maria. Mparanganyiko huu umewasababishia Wahindi Wekundu wa Kikogi kuliita hekalu lao la kipagani "cansamaria", kifupi cha "casa de Maria" (nyumba ya Maria).

Kwa "mbinu hizi za uinjilisti" za kanisa la Roman Katholiki za zaidi ya karne nzima iliyopita, je kuna ajabu yoyote kwamba mizuka inayodaiwa kuwa ni maono ya Maria huandamana na mahubiri yanayodai kwamba dini zote zinamlenga Mungu yuleyule na kwamba Ukristo ni mojawapo mionganoni mwa "njia" hizi nyingi ziongozazo kwa Mungu huyo? Makala ya hivi karibuni iitwayo "Orthodox Tradition" (1966) ina maelezo ya Matushka (mke wa kuhani wa Kirusi wa kanisa la Kiorthodoxi) safari ya Katherine Swanson kwenda Medjugorje, Croatia, kufanya uchunguzi wa tukio la hivi karibuni la mzuka uliodaiwa kuwa ni maono ya Maria na Kanisa la Roman Katholiki. Katika makala hii anatoa maelezo jinsi tukio hilo lilivyokuwa:

Mwongozaji wetualilongoza kundi letukwenda kuonana na "wapiga ramli". Wakati wa kuzungumza nao, mmoja wetu alimwuliza mmoja wa watoto wa huko maswali yafuatayo: "Je, Bikira anapowatokea hueleza ikiwa kanisa Katholiki ndilo kanisa la kweli?" Majibu aliyotoa yule mtoto yanatoa ushahidi wazi juu ya kuunganishwa kwa dini zote pamoja na kufanana kwa dini ambako, cha kushangaza, kumeongeza "mahusiano" baina ya dini mbalimbali huko Medjugorje: "Mbarikiwa Mama yetu anasema kwamba dini zote zinampendeza Mungu kwa hali iliyosawa".

Makala iliyoandikwa katika gazeti la "Life magazine", nalo linachangia katika mtazamo wa aina hii. Kwa wazo kwamba njia zote ni sahihi na sawa, basi na mizuka yote ya maono ya akina Maria nayo pia ni sahihi na sawa. Mwandishi kupitia makala hii anaafanua matukio kadhaa ya kutokea kwa Maria katika enzi zetu: Maria wa Miujiza (kama yule wa Medjugorje), Maria Mpatanishi (Ambaye, kulingana na mwandishi alivyonukuru Fr. Andrew Greeley akisema, "huwapeleka watu mbinguni kwa kupitia "mlango wa nyuma"). Maria Mpatanishi wa akina mama, na Mama Maria. Huyu wa mwisho, Mama Maria, ni jukumu ambalo mwandishi analichukulia kuwa ndilo lenye mvuto zaidi kwa wasio Wakatholiki: "Mvuto wake wenye hisia kuu ni

mgumu sana kwa ulimwengu uliojaa machafuko kuupuuzia kiasi kwamba watu ambao hawakuwa na uhusiano na Bikira hapo awali wanavutwa kwake. Inajulikana kwamba Waislamu wanamheshimu Maria kuwa ni mtakatifu na mwenye heri...vikundi vya sala vya kumuomba Maria vya watu wa dini zote vimeanza kuibuka ulimwenguni kote. Wengi wenye imani za Kiprotestanti, hata na baadhi ambao wangali wakipinga juu ya uwepo wa Bikira wa miujiza, wanapitwa na fursa hii ya Maria."

Waislamu na Waprotestanti wanavutwa kwenda kwa Maria yupi? Matengenezo ya Kiprotestanti yalianziswa yakipinga mtazamo batili juu ya Maria uliokuwa umeibuka katika nchi za Magharibi na kuleta mtengano kuanzia mwaka 1054, mtazamo uliopelekeea Kanisa la Roma kutangaza imani yao ya "Bikira alizaliwa akiwa amekingiwa dhambi". Lakini si kwamba Waprotestanti walipingana na mtazamo huo wa kimagharibi kuhusu Maria pekee; vilevile ulimpuuza kabisa, ukipinga juu ya kuwa analo jukumu katika kupokea mili mipywa wakati wa ufufuo, wala juu ya sehemu anayotekeleza katika kuleta wokovu. Kadri Roma ilivyozi kumchukulia kuwa ni sawa na "muungu wa kike", mhimiili wa nne wa Utatu Mtakatifu, hilo liliwafanya Waprotestanti wachemke kwa kuba fulsa yake na kukataa kumheshimu kabisa, hili ni hata ingawa Injili inaeleza: "Vizazi vyote vitaniti Mbarikiwa".

Siku hizi, kadri wale Wakristo waliokuwa wa mlengo wa imani ya aina moja wanapozidi kuukubali umoja wa madhehebu na kuwa tayari kuanzisha "Kanisa Moja", kumtafuta Maria anayekubalika na ulimwengu wote kumeanza, ambaye atawavutia si wale ambao wanaitwa Wakristo pekee, bali pia hata na Waislamu na hata wengine pia, sawa na jitihada ambazo zimeanza za kumtafuta "Kristo mpya" aendanaye na mtazamo wa Waislamu wa kuja kwa Mahdi pamoja na mtazamo wa Wayahudi wa Masihi ambaye bado wanamngojea aje. Huyu, kusema ukweli hatakuwa Kristo hata kidogo bali atakuwa ni yule mpingaKristo. (Jackson P. ORTHODOX LIFE., No. I, 1997, Brotherhood of Saint Job of Pochaev at Holy Trinity Monastery, Jordanville, N.Y. pp. 18-22. <http://fr-d-serfes.org/orthodox/theotokos.htm> viewed 05/11/09).

Kwa kuwa Waislamu wanakubaliana na Bikira kuzaa na humtukuza Maria (Yaonekana Maria ndiye mwanamke pekee aliyetajwa katika Korani na ametajwa mara nyingi zaidi kuliko Yesu), ni dhahiri wataipokea dini ya umoja wa madhehebu ambayo Biblia inaeleza kwamba inakuja (Ufunuo 13:4, 8). Mizuka ya matokeo ya Maria yawezekana nayo itakuwa ni sehemu ya ishara na miujiza ya uongo iliyotabiriwa kutokea nyakati za mwisho (2 Wathesalonike 2:9-12) ambayo itawadanganya wote isipokuwa wateule pekee (Mathayo 24:24).

Maono ya mizuka yamehusika na athari kwa wengi na kwa muda mrefu yamekuwa ni sehemu ya mipango ya Shetani. Kama Wakristo, tunatakiwa kuwa makini na Shetani kiasi kwamba "tusikose kuzijua hila zake" (2 Wakorintho 2:11).

## Hitimisho

Mungu ametumia nabado atatumia watu kutokewa na maono hapo baadaye. Maono yalihusika na Yesu na pia na Kanisa la Mungu. Matumizi yajayo ya ujumbe kutoka kwa kadri ya malaika watatu (malaik pia wanahusika kwa kiwango fulani kulingana na Kitabu cha Ufunuo) ni moja wapo ya mpango wa Mungu wa kipindi cha siku za mwisho wa kuihubiri injili kwa ulimwengu kama usuhuda.

Pamoja na hayo, wengi yaonekana kuwa hawaelew i jinsi Mungu alivoyoyatumia maono. Wengi wanaona woga kufikiria kwamba viumbe nya kiroho bado vinawenza kuwa sehemu ya mpango wake. Lakini Biblia iko wazi kwamba ni sehemu ya mpango wake (soma: Ufunuo 14:6-11).

Hata hivyo, katika hatua zote za historia ya Kanisa la Mungu, Shetani naye pia ametumia maono ili kupunguza kushamiri kwa Ukristo huku akijitahidi kuongeza kushamiri kwa imani za Ukristo batili wa Kigiriki na Kirumi. Shetani amepata mafanikio makubwa kwa kutumia mizuka ilijoitokeza kama maono ya Mungu.

Mizuka ilijoitokeza ikidai kuwa ni maono yaliyotumwa na Mungu ilichangia katika kuibuka kwa dini za ukristo wa Kigiriki na Kirumi, enzi za karne ya tatu kule Asia Ndogo. Katika karne ya nne ilichangia katika mabadiriko makubwa mionganoni mwa Milki ya Rumi ya kale. Katika karne zilizofuata, kule Ulaya na Afrika, nao pia walathiriwa. Wakati wa karne ya kumi na mbili kule Urusi mizuka iliwaathiri kwa kiwango kikubwa. Wakati wa karne ya kumi na sita Amerika ya Kusini ilibadirishwa. Kumekuwepo na madai juu ya kutokewa na mizuka hiyo ya Maono ya Maria katika maeneo mbalimbali katika nyakati zote za kanisa, ambayo yamesababisha athari kubwa.

Kwa kuwa Shetani ametumia kutokewa kwa mizuka kwa mafanikio ikiwa ni sehemu ya mpango wake huko nyuma, ninahisi kwamba anapanga kuitumia tena kwa kiasi kikubwa. Na yaonekana kwamba atafanya hivyo, na kufanikiwa kwa muda mchache, kulingana na 2 Wathesalonike 2:9-12 (mengi juu ya hili yanapatikana katika makala iitwayo: Fatima pamoja na Maono mengine ya 'Mizuka ya Maria', iliyomo kwenye toleo hili).

Ni wachache ndio wanaonekana kutambua kiwango cha athari ambacho mizuka imesababisha.

Sisi katika kanisa la Continuing Church of God tunatambua kwamba Mungu anaweza na atatumia maono, lakini pia tunatambua kwamba Shetani amekuwa akitumia na yaonekana atatumia mizuka kama mbadala wa maono ya Mungu hapo daadaye. Mizuka ambayo ni maono ya uongo yatokayo kwa Shetani ni sehemu ya mpango wake wa udanganyifu, wakati maono halisi yanabaki kuwa ni sehemu ya mpango wa kweli wa Mungu.

## KILICHOTOKEA KULE FATIMA NI NINI?



Madhabahu ya Fatima, Ureno

Na Bob Thiel

Mnamo Mei 13, 1917, Mzuka wa kike uliojitetangaza kuwa ni "Bibi" na kuwa ni "Bibi wa Rozari" ulyanza kutokewa kama maono ya kila mwezi ukiwatokea watoto watatu kule Fatima, Ureno. Fatima lilikuwa ni jina la binti kipenzi wa mwanzilishi wa Uislamu Muhammedi, na mji huo ulipewa jina hilo kama heshima kwa malkia wa Kiislamu wa mji huo aliyeitwa Fatima ambaye baadaye alibadiri dini na kuwa Mu-Romani Katholiki.

Ni nini kilitokea huko Fatima mwaka 1917?

Kwa hakika hakuwa Maria, mama wa Yesu. Vigezo kadhaa, ikiwemo jinsi mzuka ulivoyotokea, unaondoa uwezekano kabisa wa kwamba maono hayo yalikuwa ni yeye. Mzuka uliotokea ulikuwa ni pepo lenye umbile la kike. Tukio hili limeonekana kuwa ndilo mashuhuri zaidi mionganoni mwa maono ya mizuka yaliyotokeza katika karne ya 21.

Tofauti na wengi mionganoni mwa Wakatholiki waaminivyo, huyu "Bibi wa Fatima" kamwe hakuwahi kujitangaza kwamba yeye alikuwa ni Maria, mama wa Yesu. Hata na maono mengine mengi ya mizuka mashuhuri mionganoni mwa ile ikubaliwayo na Wakatholiki kuwa ni ya maono ya "Maria" nayo vilevile haikuwahi kujitangaza kwamba ilikuwa ni Maria.

### Kilichoonekana ni Nini?

Kuanzia tarehe 13 Mei, 1917, watoto watatu (Lúcia dos Santos, miaka 10; Jacinta Marto, miaka 7; pamoja na Francisco Marto, miaka 9) walidai kwamba waliona aina furani ya maono ya mwanamke mara sita, mara moja kila mwezi. Kuzuka kwa kitu hicho kwa kila mwezi kukahitimishwa na tokeo pale makumi ya maelfu ya watu walioenda kushuhudia walidai kushuhudia namna ya "mwujiza"/kubadirika kwa anga hapo tarehe 13 Oktoba, 1917.

Yule mtoto mkubwa (Lúcia) akiwa na kasisi wake (Manuel Marques Ferreira), mwanzoni na ni kwa usahihi walidhani kwamba mzuka huo ulikuwa ni wa kutoka kwa Shetani, kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo muonekano wake wa kutisha.

“Bibi” aliyewatokea hakuwa amevaa mavazi ya heshima, bali nusu uchi kiasi kwamba hata makahaba wa enzi za miaka ya 1917 kule Ureno walikuwa hawawezi kujiachia nusu uchi hivyo:

Mahojiano baina ya kasisi wa parokia hiyo na wale watoto walioyaona maono hayo yaliandikwa katika ripoti. Mahojiano haya ya kwanza yaliyanywa na kanisa na yanaweza kusomwa katika kitabu kitwacho: Os Mouros Fatimidas e as Aparicoes de Fatima...Kitu cha ajabu kuhusu tukio la mzuka wa kwanza ni kuwa wale watoto walidai yule Bikira alikuwa amevaa siketi isiyovuka magoti na kwamba alikuwa amevaa soksi nyeupe; kinyume kabisa na jinsi mizuka mingine ya Bikira iliyotangulia ilivyowahi kuva. Alikuwa amevaa mkufu wenye medali...macho yake yalikuwa meusi jambo ambalo linamfanya asiwe na macho ya wazungu wan chi za Magharibi kama Maria mama wa Yesu alivyokuwa. Maelezo haya yaliwfanya wengi wa wakazi wa eneo hilo kudai kwamba Bibi huyo alikuwa ni binti wa Muhamadi aliyetwa Fatima, wala si Bikira Maria. Baadaye Kanisa liliwashawishi watoto hao wabadiri maelezo na kusema kwamba alionekana sawa kabisa na aonekanavyo kwenye sanamu na picha za Maria zilizomo kanisani na alikuwa amevaa vazi refu. Siketi fupi ilichukuliwa kuwa ni udhalilishaji na aibu. (Imenekuriwa toka mtandao: Fraud at Fatima. <http://www.miraclesceptic.com/fatimafraud.html> 04/26/11).

Mwaka 1917, kasisi wa parokia hiyo, Manuel Marques Ferreira, alifanya mahojiano na watoto hao, maelezo ya mahojiano hayo yaliripotiwa kwamba Bibi aliyewatokea alionekana:

Mavazi yake alikuwa amejifunika nguo nyeupe, ambayo ilianzia kichwani na kufika chini kidogo ya kiuno ikifunika siketi kiunoni, ambayo ilikuwa ni ya rangi ya dhahabu kuanzia kiunoni hadi kuvuka mishipi miwili aliyokuwa amejifunga, mishipi iliyokuwa mmoja juu na mwingine chini ya upindo. Siketi yote ilikuwa nyeupe na ya dhahabu... na ilifika juu ya magoti pekee; alivaa joho jeupe...hakuwa amevaa viatu, lakini alivaa soksi nyeupe zisizo za dhahabu; shingoni mwake alivaa mkufu wa dhahabu wenye medali iliyochongoka. (Imenekuriwa toka makala: Interrotagórios de Artur de Oliveria Santos, Doc. 53, Documentação Crítica de Fátima I. Fátima Sanctuary, 1992, Ukurasa wa 375 kama ulivyonukuriwa na kutafasiriwa na Fernandes J, D'Armada F. Siri toka Mawinguni: Historia iliyojificha ya Tukio la Fátima. Anamolist Books, San Antonio (Texas), 2006, Ukurasa wa 152).

Watoto hao pia baadaye walihojiwa na Kasisi wa Kikatholiki Canon Manuel Nunes Formigão, ambaye ripoti yake ilieleza kwamba:

Jacinta anathibitisha kwamba vazi la Bibi yetu liliishia juu ya magoti pekee... Bibi yetu asingeweza kututokea akiwa amevaa tofauti na mavazi ya heshima na yasiyo dhalilisha...

Hili linaleta tatizo kubwa, likipinga uhakika wa Maono haya, likiibua katika roho woga kwamba swala hili lote ni utatanishi, ulioandalowiwa na Mfalme wa Giza mwenyewe. (Toka: Fernandes, Ukurasa wa 153; pia na Santo ME. Os Mouros Fatimidas e as Aparições de Fátima. Assírio & Alvim, 2006, kurasa za 271-218).

Hivyo angalau makasisi wawili wote mwanzoni waliarifu kwamba watoto wawili mionganii mwao walidai kwamba kile kilichotokea kule Fatima kilivaa siketi fupi. Siketi ambayo kwa kiwango cha watu wa Ureno wa miaka ya 1917 ilikuwa ni aibu na udhalilishaji isiyostahili mwanamke kuva hivyo (huyo “Bibi” aliyewatokea alionekana kufanana na muungu wa kike Diana). Haiwezekani kabisa kwamba Maria wa kweli angetokea akiwa katika hali hiyo (soma: 1 Timothy 2:9). Hivyo, wakati tukio la Fatima siyo kitu cha kubezwa kwamba hakikutokea, bado linapaswa kuchunguzwa kwa uangalifu mkubwa kwa kuwa haiwezekani kabisa mama wa Yesu akajitokeza katika hali kama ile.

Pamoja na kuyaelewa haya, bado kanisa liliamua kujenga madhabahu kubwa kwenye eneo hilo yenyen majengo kadhaa. Madhabahu ya Fatima ni eneo kubwa kiasi linakumbusha juu ya jiji la Vatican.

Jarida la juu la makala ya gazeti hili la Habari za Unabii wa Biblia linaonyesha sanamu kubwa ya kuchongwa iliyoko kwenye sehemu ambapo mizuka ya Fatima ilikuwa ikitokea. Mwonekano wa sanamu hiyo yaonekana ndivyo ambavyo Wakatholiki wengi wanapenda kuamini ndicho kilichotokea kule Fatima (kwa kuwa ndivyo wengi wamefanywa waamini). Ukweli ni kwamba ile picha iliyopembeni mwake, yenyen siketi fupi, kwa kweli ndiyo inayowakilisha maelezo sahihi yaliyotolewa na watoto hao watatu walioshuhudia na kueleza namna “Bibi wa Fatima” alivyoonekana. Sanamu hiyo haikuwa ya Maria, ingawa ni ya mzuka uliovalia siketi fupi uliotokea mwaka 1917.

Baadhi, inasikitisha kwamba hupenda kuuamini uongo (soma: Ufunuo 22:15) kwamba Maria mama wa Yesu alijitokeza kule Fatima na kwamba alitoa ujumbe toka kwa Mungu kwa ulimwengu—jambo kama hili, wakati wale ambao hawana “upendo wa ukweli” watajikuta wanauamini uongo jambo ambalo litatokea tena (2 Wathesalonike 2:9-12).

Mamillioni huitembelea madhabahu ya Fatima kila mwaka, wengi wanaamini kwamba ni mama wa Yesu ndiye aliyetokea huko. Wanaamini alitoa jumbe za kinabii ambazo zimetimizwa na zingine ambazo bado zitatimizwa baadaye. Lakini, Biblia haitamki kabisa kwamba Maria, mama wa Yesu, angekuwa na jukumu katika kufanya maono ya kimiujiza baada ya kufariki kwake ambayo yangesababisha nabii kubadirika ama mafundisho ya kanisa kugeuzwa.

(Taarifa kadhaa alizozileta huyo “Bibi wa Fatima” nazo pia ziliikuwa ni za makufuru na tutaweza kuzielezea kwenye makala zizazo za gazeti hili).

## Fatima na Dini Zingine

Dini zingine zisizo za Kikatholiki, nazo zimejihuisha na Fatima.

Ijapokuwa Maria siyo sehemu ya dini ya Kibudha (Buddhism), kiongozi wa Wabudha wa Kitibeti, Dalai Lama, alisali kwenye kanisa dogo lililopo Fatima mwaka 2001 alipotembelea eneo hilo. Watu wa imani za kipagani nao wamevutika kwa "miungu wa kike" wanaopendwa na wengi, na hivyo ndivyo wanavyomchukulia "Bibi wa Fatima."

Pamoja na madai ya Wakatholiki, Waislamu fulani wao huamini na wanadai wazi kwamba ilikuwa ni binti wa Muhammedi Fatima ndiye aliywatokea wale watoto kule Fatima mwaka 1917, hivyo baadhi ya Waislamu nao wanachukulia eneo hilo kuwa ni takatifu na wakati mwingine hulitembelea. Endapo hapo baadaye kutaibuka mizuka ikidai ni maono na kusema chochote moja kwa moja kwa Waislamu huko Fatima ama kwingine, hilo linaweza kuwa ni swala muhimu katika kuwafanya Waislamu, japoqua hata kwa muda, wakubaliane na mamlaka ya Mnyama (soam: Ufunuo 13:4,8).

Wahindi waumini wa dini ya Kihindu (Hindus) kwa muda mrefu wamevutwa na mizuka inayodai kuwa ni Maria ikiwemu na sanamu zake. Wahindu waliruhusiwa na viongozi wa Kikatholiki waendeshe sherehe yao ya kipagani ya kumwabudu Bibi wa Fatima kwenye eneo la Madhabahu ya Fatima tarehe 5 Mei 2004. Pamoja na kwamba hili liliwaudhi baadhi ya Wakatholiki, kwa kuwa liliruhusiwa na viongozi ni ushuhuda kwamba Wakatholiki wengine nao wataafiki, matumizi ya "Maria", na/ ama matumizi ya aina kama hiyo yasiyo sahihi ili kuendeleza ajenda yao ya umoja wa madhehebu.

Jionee pia taarifa juu ya 'Maria' kuhusu India:

"Mama Maria anaheshimiwa kwa upendo mkubwa mionganoni mwa jamii za Kihindi akichukuliwa kuwa ni mama na mlinzi wa akinamama, alisema Mhubiri Jayaseellan Pitchaimuthu...Mhubiri huyo alieleza kwamba siku ya sikukuu ya Maria inaumuhimu na umaarufu mkubwa katika mtazamo wa Wahindi kwa sababu ya kuhusika kwake na imani zingine.

Waumini wa dini zingine, ikiwemo Wahindu na Waislamu, "huchukulia maombi kwa Maria kwa heshima kubwa," alisema. Maelfu ya wanaomcha; "wote Wakatholiki na wasio-Wakatholiki", humiminika kila juma kwenda kwenye eneo la kutokea kwa Maria lililoko Velankanni, karibu na Chennai, Kusini mwa India, pamoja na kwenye maeneo mengine ambako miujiza kadhaa imetokea, alisema. Mhubiri huyu alifafanua kwa namna hii: "Ibada kwa Maria kadharika zinaongoza kwenda kwenye uwanja wa makubaliano baina ya dini mbalimbali". (Imenekuriwa toka: Gonzales AA. Indian migrants in Holy Land prepare for Marian feast. (<http://www.catholicnewsagency.com/news/indian-migrants-in-holy-land-prepare-for-marian-feast>).

Sio wote wanaliunga mkono hili. Wengi wanamashaka. Askofu Kennedy wa kanisa la Celtic Orthodox Church aliandika kwamba Fatima lilikuwa ni tukio la kiulaghai:

Mdanganyifu mkuu wa Fatima anaahidi wokovu kwa wale watakaofanya maombi kwa Moyo Mtakatifu wa Maria... Hili linatufanya tuwe na uhakika kwamba Mungu hajamtuma

Maria aje duniani kuja kubadiri mpango wa Miungu wa milele wa wokovu. Ni aina hii yan udanganyifu iletayo maelezo ya uongo kuhusu Maria; kwamba ni Mpatanishi wa neema zote n.k. Udanganyifu wa ibilisi unaonekana kwa kiuwango kikubwa ndani na nje ya kanisa kadri inavyoshuhudiwa kupitia idadi ya nafsi zenye nia njema lakini zilizodanganyika zinazotangaza kwamba Maria ni Mpatanishi wa neema zote. Taarifa kama hiyo ingeelewekaje kama ingetamkwa kwa Mitume? Wokovu huu tunaoufurahia umetoka kwa Mungu kupitia katika Kristo; "Mwana wa Adamu Yesu Kristo, aliyejitoa ili awe sadaka kwa wote". (1 Timotheo 2:1, 3-6)... Tunapaswa KUMZUIA IBILISI katika jitihada zake kwa kutangaza wazi maono ya Fatima yalikuwa ni hila na ulaghai, ni kazi ya Ibilisi na ni machukizo kwa Mungu, kwa Maria na kwa Kanisa. (Imenekuriwa toka: Kennedy BJ, Bishop. The Fatima Affair. <http://www.celticorthodoxchurch.com/fatima.html> viewed 05/17/12).

Wengine wanataka Fatima itumike baina ya umoja wa madhehebu, wengine wanaichukulia kuwa ni udanganyifu. Na hivyo ndivyo ilivyo, Fatima ni ulaghai!

### Fatima dhidi ya Papa Francis

Pamoja na udanganyifu wa Fatima, Papa Francis alimuomba Kardinali José Policarpo wa Lisbon auweke wakifu upapa wake kwa "Bibi wa Fatima" mnamo tarehe 13 Mei, 2013, wakati wa sherehe ya jubilee ya kutokea maono ya kwanza ya huko Fatima.

Zaidi ya hapo, Papa Francis aliagiza ile sanamu tuliyionyesha kwenye jarida la mbele la gazeti hili, ipelekwe Vaticani ili aitumie kuuweka wakfu ulimwengu kwa kile wanachokiita "Moyo mtakatifu wa Maria" tarehe 13 Oktoba, 2014. Sikukuu wanayoita 'mwujiza wa juu'. Mwujiza huo kwa bahati mbaya umefanikiwa kuwashawishi wengi kwamba tukio la Fatima lilitoka kwa Mungu.

Papa Francis ndiye amekuwa Papa aliye mbele zaidi katika "mambo ya Maria" kushinda papa ye yeyote aliyetangulia katika kuanza kwa upapa wake katika miongo ya hivi karibuni. Ninaamini kwamba anajaribu kuuandaa ulimwengu uweze kuipokea kwa upana zaidi imani juu ya wadhifa wa Maria katika wokovu.

### Fatima Yaweza Kutufundisha Kitu Gani?

Je, kunachochote ambacho Wakristo wa kweli wanaweza kujifunza kutoka Fatima?

Yesu alionya:

24Kwa maana watatokea makristo wa uongo na manabii wa uongo na kufanya ishara kubwa na miujiza mingi ili kuwapotosha, hata ikiwezekana wale wateule hasa. 25 Angalieni, nimetangulia kuwaonya mapema. (Mathayo 24:24-25).

Lakini, hata ikiwa bado hatujafikia hatua yenye hasa, wengi tayari wamedanganyika kutokana na Fatima. Ama hawajui au wameshindwa kuupambanua ukweli wa nini hasa kilitokeo

huko.

Mtume Paulo alifundisha kwamba katika nyakati za mwisho udanganyifu utaongezeka na kuzidi kuwa wa hatari:

13Lakini watu waovu na wadanganyaji watazidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika. 14Bali wewe, udumu katika yale ulijifunza na kuyaamini kwa uthabiti, ukitambua ya kuwa ulijifunza hayo kutoka kwa nani. (2 Timotheo 3:13-14).

Ni kwa jinsi gani Fatima, au hata na matukio mengine mengi ya mizuka, inaendana na hili? Fatima inadaiwa ni tukio lililosuhudiwa na watoto watatu, pamoja na iwapo watu watazingatia maelezo ya kile kilichoonekana, wataweza kupambanua kwa urahisi kabisa kwamba yule “Bibi wa Fatima” ni hila na ulaghai wa Shetani.

Lakini kwa kuwa “Bibi wa Fatima” ni udanganyifu na wadanganyaji watazidisha katika nyakati za mwisho, ni kitu gani kitatokea endapo mzuka mmoja ama mingi ya maono ya “Maria” itatokea hadharani mbele ya wengi? Waziwazi kiasi ambacho haitawezekana kuikana?

Ni dhahiri walio wengi watatembea kwa kuona na si kwa imani na hivyo watausadiki uongo. Wakristo hawatakiwi kufanya hivyo (2 Wakorintho 5:7).

Fuatilia pia kifuatacho:

6Nanyi sasa mnajua kinachomzuia, ili kwamba apate kudhihirishwa wakati wake utakapowadia. 7Maana ile nguvu ya siri ya uasi tayari inatenda kazi, lakini yule anayeizuia ataendelea kufanya hivyo mpaka atakapoondolewa. 8Hapo ndipo yule mwasi atafunuliwa, ambaye Bwana Yesu atamteketeza kwa pumzi ya kinywa Chake na kumwangamiza kabisa kwa ufunuo wa kuja Kwake. 9Kuja kwa yule mwasi kutaonekana kana kwamba ni kutenda kazi kwake Shetani ambaye hutumia nguvu zote, ishara, maajabu ya uongo 10na kila aina ya udanganyifu kwa wale wanaoangamia kwa sababu walikataa kuipenda kweli wapate kuokolewa. 11Kwa sababu hii, Mungu ameruhusu watawaliwe na nguvu ya udanganyifu, ili waendelee kuamini uongo 12na hivyo wote wahukumiwe ambao hawakuamini ule ukweli bali wamefurahia uovu. (2 Wathessalonike 2:6-12).

Siwezi kujizua bali kufikiri kwamba pengine mzuka uliotokea kule Fatima mwaka 1917 uliruhusiwa tu kutokea ukiwa katika siketi fupi na usidai moja kwa moja kwamba ulikuwa ni Maria kutoka kwa Mungu (soma: Ayubu 1:9-12; 2:4-6; 3 Wafalme 22:20-22; 1 Wafalme 22:20-22) ili wale waupendao ukweli kwa dhati waweze kutambua kwamba maono hayo yasingweza kuwa ya Maria wa Biblia. Hili ni pamoja na “mwujiza wa juu” (ambao kulikuwa na maelezo mengi yatofautianayo juu yake kitu kinachonifanya niamini kwamba ushawishi wa Shetani hata kwenye swala hilo nao ulikuwa umedhibitiwa). Vilevile ninaamini kwamba hii ndiyo sababu ni kwa nini hata matukio mengine ya mizuka yameelezewa yakiwa na taarifa za uongo (mfano: Medjugorje), alitokea akiwa kama muungu wa kike (mfano: Guadalupe), hakudai kuwa ye ye ni Maria (mfano: La Salette), na/ama alitokea kwa mtu mmoja au wachache tu—

Mungu amekuwa akidhibiti uwezo wa Shetani.

Pamoja na hilo, muda unakuja ambapo m izuka itakayojitokeza haitakuwa chini ya udhibiti huu (soma: 2 Wathessalonike 2:7), na hilo yaweza kuwa ndiyo sababu kwa nini wengi watapotoshwa kulingana na Yesu alivyosema (Mathayo 24:24; Marko 13:22). Lakini Mungu atakuwa na njia kwa ajili ya wamwaminio ya kuepukia (1 Wakorintho 10:13) udanganyifu.


Kwa wale walio “wanaupendo kwa ukweli” (2 Wathessalonike 2:10), “Waweza kuamini kwamba Mungu...katika kila jaribu atatoa pia na njia ya kutokea” (1 Wakorintho 10:13). Pamoja na wanadamu walio wengi kutoliamini kwa dhati, neno la Mungu ndilo chanzo kilicho cha uaminifu ambacho tunapaswa kulitumia kuanmua matukio yote ya maono ya kale, ya sasa na yajayo pamoja na ishara na miujiza (soma: Yeremia 23:28; Ufunuo 20:12; Waebrania 4:12; 2 Timotheo 3:16).

Bibi wa Fatima ilikuwa ni kutokea kwa pepo ambalo watu wanaweza kujithibitishia bila mashaka kwamba hakuwa Maria, japo mamilioni wanauamini uongo kuhusu mzuka huo. Wakati utakuja ambapo kitu kama hicho kitatokea hadharani mbele ya wengi.

omba ili uweze kuwa na imani ya “kutembea kwa imani, wala si kwa kuona” (2 Wakorintho 5:7), hata pale kila akuzungukaye atakuwa amehadaiwa!

# KOZI YA KUJIFUNZA BIBLIA

## Somo la 2: Hapa tunakuletea habari njema . . . UJUMBE uliotumwa toka Mbinguni



Bob Thiel, Mhariri Mkuu.  
Imechapichwa 2014 na Continuing Church of God

Utangulizi: Kozi hii inatokana kwa kiwango kikubwa na Kozi kwa Mawasiliano iliyohaririwa mwaka 1954, ilioanza chini ya usimamizi wa hayati C. Paul Meredith kuitia Radio Church of God. Baadhi ya maeneo yake yameboreshwa ili yaendane na karne ya 21 (japo mengi ya maandishi ya awali yamebaki yalivyo). Kadharika imeongezewa vifungu toka Maandiko Matakatifu, pamoja na taarifa na maswali ambayo hayakuwemo katika kozi ya awali.

### Hapa tunakuletea habari njema . . . UJUMBE uliotumwa toka Mbinguni

NI KWA NINI Injili ya kweli ya Yesu Kristo haihubiriwi na wengi leo? Kwanini wengi hawajawahi kuisikia injili yenye ya Yesu -- ule ujumbe aliouhubiri?

Tambua kwamba YESU hakuja duniani akiwa si sawa na wanafalsafa wa kibinadamu ama mwanaharakati bali alikuwa ni MJUMBE ATOKAYE MOJA KWA MOJA KWA MUNGU, Mwumbaji wa mbingu na dunia, yule ambaye anakupa wewe kila pumzi na uhai, yule ambaye ni mwenye Hekima kuitia Wote, atambuaye mwisho kutokea mwanzoni. Ukilijua hili, basi unapaswa uusikilize ujumbe wake!

Kuanzia mwanzo hadi mwisho wa Agano Jipya, UJUMBE huo—

INJILI hiyo—imerudiwa rudiwa kufundishwa. Pamoja na hilo tumeishia kwenye lundo la madhehebu, yakifundisha ujumbe tofauti na ule aliofundisha Yesu—na madhehebu yote hayo yakijiita kwa jina ya Kristo.

Kwanini?

Ukwelinikwambawanadamuyaonekanahawakotayarikuupokea UJUMBE WA YESU pasi kuugeuza. Wanadamu wameshindwa kutambua kwamba Mungu yuleyule aliyeaongoza akina Isaya, Danieli, Mika, pamoja na manabii wengine waandike kuhusu Ufalme wake ujao, ndiye huyohuyo aliyemtuma Yesu aje ulimwenguni KUIANDAA NJIA ya kuanzishwa kwa Ufalme huo.

Yesu ALIANZA huduma yake pale alipoenda Galilaya:

“.....Galilaya akihubiri Habari Njema za Mungu, 15akisema, “Wakati umewadia, Ufalme wa Mungu umekaribia. TUBUNI na KUIAMINI Injili” (Marko 1: 14- 15).

Yesu alitangaza toba ikiwa ndiyo jambo muhimu katika Injili ya Ufalme wa Mungu, au serkali. Unatakiwa uwe tayari kubadirika – kutubu dhidi ya njia zako – ili uweze kustahili kuingia kwenye ufalme huo.

Tambua kwamba Yesu hakusema: “Niamini tu MIMI”. Bali alisema: “lamini INJILI”. Injili hii au Habari Njema ilikuwa kitu gani? Yesu alikuja akihubiri habari njema -- siyo habari kuhusu yeze mwenyewe pekee kama Mwokozi –bali ni juu ya UFALME wa Mungu—UJUMBE kwamba Mungu ni Mtawala Mkuu wa mbingu na dunia, kwamba hivi karibuni atausimika ufalme wake hapa duniani, na pia kwamba tunapaswa tuutambua utawala wake juu ya maisha yetu sasa. Hii ndiyo Injili ya kweli! Na huo ndio ujumbe ambaa Yesu aliuleta hapa duniani kutoka kwa Mungu Baba!

### Ujumbe Siku hizi Umepotoshwa

Wengi wenu mmesikia injili dhaifu, isiyoelewaka, ya hisia za kuvuta moyo ambayo INAUKANA ule ujumbe ambaa Yesu aliuleta kutoka kwa Mungu juu ya kuja kwa UFALME WA MUNGU UTAWALAO DUNIA hivi karibuni.

Mara nyingi, utasikia mawazo na mahubiri mengi yasiyo na mashiko, yenyе mwelekeo wa mvuto wa kiroho kama: “Kwa Wakristo kila mahali wakifanya kazi kwa pamoja kuleta amani, kuvumiliana, na upendo wa kindugu, hatimaye ufalme wa Mungu utasimikwa katika mioyo ya wanadamu wote”.

Je, umewahi kusikia aina hii ya mazungumzo? Yawezekana umewahi kusikia, kwa sababu hii ndiyo aina ya falsafa inayoeneza na mamia ya wachungaji wa Kiprotestanti wa leo kote ulimwenguni. Ni mtazamo pia ambaa unaendana na matangazo ya kuunda umoja wa madhehebu yanayotolewa na Vaticani pamoja na baadhi ya makanisa ya Kiorthodoxi ya Mashariki. Pamoja na ukweli wazi wa JANGA lilitabiriwa katika unabii kutokea katika nyakati za ulimwengu huu ambaa tulijifunza katika somo la kwanza, wengi wa WATU hawa (na kwa wachungaji wa Kiprotestanti, pia hata na WANAWAKE) yaonekana hawaoni haja yoyote ya Mungu kuijingiza katika maswala ya wanadamu. Wanajaribu kuubadiri unabii huu wa

Mungu Kujingiza kwa kuufanya "unamaanisha KIROHO", na wanaficha macho yao dhidi ya UKWELI juu ya majanga ya dunia yanayozidi kuongezeka!

"Ufalme wa Mungu" mara nyingi hutumika kama neno la hamasa tu la kutaja hali ya moyoni ambayo mwanadamu anaweza kuifikia kwa kuweka jithada zake MWENYEWE akisaidiwa na Roho Mtakatifu. Jina la Mungu hufanywa kama kiungo cha kuongeza utamu kwenye swala hilo la rohoni ambalo ni la hali ya kujisikia kuwa na Mungu japo ungali unakufa na unaishi kwa matumaini tu.

Ndiyo, wengi wenu mmewahi kusikia injili za kibinadamu kuhusu Yesu alichofanya alipokuja kama Kristo, na hadithi za kusisimua juu ya kile wanachokiita "ufalme" utakaowekwa "moyoni" mwenu. Lakini ukweli ni kwamba UKWELI wa kiroho hautakiwi utokane na mawazo na kutafakari kibinadamu; huja ikiletwa kama ufunuao toka kwa Mungu. Unapatikana katika Neno lake—Biblia.

Je, Biblia yako inafunua kwamba Ufalme wa Mungu ni jambo la kufikirika tu? Hata kidogo, NI UFALME WA SERKALI HALISI utakaoitawala dunia hii! Ikiwa ni hivyo, sasa ni nani atakayekuwa mfalme (rais) wa Ufalme huo? Sheria zitakazotumika kuongoza ufalme ni zipi? Ni lini atakapochukua jukumu la kuitawala dunia hii?

Kadri utakavyokuwa ukijisomea utangulizi huu—pamoja na maswali yatakayofuata—kuwa makini kubaini majibu kwa maswali. Majibu yanapatikana katika Biblia yako.

## Injili Ilifichuliwa kwa Maria

Kabla Yesu hajazaliwa, malaika alimwambia Maria juu ya lengo la kuzaliwa kwake:

"32Yeye atakuwa mkuu, naye ataitwa Mwana wa Aliye Juu. Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi baba yake. 33Ataimiliki nyumba ya Yakobo milele na ufalme Wake hautakuwa na mwisho" (Luka 1:32-33).

Huyu mjjumbe wa kimalaika kutoka kwa Mungu alifichua kwa Maria ukweli muhimu amba ulimwengu huu hauuji kabisa! Malaika alimfunulia Maria kwamba mwanae KRISTO siku moja angechukua na kumiliki kiti halisi cha ENZI – ENZI/UTAWALA wa dunia – KITI CHA ENZI CHA DAUDI! Historia na unabii vyote vinathibitisha kwamba Kiti cha Enzi cha Daudi kingali kikitawala hadi leo - akingojewa Kristo arejee kukichukua! (Iwapo bado haujaufahamu ukweli huu, waweza kusoma makala ya Dr. Thiel iitwayo: "Waingereza na Wamarekani katika Unabii & Makabila ya Israeli". (Agiza kupitia mawasiliano ya Kanisa la Continuing Church of God).

Malaika vilevile alisema kwamba Kristo angeitawala nyumba ya Yakobo MILELE. Malaika hakusema "angetawala miyoni ama kiroho, pasipo kuonekana ndani ya nyoyo za wanaomwamini". Bali alisema "ataitawala nyumba ya Yakobo" – Ni serkali halisi, ni utawala halisi, hakuna longolongo, hakuna kufumbafumba! Alitabiriwa kuzitawala tawala hizi na nyumba hii ya Yakobo zilizokuwa duniani, hivyo hapo hakuna kuhamishwa bali

ataitawala dunia.

## Yesu Alihubiri Injili Halisi ya Ufalme

Yesu mwenyewe alihubiri "injili ya Ufalme" katika kipindi chote cha huduma yake (Mathayo 9:35) – alihubiri HABARI NJEMA ZA UTWALA WAKE UJAO WA ULIMWENGU. Mitume walijua kwamba angerejea na kuuletea "ulimwengu" huu wa sasa (neno "ulimwengu" lililovuviwa na kuandikwa awali kwa Kigiriki linamaanisha "zama") hitimisho kwa kuusimika Ufalme wake utakaotawala mataifa yote. Walimuuliza Yesu afafanue: "Tuambie, mambo haya yatakuwa lini? Nayu ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa zama hizi?" (Mathayo 24:3) – "mwisho wa enzi /zama hizi".

Inajulikana wazi kwamba kanisa la awali la Agano Jipyä lilitarajia kurudi kwa Kristo kuja kwenye dunia hii. Katika kuwafundisha kwamba hili halitatokea hadi kwanza kukengeuka kwa kiwango kikubwa kutokee kwanza, Paulo alivuviwa kuandika kwamba kutatokea "muanguko mkubwa" –kanisa kuperomoka kwa KUUACHA UKWELI – kabla ya kurudi kwa Kristo (2 Wathesalonike 2:3). Hatua ya awali ya aina hiyo tayari ilikuwa imekwisha kuanza kutokea hata wakati anaandika haya: "Wapo wawasumbua ninyi wakitaka kuigeuza Injili ya Kristo" (Wagalatia 1:7).

Kisha katika enzi zetu hizi – kipindi cha machafuko ya wakati wa mwisho wa zama hizi -- KRISTO ATAREJEA AJE "KUTAWALA MATAIFA YOTE KWA FIMBO YA CHUMA" (Ufunuo 19:15) kwa miaka elfu moja, au millennia (Ufunuo 20:4) hapahaha katika dunia hii (Ufunuo 5:10).

Ebu tulia na utafakari. Je maandiko tuliyoyaona yanaonyesha kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa uwe ni kanisa, ama kwamba kanisa – liundwalo na wanadamu wenyewe – lingeweza kuibadiri jamii ya ulimwengu huu hadi kufikia kiwango ambacho inaitwa kuwa ni Ufalme wa Mungu? La Haiwezekani!

Hata mwanahistoria maarufu ulimwenguni, Edward Gibbon, katika kitabu chake kiitwacho Decline and Fall of the Roman Empire (Kuperomoka na Kuanguka kwa Milki ya Rumi), aliandika kwamba WAKRISTO WA KANISA LA AWALI WALIAMINI juu ya kurejea kwa Kristo kiuhalisia kuja kuusimika Ufalme wa Mungu juu ya dunia hii. Katika sura yake ya 15 ijlukanayo sana inayohusu Kanisa la kikkristo, alisema:

"Imani ya kale na iliyojulikana sana juu ya utawala wa Millennia ilikuwa inahusishwa na kuja kwa Kristo mara ya pili. Sawa na jinsi kazi ya umbaji ilivyokuwa imekamilika katika siku sita, kipindi hicho katika hali ya sasa, kulingana na imani ya kale iliyohuishwa na nabii Eliya, ilitajwa kuwakilisha miaka elfu sita. Kwa mlinganisho huu ilielezewa kwamba kipindi hiki kirefu cha kazi ngumu na taabu nydingi, ambacho sasa kilikuwa kinalekeea kufikia tamati, kingefuatiwa na Sabato ya furaha ya miaka elfu moja; na kwamba Kristo, akiambatana na kundi la watakatifu walioshinda na wateule waliookwepa mauti, ama waliohuishwa kwa mwujiza, wangetawala juu ya dunia hadi wakati ulioamuliwa wa kufufuliwa watu wote uwadie."

Hapa tunapata ushahidi wa kustaajabisha hata kutoka kwa mwanahistoria asiyé muumini wa Ukristo kwamba ujumbe wa Kristo juu ya utawala wa Mungu hapa duniani ulikuwa umefundishwa na kuaminiwa na Wakristo wa awali. Wale walioishi punde tu baada ya Kristo, ni dhahiri waliujuwa UKWELI. Bado ulikuwa HAUJAPOTEA! Iwapo mtu akiyaangalia maandiko ya awali kutoka karne ya pili, atakuta kwamba ni dhahiri wengi wa viongozi waliomkiri Kristo, walifundisha juu ya utawala wa millennia na juu ya mpango wa miaka elfu saba!

Yesu pamoja na wengine wa Agano Jipya waliufundisha:

31 "Mwana wa Adamu atakapokuja katika utukufu wake na malaika wote watakatifu pamoja naye, ndipo atakapoketi juu ya kiti cha enzi cha utukufu wake. 32 Mataifa yote watakusanyika mbele zake, naye atawatenga kama mchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi. 33 Atawaweka kondoo upande wake wa kuume na mbuzi upande wake wa kushoto.

34 "Ndipo Mfalme atawaambia wale walioko upande wake wa kuume, 'Njoni, ninyi mliobarikiwa na Baba yangu, urithini Ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuumbwa kwa ulimwengu' (Mathayo 25:31-34).

9..." "Wewe unastahili kikitwaa kitabu na kuzivunja lakiri zake, kwa sababu ulichinjwa na kwa damu Yako ukamnunulia Mungu watu kutoka katika kila kabilia, kila lugha, kila jamaa na kila taifa. 10 Wewe umewafanya hawa wawe ufalme na makuhani wa kumtumikia Mungu wetu, nao watamiliki katika dunia." (Ufunuo 5:9-10).

4 Kisha nikaona viti vyá enzi vilivyokuwa vimekaliwa na hao waliopewa mamlaka ya kuhukumu. Nami nikaona roho za wale waliokatwa vichwa kwa sababu ya ushuhuda wa Yesu na kwa sababu ya neno la Mungu. Hawakuwa wamemsujudia huyo mnyama wala sanamu yake wala hawakupokea ile chapa yake kwenye vipaji vyá nyuso zao au kwenye mikono yao. Wakawa hai na kutawala pamoja na Kristo miaka 1,000. 5 (Wafu waliosalia hawakufufuka mpaka ilipotimia hiyo miaka 1,000.) Huu ndio ufufuo wa kwanza. 6 Wamebarikiwa tena ni watakatifu wale walio na sehemu katika huo ufufuo wa kwanza. Hao mauti ya pili haina nguvu juu yao, bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye kwa muda wa miaka 1,000 (Ufunuo 20:4-6).

Katika enzi za Agano la Kale, Nabii Mika alivuviwa aandike:

1 Katika siku za mwisho mlima wa hekalu la BWANA utaimarishwa na kuwa mkuu kuliko milima yote, utainuliwa juu ya vilima na mataifa yatamiminika humo. 2 Mataifa mengi yatakuja na kusema, Njoni, twendeni mlimani kwa BWANA, kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo. Atatufundisha njia zake, ili tutembee katika mapito yake." Sheria itatoka Sayuni, neno la BWANA litatoka Yerusalem.

3 Atahukumu kati ya mataifa mengi na ataamua migogoro ya mataifa yenye nguvu na yaliyo mbali. Watafua panga zao ziwe majembe ya kulimia na mikuki yao kuwa miundi ya kukatia matawi. Taifa halitachukua upanga dhidi ya

taifa, wala hawatajifunza vita tena. 4 Kila mtu ataketi chini ya mzabibu wake na chini ya mtini wake, hakuna mtu atakayewaogopesha, kwa kuwa BWANA Mwenye Nguvu amesema. (Mika 4:1-4).

Wote wanadamu na wanyama wataishi vizuri na kwa amani katika nyakati hizo. Agano Jipya linathibitisha kwamba viumbe wote watanufaika katika nyakati hizo:

19 Kwa maana viumbe vyote vinangoja kwa shauku kudhihirishwa kwa watoto wa Mungu. 20 Kwa kuwa viumbe vyote viliwekwa chini ya ubatili, si kwa chaguo lao, bali kwa mapenzi Yake Yeye aliyevitisha katika tumaini, 21 ili kwamba viumbe vyote vipate kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa kuharibika na kupewa uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu (Warumi 8:19-21).

Enzi hizo za "uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu" ambazo Mtume Paulo anaziongelea, zitatukia pale Yesu Kristo atakaporejea kuja kuusimika ufalme wake.

Na huu ndio wakati ambapo watu wa Mungu watatumia kusaidia kuboresha na kurejesha sayari iliyoharibiwa irudi katika hali yake:

12 Watu wako watajenga tena magofu ya zamani na kuinua misingi ya kale, utaitwa Kutengeneza Kuta Zilizobomoka, Mwenye Kufanya upya Barabara zenyé Makazi (Isaya 58:12).

Hivyo, watu wa Mungu watawawezesha watu waone ni vyepesi kuishi mijini (na popote pengine) katika enzi hizo za ufanywaji upya wa dunia. Ulimwengu kiukweli utakuwa ni mahala pazuri pa kuishi.

NI NANI aliyesema kwamba Kristo angeusimika utawala wa Mungu juu ya dunia? Jibu ni kwamba ujumbe huu ulihubiriwa na manabii wa Agano la Kale, na mitume na wainjilisti wa Agano Jipya, na pia na Yesu Kristo mwenyewe, na hata imetajwa katika maandiko mengi ya kihistoria.

Ujumbe huu ndio chimbuko halisi la injili ya kweli. Jifunze maswali yafuatayo kuitia Biblia yako, na UTHIBITISHE hili kwa macho yako wewe mwenyewe.

## Maelekezo Muhimu ya Mwisho

Sasa tuko tayari kwa ajili ya somo lenyewe. Je, Biblia yako iko mbele yako? Kama haiko, tafadhari usiendelee kusoma zaidi kozi hii!

SIMAMA HAPA! NENDA KALETE BIBLIA yako.

Vilevile kumbuka kuandaa karatasi kadhaa, pamoja na penseli ama kalamu, ili uweze KUCHUKUA NOTISI zitakazokuwezesha kukumbuka kile unachojifunza.

Kozi hii imejikita kwenye nakala ya Biblia iitwayo New King James Version (NKJV) kwa kuwa imekusudiwa iwe ni tafsiri ya neno kwa neno na inatumia aina ya lugha ya Kiingereza ambayo inazungumzwa katika karne hii ya 21. Kwa mengi katika somo, waweza kutumia nakala zingine za tafsiri ya Biblia, lakini maswali

na majibu hususani yanalenga tafsiri ya NKJV labda pale tu patakapoelekezwa. Hivyo, kwa wengi, nakala ya NKJV ndiyo chaguo bora la kutumia katika Kozi ya Kujifunza Biblia.

Sasa tuko tayari kuanza kujisomea kozi hii. KUMBUKA unapaswa uifungue Biblia yako ili kujithibitishia kila aya tunayotoa kama kieleelzo cha kile tunachosema katika kozi hii. Usiamini tu kile tukisemacho (timu ilioongozwu na marehemu C. Paul Meredith na/ama Bob Thiel)—amini kile ambacho Biblia inakifundisha.

Unapaswa USOME, na kurudia tena kusoma, na kwa kweli ujifunze KILA AYA KATIKA BIBLIA YAKO. Hii ni kozi ya KUJIFUNZA Biblia—ni kujisomea Biblia, siyo tu kujisomea haya maneno tunayokutumia. Maneno yetu yamekusudiwa tu yakuongoze kufika pale unakotakiwa kuangalia katika Biblia yako—ni kukusaidia ujue namna ya kujifunza Biblia.

Sasa, ukiwa na Biblia yako, KAMUSI (DICTIONARY) kama unayo, na karatasi zako za kuandika na penseli ama kalamu zote juu ya meza yako mbele yako, mfumo wa kujisomea utakuwa kama ifuatavyo: Andika kwa ufasaha kwenye karatasi yako, kichwa cha somo: “Somo la 2, Sehemu ya 1,” na upapigie mstari chini yake. KIANDIKE KICHLWA CHA SOMO pamoja na kila kichwa cha sehemu ya maswali. Kisha, chini yake andika namba ya kila swali, na uandike jibu kwa kila swali, kwa mwandiko wako mwenyewe (baadhi yenu mwaweza kuamua kuandika kwa computer ama typewriter). Kama MFANO, kwa ajili ya kipengele cha swali, hivi ndivyo utakavyoandika kwenye karatasi ama notebook yako: Ufalme Ujao Ulihubiriwa na Manabii wa Kale. Kisha andika:

1. Amosi 3:7—“Hakika Bwana Mungu hatafanya jambo lolote, pasipo kwanza kuwafunulia siri yake watumishi wake manabii”.

Vilevile andika chochote kingine unachohitaji kukikumbuka. Jifunze na uelewe hili.

Hifadhi somo hili pamoja na notisi zako pia na majibu ya maswali kwenye faili ama jarida. USITUTUMIE MAJIBU YAKO YA MASWALI YA MASOMO HAYA. Yatunze tu kwa ajili ya kujikumbusha. (Inawezekana pengine tutatoa cheti (certificate) kwa wale watakaokamilisha kozi yote au hata sehemu kubwa ya kozi hii, ila hili litakuwa ni baada ya mwaka 2014, na tutalitangaza hili kupitia mtandao na sehemu zingine. Endapo tutafikia kufanya hivyo, basi tutakuomba ututumie nakala za masomo uliyokamilisha).

Kwa kuyaandika majibu kwa maswali haya, na pia kwa kuandika notisi zitokanazo na aya za Biblia unazojifunza kwa kila swali, utakuta kwamba inakuwezesha KUKUMBUKA yale ullyojifunza. Inachukua muda zaidi kidogo kwa kufanya hivyo, lakini hii ndiyo itakusaidia KUJIFUNZA masomo yako vema, na kuyakumbuka baadaye.

Wengine huuliza, “Huku KUANDIKA kweli kuna UMUHIMU wowote?”

Jibu ni NDIYO!

NI MUHIMU SANA!

Kwa nini?

Tunahitaji uielewe Biblia ki-ukweli. Wakristo wanatakiwa kuwa walimu (soma. Waebrania 5:12) na hivyo wanahitaji kuijua Biblia yao vema ili “Sikuzote mwe tayari kumjibu mtu ye yote atakayewauliza kuhusu tumaini lililomo ndani yenu. Lakini fanyeni hivyo kwa upole na kwa heshima” (1 Petro 3:15).

Kwa kuandika kile unachojifunza itakusaidia kukumbuka vema.

Halikadharika, ITAKUWEZESA KUFANYA MAPITIO YA MASOMO YAKO KWA HARAKA, kila ihitajikapo, endapo utakuwa nayo katika mtindo huu. Vilevile, itakusaidia sana katika kuifafanua Biblia kwa wengine.

TUNAKUPATIA DONDODA ZA BIBLIA ZA UKWELI KWA UFUPI NA KWA UFASAHA. Utahitaji kufanya marejeo kwenye masomo haya na MAELEZO YAKE ukitumia sasa ufanuzi wako mwenyewe kwa miaka mingi ijayo kila utakapo yatumia kuifafanua vipengele mbalimbali katika Biblia. Kumbuka, utahitaji kutumia angalau nusu saa kila siku ukijisomea BIBLIA YAKO ukitumia hii Kozi ya Kujifunza Biblia.

Sasa SOMA MANENO YALIYOANDIKWA KWA HERUFI NZITO KATIKA HAYA MAELEKEZO MUHIMU YA MWISHO hadi kufikia mwisho wa sehemu hii—Usijali herufi zilizo andikwa kwa wino mdogo. NA HAPO GHAFLA UTAKUTA UNAPATA PICHA YA KILE UTAKACHOJIFUNZA NDANI YA SOMO HILI! Vlichwa vyaa kila hatua ya Somo hili vimeandikwa kwa mtindo huu. TUMIA MANENO YA WINO MZITO KUELEWA KICHLWA CHA KIPENGELE UNACHOJIFUNZA!

## SOMO LA 2

### Sehemu ya I

#### Ufalme Ujao Ulihubiriwa na Manabii wa Kale

1. Je, Mungu hujiingiza katika maswala ya dunia pasipo kwanza kuwafunulia nia yake manabii wake? Amosi 3:7.
2. Mamia ya miaka iliyopita, je, ISAYA, Nabii, ALITABIRI juu ya kipindi ambacho Mungu angeusimika ufalme wake duniani? Isaya 2:1-4. Je, ufalme huo unaelezewa kuonyesha kwamba ni UFALME HALISI UTAWALAO JUU YA DUNIA? Je wewe unadhani kungeweza kuwa na “milima” (tawala za mataifa ya kidunia) huko mbinguni? Je, kutakuwa na vurugu na vita katika ufalme huo kama ilivyo kwa sasa miongoni mwa mataifa? Aya ya 4.
3. Je, utawala wa Mungu juu ya dunia hii na kubadiri tawala zote KULITABIRIWA NA DANIELI? Danieli 2:36-45. Zingatia aya ya 44 zaidi. Je, falme zingine bado zitaendelea kuwepo pale Kristo atakapoanza kuusimika utawala wake? Aya ya 44. Nini kitatokea kwa tawala hizo? Je, haya yote yanaonyesha kwamba Danieli alifahamu kwamba Ufalme wa Mungu utakuwa ni ufalme-serkali halisi wenye mamlaka

na uwezo juu ya mataifa yote?

4. Je, DAUDI alizungumza kuhusu Mungu kutawala juu ya dunia? Zaburi 67:4.

5. Je, MIKA aliwahi kusema Mungu atausimika Ufalme wake juu ya dunia hapo baadaye? Mika 4:1-5.

6. Ni wapi ambako YEREMIA anakutaja kwamba kiti cha enzi cha utawala huo kitakako kuwa? Yeremia 3:17.

7. Ni nani ambaye Isaya alitoa unabii kwamba angeitawala dunia? Soma Isaya 11:1-4. Huyu "shina la Yes" hasa ni nani? Matendo 13:22. Je, ni Daudi ama ni mtu mwingine? Sasa huyu tawi ama chipukizi ni nani? Aya ya 23. Na huyu TAWI linaloota kutoka kwenye mizizi ya Yes ni nani hasa? Yeremia 23:5-6. Hivyo tumeona UTHIBITISHO MARA DUFU kuwa Kristo atatawala.

8. Je, Danieli aliwahi kutabiri juu ya kipindi ambapo Watakatifu wangepepe kutawala juu ya dunia katika Ufalme wa Mungu wakiwa na Kristo? Danieli 7:18, 21-22, 27.

9. Kutokana na tulicho jifunza, je, hatugundai kwamba Manabii wa Agano la Kale pamoja na Wainjilisti WOTE WANAKUBALIANA katika kutufahamisha kwamba Mungu ataingilia maswala ya wanadamu na kuusimika utawala wake – Ufalme wake – hapa juu ya dunia ukiwa chini ya Kristo? Je, Mungu hubadirikabadirika katika lengo lake Kuu? Malaki 3:6; Waebrania 13:8.

10. Je, Kitabu cha Ufunuo kinaonyesha kwamba Wakristo watatawala juu ya dunia wakiwa na Yesu Kristo? Ufunuo 5:8-10, 20:4.

11. Tumeona kwamba Mungu, kuititia kwa manabii wengi waliovuviwa wa enzi za Agano la Kale, aliujulisha ulimwengu juu ya kuja kwa tukio hili la kusimua. Lakini, zaidi ya hili, je, Mungu alimtuma pia Kristo akiwa kama MJUMBE maalum aje atangaze kabla ya wakati tukio hili tukufu kwetu? Na je, amewatuma WAJUMBE WENGINE WA ZIADA waje kuitangaza HABARI NJEMA ama INJILI kwetu sisi tunaoishi KATIKA NYAKATI HIZI ZA MWISHO?

## KRISTO – Mjumbe Maalum

1. Je, YESU ALITUMWA AKIWA NA UJUMBE? Yohana 6:38; 12:49; 14:24.

2. Yesu alipokuja humu duniani alitoka wapi? Yohana 3:13. Alitumwa na Nani? Aya ya 34.

3. Alikuwa ametumwa kwa nani? Matayo 15:24; Yohana 1:11.

MAELEZO: Kristo alitumwa kimsingi kwanza kwa "Walio wake" taifa lake—kwa Nyumba ya Israeli—akiwa na ujumbe wake wa Injili! UNAOHUSU UFALME WA MUNGU UJAO. Baadaye, hata hivyo, alitoa unabii kwamba wanafunzi wake wangeuhubiri UJUMBE HUU KWA ULIMWENGU WOTE: Mathayo 24:14; 28:19-20.

4. Katika mahubiri ya kwanza kuelekezwa kwa watu wa mataifa, Petro anaeleza mengi yanayothibitisha kile ambacho tumejifunza, na anaongezea elimu yetu juu ya ujumbe huu wa Agano Jipy. Soma Matendo 10:36-37 na ujibu haya maswali: (1) Ni nani aliyelitura neno hili, au ujumbe? (2) Je, ni kwa nani neno hilo lilitumwa kwanza--je, ni kwa Watu wa Mataifa? (3) Je, lilihubiriwa na nani? (4) Je, lilihubiriwa ama lilitangazwa wapi? (5) Ni wapi ambako Kristo alianzia kulihubiri? (6) Ni lini ambapo ujumbe huu ulianza kwanza?

5. Soma Marko 1:14-15. (1) NI LINI Ujumbe huu ulipoanza? (2) Ni nani alihubiri? (3) Ni kuanzia WAPI alianza kuuhubiri? (4) NI UJUMBE GANI, uliokuwa umetumwa toka kwa Mungu, ambao alihubiri?

6. Katika Marko 1, linganisha aya ya 1 na aya ya 14. Je, Injili ya Yesu Kristo ndiyo injili yenye aliyoihubiri?—yaani taarifa juu ya Ufalme wa Mungu ujao? Kimsingi SIYO UJUMBE UNAOMHUSU YEYE BINAFSI na juu ya KUMWAMINI yeye, bali ni JUU YA KUUAMINI ULE UJUMBE aliouleta.

MAELEZO: Ni wachache wanaoielewa "Injilia ya Kristo". DATU LEO wanafundishwa katika makanisa kwamba "injili ya Kristo" inahusu kuyajua na kuyaamini matukio ya kipindi cha maisha ya Kristo pekee, na juu ya kuwa Mwokozi wao. HAWAFUNDISHWI UJUMBE WOTE WA INJILI ALIYOILETA—INJILI YA UFALME UNAOKUJA!

7. Maelezo katika Marko 1:15, kwamba "Ufalme wa Mungu umekaribia", yana maanisha nini? Kumbuka, injili ya Ufalme ambayo Yesu Kristo alihubiri HAIKUWA umbe juu ya kurejesha utawala wa watu katika eneo la Yudea enzi za miaka 2000 ILIYOPITA. Tunaliujuje hilo? Ebu na tuendelee kujifunza.

8. Pale Wayahudi walipotaka kumfanya Yesu Kristo awe mfalme wao, alifanya nini? Yohana 6:15. Pale wanafunzi walipomwuliza Yesu endapo wakati huo angeurejesha Ufalme, jibu lake lilikuwa ni nini? Matendo 1:6-7. Je, Yesu alikana kwamba Ufalme utakuwa ni wa zama hizo? Je, alionyesha kwamba ufalme UNGEKUJA wakati wa zama zizajo—ZAMA ZETU ZA SASA? Mathayo 24:3. (Kumbuka kwamba neno la Kigiriki lililotafsiriwa kama "ulimwengu/dunia" kiukweli linamaanisha zama—siyo dunia). Kwa ujumla, maana iliyomo katika Marko 1:15 ni kwamba wakati "umekaribia" hivyo tunapaswa KUTUBU ili tustahili kuingia kwenye Ufalme huo.

MAELEZO: NENO "INJILI" LINAMAANISHA "HABARI NJEMA" au "Habari za Furaha" za Ufalme! Mungu anajua zaidi kuliko tuwezavyo kufikiria, jinsi ufalme huo utakavyokuwa ni eneo la kufurahisha! VITU VINNE NI MUHIMU ILI KUUNDA UFALME: (1) ENEO LA (2) MFALME ama MTAWALA, juu ya (3) WATAWALIWA ama raia, kukiwa na (4) SHERIA ama serkali. Hivyo tunaweza kuifafanua Injili ya kweli kuwa ni "HABARI NJEMA ZA ENEO AMBALO MFALME atawatawala RAIA wake akitumia SHERIA pamoja na serkali ya Mungu".

INJILI YA KWELI, HIVYO BASI, INAHUSISHA ujumbe kumhusu Kristo ambaye ndiye Mfalme—lakini ni zaidi ya hayo. Kristo, pale atakapokuja, atafanyika Mtawala juu ya mataifa yote. Injili inahusisha pia ujumbe wa wokovu, ambao unamaana ya kufanyika RAIA wa ufalme huo (Waefeso 2:19). Sheria za Mungu ndizo zitafanyika sheria za kuendesha utawala wa nchi.

## Mitume Wanaendezea Kuuhubiri Ujumbe!

1. Je, YESU ALIWAAMURU WATUMISHI WAKE WAIHUBIRI injili hii ileile? Luka 9:1-2. Na kadri Mitume walipokuwa wakienda kwa mataifa, je, walikuwa wawafundishe UJUMBE ULEULE ambao Yesu Kristo alikuwa amewafundisha? Mathayo 28:19-20.
2. Je, PHILIPPO, Mwinjilisti, aliihubiri Injili ya Ufalme kwa Watu wa mataifa wa Kisamaria? Matendo 8:12.
3. Je, PAULO aliihubiri Injili ya Ufalme? Matendo 19:8 na 14:21-22; Kwa watu wa mataifa wa Efeso, ni Injili ipi ambayo Paulo aliihubiri? Matendo 20:25. Ni Injili ipi ambayo Wayahudi waliokuwa Rumi hatimaye waliikataa? Matendo 28:23-28.
4. Kufuatia Wayahudi kuikana na kuikataa Injili, Je, Paulo alienda kuihubiri INJILI ILEILE kwa Watu wa mataifa? Aya ya 31. Na kisha je, Paulo aliihubiri Injili ya Ufalme wa Mungu kwa wote Wayahudi na Watu wa mataifa, hakufanya hivyo?
5. Je, ilitabiriwa kwamba WATUMISHI WA UONGO watajaribu kuhubiri “INJILI TOFAUTI”—Injili za aina nyingine badala ya Injili ya kweli ya Kristo? Wagalatia 1:6. Ni Injili ngapi ndizo sahihi, tofauti na ile alioihubiri Paulo? Wagalatia 1:8. Je, si kwamba hizi injili zingine ni upotoshaji wa Injili ya Ufalme aliyoleta Kristo? Wagalatia 1:7.
6. Kwa kuwa wapo mitume wa uongo, si kwamba watajaribu KUUPOTOSHA ujumbe wa Kristo juu ya eneo halisi, juu ya watakaotawala, juu ya raia, sheria ama serkali ya Ufalme wa Mungu? Je, hawatajaribu kujifanya waonekane kama vile kile wanachokisema ni cha kweli? 2 Wakorintho 11:13-15.
7. Ni Injili ipi ambayo inatakiwa ihubiriwe na kutangazwa LEO? Mathayo 24:14; Marko 13:10.

MAELEZO: Wahubiri kwa ujumla, katika siku hizi za giza hawaihubiri Injili ya kusimikwa kwa mamlaka ya Mungu mwenyewe ya kuisimamia dunia na maandalizi tunayotakiwa kuyafanya katika kutarajia hili. Badala yake, jithiada zao zimejikita katika “Uundwaji wa Umoja wa Madhehebu”—harakati za makanisa ya kibinadamu za kujaribu kuwaunganisha pamoja ili wawe na ulinzi wa pamoja!

Sasa umejionea kwamba ujumbe wa Injili umetangazwa tokea mwanzo wa Biblia yako hadi mwisho wake. Siyo mawazo ya wanadamu ambayo hayana uvuvio, bali ni ujumbe ambao umekuwa ukitangazwa “kwa vinywa vya manabii wake watakatifu tangia mwanzo wa ulimwengu” (Matendo 3:21). Huu ndilo tumaini la mwisho kwa amani ya ulimwengu!

Ebu na TUSHANGILIE kwa ajili ya HABARI NJEMA hii!

AMANI I KARIBU! Sehemu ifuatayo ya somo hili itafunua ni lini Yesu Kristo atarejea kuja kuusimika utawala au Ufalme wa Mungu usiroyumba hapa duniani. Ebu na tulielewe vema swala hili muhimu.

## NI LINI Kristo Atarejea?

Wa-agnostic au wa-atheist (Wasioamini kwamba kuna Mungu) wanaweza kuyadhihaki mafundisho ya Yesu Kristo. Lakini hakuna muumini yeyote awezaye kukana kwamba Yesu Kristo alikuja duniani takribani miaka 1900 iliyopita!

Hili ni moja ya maswala ya kihistoria ambalo ukweli wake umethibitika bila ya shaka.

Hata hivyo kile ambacho ni wachache tu wanatambua ni kwamba Yesu aliahidi, “NITAKUJA TENA” (Yohana 14:3).

Wakati wa kupaa kwake, Mitume walishitushwa kwa kutokewa na wajumbe wawili wa Mungu waliosema: “Huyu Yesu, aliyetwaliwa kutoka kwenu kwenda mbinguni, atarudi kwa namna ileile mliyamuona akienda mbinguni” (Matendo 1:11).

Hapa tunaona wajumbe wawili wa kimalaika waliotumwa moja kwa moja kutoka kwa Mungu kuja kuyathibitisha maneno ya Yesu kwamba angekuja tena. Kanisa la AWALI lililokuwa na uvuvio la Agano Jipyu LILIJUA Yesu alimaanisha kile alicho sema. Walikiamini. Walikfundisha. Lakini ulimwengu umekipoteza!

Edward Gibbon katika kitabu chake mashuhuri cha historia kii twacho: The Decline and Fall of the Roman Empire (Kuporomoka na Kuanguka kwa Milki ya Rumi), sura ya 15, alisema: “Taratibu, baada ya miaka kupita, ukweli kwamba Yesu inampasa kwa MARA YA PILI kuja kuingilia maswala ya ulimwengu ulianza kuonekana kama hauna umuhimu. Ndani ya karne moja na nusu baada ya Kristo, ukweli huu ulianza kugeuzwa kuwa ni fumbo tu—kuwa ni mfano tu ulioletwa na Wayahudi. Hatimaye, baada ya nyakati za Mfalme Constantine, ulianza kuchukuliwa kuwa ni uzushi mkubwa uliokuwa unaandamana na adhabu ya kifo. ULIMWENGU hadi leo ungali UKIUDHIHAKI UKWELI WA WAZO hili kwa sababu hawataki kuuamini!

## Wazo Lipi Ndilo Sahihi?

KATIKA KIZAZI HIKI CHA KUOGOFYA CHA ATOMIC NA SILAHA ZINGINE ZA UANGAMIFU MKUBWA, wazo la kushtua kwa mara nyingine linalekezwa kwenye uwezekano wa kurudi kwa Kristo katika uwezo wa kiungu. Hata hivyo ni mionganoni mwa wale ambao pekee ndio wanatambua kwamba ni Mungu pekee ndiye awezaye kuwaokoa wanadamu, wamejawa na mkanganyo mkubwa—ipo mitazamo mamia kwa mamia ya kibinadamu iliobuniwa kujaribu kuelezea ni lini, ni kwa jinsi gani na pia ni kwa nini Yesu Kristo atarudi.

MAKANISA yako katika MIKANGANYIKO na mashaka. Wengi wao hawaamini kwamba Mungu ataingilia kat, lakini pia

wamo katika uoga kwamba mwanadamu amefikia uwezo wa kuangamiza maisha yote toka sayari hii!

Ni wakati muafaka utupasao tuutambue ukweli juu ya LINI Yesu ataitimiza ahadi yake, "Nitakuja tena!"

Mashuhuri mionganoni mwa mamia ya mitazamo mbalimbali ni MITAZAMO YA AINA TATU KUU juu ya kurudi kwa Kristo.

## Je, Kanisa Ndilo Ufalme?

Kwa dhahiri mtazamo uliojikita kwa wengi ni dhana kwamba MAKANISA YA LEO NDIYO UFALME WA MUNGU na kwamba Yesu Kristo ALIKUJA mara ya pili kupitia kwa Roho Mtakatifu kwenye siku ya Pentekoste (Matendo 2). Kwa vile Kristo alitangaza katika Injili kwamba angerudi kuja kutawala, basi inafundishwa kwamba Yesu aliwakabidhi mitume pamoja na walowafuatia haki ya kutawala na kuyahukumu mataifa.

Kutoka kwenye dhana hii ndiko kuliibuka desturi ya enzi za Zama za Kati ya Kanisa kuyatawala mataifa na kupenyeza matakwa yake kwa watawala wa serkali za dunia hii. HII ILILIFANYA KANISA—ambalo ilikuwa likijita kuwa ni Ufalme wa Mungu – liwe NI SEHEMU YA ULIMWENGU huu, liwe ni sehemu ya mfumo huu wa utawala wa kibinadamu. Kanisa likashindwa kutazama ukweli kwamba Yesu alisema: "Ufalme Wangu, siyo wa ulimwengu huu"—yaani mfumo huu (Yohana 18: 36).

Hizi ni zama za utawala wa wanadamu waonao mauti na kuharibika wanaoongozwa na shinikizo la Shetani (Luka 4:5-6). Ufalme wa Yesu SIYO WA ZAMA HIZI. Ni ufalme wa elimwengu wa kesho—"ulimwengu ujao" (Waebrania 2:5).

Pale alipohojiba endapo angeusimika ufalme katika wakati huo, Yesu aliwajibu mitume: "Siyo juu yenu kujua nyakati na majira ambayo Baba ameyaweka katika mamlaka yake. Lakini mtapokea nguvu mtakapojiliwa na Roho Takatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu . . . na hadi mwisho wa dunia" (Matendo 1:6-8).

Katu Kristo hakuwahi kuwaagiza mitume wake WAKAYATAWALE MATAIFA ya ulimwengu huu. Badala yake, aliwaagiza wawe mashahidi kwa kuihubiri injili!

Tambua kwamba mitume waliambiwa hawawezi kujua muda na nyakati za kuusimika Ufalme, bali walikuwa wajazwe na Roho Takatifu kwenye siku ya Pentekoste. Hivyo kuja kwa Roho Takatifu kusingeweza kuwa ndiko kurudi kwa Yesu Kristo. Badala yake, mitume walipewa nguvu kwa Roho Takatifu ili wawe mashahidi -- wa kitu gani? – wa tukio la kufufuka na wa Injili ya Ufalme. Yesu aliwaagiza wanafunzi "kuyafundisha mataifa yote". Aliwaaahidi atakuwa pamoja nao katika Roho hadi mwisho wa zama hizi – mwisho wa ulimwengu huu wa sasa wa utawala mbovu wa kibinadamu (Mathayo 28:19-20).

"Na injili hii ya ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote kama ushuhuda kwa mataifa yote, ndipo mwisho utakapokuja", alisema Yesu Kristo (Mathayo 24: 14). Mwisho wa kitu gani? Wa zama hizi, mfumo wa utawala wa ulimwengu huu –Pale Yesu atakapokuja tena! (Mathayo 24:3). Dhiki Kuu itaanza na ulimwengu utapitia mabadiriko makubwa (Mathayo 24:21-22).

Kristo hakurejea na kuanzisha Ufalme katika enzi za mitume. Badala yake, aliagiza Injili ihubiriwe ili kuuandaa ulimwengu kwa ajili ya kurudi kwake – KUJIINGIZA kwake katika maswala ya wanadamu kwa kutawala ulimwengu huu kwa miaka 1000 (Ufunuo 20:4).

## Baada ya Millennia

Mtazamo mwingine ambao ni wa hivi karibuni zaidi ni fundisho kwamba Yesu ATAREJEA TU BAADA ya kuwepo kwa amani na utulivu utakapotapaka duniani pale mataifa yote yatakapokuwa katika maelewano sahihi! Wakatholiki mbalimbali yaonekana wanaamini aina ya imani hii. Ni KUSHINDWA KUELEWA KWA KIWANGO GANI matukio ya ulimwengu pamoja na unabii wa Biblia! Biblia inaonya kutakuwa na matangazo ya uongo juu ya kuwepo kwa amani (mfano 1 Wathesalonike 5:3).

Kurejeshwa kwa amani na utulivu kutakuja baada ya Yesu Kristo kuingilia kati katika maswala ya dunia. Kwa sasa Yesu yuko mbinguni. Ni yeze "ambaye mbingu zilibidi zimpokee hadi zije zama za kufanywa upya mambo yote" (Matendo 3:21).

Pale Yesu atakaporejea, "mabalozi wa amani watalia kwa uchungu. Njia kuu zimekuwa magofu" (Isaya 33:7-8). Dunia itakuwa katika vurugu – siyo katika amani – kabla hajarejea.

KRISTO HAREJEI BAADA YA UTAWALA WA MILLENNIA (miaka 1000) ya utawala wa amani wa kibinadamu. Ni kuja kuondolea mbali utawala mbovu wa kibinadamu na kuusimika Ufalme – Utawala -- wa Mungu ndiyo sababu Yesu anakuja mara ya pili. Wakristo waliofufuliwa "waliishi na kutawala na Kristo kwa miaka elfu moja" (Ufunuo 20:4, sehemu ya mwisho. Ikiwa wanatakiwa watawale pamoja na Kristo, basi ni dhahiri Kristo atakuwa tayari kesha kuja kabla ya hiyo miaka 1000 haijaanza!

## Kabla ya Millennia!

Fundisho la tatu kuu ni kwamba KRISTO ANAREJEA KABLA YA MILLENNIA. Hii ilikuwa ni IMANI ILIYOFUNDISHWA KATIKA ENZI ZA KANISA LA AWALI LA AGANO JIPYA KABLA UKWELI HAUJAPOTEA! Kanisa la awali liliovuvi la kimitume liliuju kwamba Kristo alikuwa arejee kabla ya millennia.

Kuja kwa Kristo mara ya pili ni sehemu muhimu katika MPANGO WA MUNGU. Imetapaka kote katika Biblia – Agano la Kale na Jipy. Mungu amekuwa akitangaza mwisho ama hitimisho la mpango wake "tangia mwanzo" kupitia kwa manabii wake na mitume. Lakini ulimwengu haujaukulali ujumbe wao (Isaya 46: 10).

Yesu aliweka WAZI KABISA punde tu kabla ya kupaa kwake kwamba angerejea akionekana waziwazi baada ya matukio yaliyoainishwa kutimia. Alitoa mfuatano wa matukio haya kwa wanafunzi wake walipokuwa kwenye Mlima wa Mizeituni. Utakuta hayo yameandikwa katika Mathayo 24, Marko 13 na Luka 21.

Kadri ya miaka sitini baadaye alimpa Yohana kitabu cha Ufunuo, akitoa ufanuzi ulio wazi zaidi wa matukio ya ulimwengu yaongozayo hadi kufika kwenye Siku ya Bwana – siku ambapo

Kristo atarejea.

Katika Mathayo 24:32-33, Yesu alitoa MFANO ili tuweze kuuujua muda wa kurudi kwake. Kwa kuwa Yesu aliweka msisitizo kiasi kikubwa juu ya kukesha/kuwa makini na kungojea ili siku hii isije kutukia wakati hatujitambui, ni wakati muhimu kwamba tujifunze na KUELEWA umuhimu wa KUJA KWA KRISTO KWA MARA YA PILI!

## SOMO LA 2 Sehemu ya 2

### Ni Lini Kristo Atarudi?

1. Je, watu katika kipindi cha siku za Kristo walitarajia kwamba Ufalme wa Mungu ungesimikwa katika nyakati zao? Luka 19:11. Je, Yesu alisema kitu gani katika kutoa jibu juu ya wazo hili lililokuwa la makosa? Aya ya 12. Linganisha Mathayo 25: 13-30 pamoja na mfano ulio katika Luka 19:11-27.

2. Katika MFANO huu, je, Yesu anajitolea picha yeye mwenyewe kuwa ndiye MTU TAJIRI/KABAILA aliyefafanuliwa katika Luka 19:12?

3. Je, mbingu, kulingana na mfano huu, ndiyo nchi/ufalme wa mbali? Je, Kristo atapokea ufalme akiwa huko mbinguni kisha arudi? Linganisha Luka 19:12 na Danieli 7:13-14. Je, mfano huu hauonyeshi kwa uwazi kabisa hali ya sasa ya zama za kanisa ambayo BADAAYE Yesu atarajea kutoka nchi ya mbali -- Mbinguni?

4. Kulingana na mfano huu, je, kuna kipindi cha wakati ambapo watumishi wanapaswa kufanya biashara na kuzalisha taranta zao? Kulingana na mfano katika Luka, hawa watumishi ni akina nani? Je, Wakristo wanaitwa watumishi mahali popote? 1 Petro 2:16; Yohana 18:36.

5. NI WAJIBU GANI AMBAO WATUMISHI WANATAKIWA KUUTIMIZA kabla ya mwisho wa zama hizi na kabla ya kurejea kwa Kristo mara ya pili? Mathayo 24:14. Je, Yesu aliahidi ataendelea kuwa na kanisa lake katika harakati zao za kuihubiri Injili ya Ufalme hadi mwisho wa zama uwadie? Mathayo 28:19-20.

MAELEZO: SIKU HIZI, Je, makanisa ya Kigiriki - Kirumi yanahubiri injili imhusuyo Kristo binafsi – na wala siyo ujumbe wa Injili ambao yeye alikuja kuuhubiri? Injili zao siyo INJILI YA KWELI YA UFALME WA MUNGU-Wagalatia 1:6. Injili ya Paulo ilikuwa ni ipi? Matendo 28:31.

INJILI ya Ufalme inapaswa katika siku hizi za mwisho, IPELEKWE KWA MATAIFA YOTE KABLA MWISHO haujafika! Mathayo 24:14.

6. Kipindi kifupi baada ya Kanisa la Agano Jipya kuanza, Je, WALIMU WA UONGO waliinuka wakitangaza kwamba siku ya Kristo tayari ilishakuja? 2 Wathesalonike 2:1-2. Je, Paulo alipinga fundisho na imani hiyo kwamba tayari Kristo

alikuwa kesa rudi kwa mara ya pili? Aya ya 2-4.

7. Je, kulikuwa kutokee kuanguka kwenye upotofu -- KUKENGUEUKA – katika nyakati za kuelekea mwisho wa enzi za huduma ya mitume, na pia kabla Kristo hajarejea? Aya ya 3.

8. Je, baadhi ya ndugu katika imani walikuwa wametabiriwa kwamba wangeanguka kutoka katika imani? 1 Timotheo 4:1 ("anguka kutoka katika imani" tafsiri ya neno kwa neno ya Young's Literal Translation imelitafsiri kama; "wataiacha imani").

9. Je, Mtume Paulo alitoa onyo hilo la kuanguka "kutoka kwenye imani" katika 2 Wathesalonike kwa ndugu waliokuwa kwenye imani? 2 Wathesalonike 2:1-4.

10. Sasa ni nani ambaye ndiye ameahidiwa kuokolewa? Mathayo 24:13.

11. Ni lipi jingine ambalo Wakristo wanapaswa walitende? Luka 21:34-36; Mathayo 24:20; Luka 21:27-28.

12. Je, Yesu anakuja kabla ama ni baada ya Dhiki Kuu iliyotajwa katika Mathayo 24:21? Mathayo 24:29-31.

Tambua pia kwamba, kuanguka kutoka kwenye ukweli kunaashiria tu mwanzo wa matukio mengi ya kipindi kirefu, ikiwemo majoribu na vikwazo, kwa kipindi cha takribani miaka1900 kitakachoishia kwenye kurudi kwa Yesu kristo!

### Yesu Anatoa Onyo!

1. Je, siku ya Mungu kuingilia mambo ya dunia na pia kuja kwa Kristo mara ya pili kutakuwa kukitarajiwa na wengi? Mathayo 24: 42, 44. Ama ITAWADIA pasipo KUTARAJIWA na walio wengi? Luka 21:34-35.

2. Kurudi kwake Yesu alikulinganisha na kipindi kipi katika historia ya dunia? Mathayo 24:37. Je, watu kabla ya Gharika walikuwa wanatarajia kwamba Mungu atatumia uwezo wake kuingilia kati maswala yao? Je watu walio wengi wa kipindi hiki wanatabua kwamba Mungu ataingilia maswala ya dunia katika nyakati hizi zetu? Luka 17:26-30.

3. Je, kristo atarejea katika wakati ambao sisi, tungetegemea kuwa atakuja? Luka 12:40. Je, Wakristo wameahidiwa kujua siku na saa ya kurejea kwake? Mathayo 25:13.

MAELEZO: Je, ONYO la Yesu lililenga kipindi chetu – wale watakoukuwa wakiishi "pale ajapo"? Jionee jibu la Yesu katika Luka 12:43 kwa mara ingine tena. Yesu alitisitsizia TU FUATILIE kwa makini MATUKIO YA ULIMWENGU ili pengine hata tutambue kwa kuzielewa ishara, ni mwaka gani anarejea – ili tuweze kuwa tayari pale ajapo.

4. Je, tunaweza KUJUA UKARIBU wa wakati wa kurejea kwake? Mathayo 24:32-34. Je, Yesu tayari kuititia sura hii ametupa ISHARA za nyakati alizokuwa akimaanisha?

5. Je, Paulo alifundisha kwamba Wakristo wa kweli walikuwa nao wakutwe na mwisho pasipo kutarajia? 1 Wathesalonike 5:1-5.

6. Ni kipi ambacho wote Paulo pamoja na Yesu walikufundisha kwamba Wakristo walipaswa wakifanye? 1 wathesalonike 5:6; Marko 13:33-37.

7. Je, Mungu huwa anajiingiza katika maswala ya wanadamu pasipo kwanza kuwafanya WAJUE MPANGO wake? Amosi 3:7 na Isaya 46:10.

Je, kuwa mtendakazi katika kutimiza hatua ya mwisho ya kazi kupitia Kuieneza Injili ya Ufalme kabla ya mwisho wa zama, NDIYO MAANDALIZI ya wakati wa Kristo kurudi kuja kuyatawala mataifa?

8. Baadhi ya madhehebu na vikundi wanaamini kwamba Kristo tayari alisha rudi. Je, Yesu alionya kwamba mawazo kama hayo yangeweza kudaiwa na baadhi kipindi kifupi kabla hajarejea kweli? Mathayo 24:26.

9. Na wakati huohuo, je, wengine wataamini kwamba kurejea kwake bado ku-mbali na ama hata kwamba hawezu kurudi kabisa? 2 Petro 3:4-7 na Mathayo 24:48.

Je, mawazo yoyote kati ya haya yako sahihi?

10. Pamoja na kile ambacho wengine wanakichukulia kuwa ni kuchelewa, je, Yesu hataweza kurudi? 2 Petro 3:8-13.

## Mtiririko wa Matukio Unathibitisha!

1. Danieli anatoa MAELEZO FASAHA ya MFUATANO WA MATUKIO ambayo ni sharti yatokee kabla Kristo hajarejea. Soma Danieli, Sura ya 2, hususan aya ya 44. Gundua MFUATANO WA MILKI ZA KIDUNIA ZA WATU WA MATAIFA kama zilivyozelezeza katika aya ya 36 hadi 42.

2. Wakati wa MUUNGANO WA MWISHO WA WAFALME 10 katika Ulaya, unaowakilishwa na vidole vya miguu (Danieli 2:42) na pembe kumi (Danieli 7:24; Ufunuo 17:12-13), je, Mungu wa mbinguni ndipo atakapousimika Ufalme wake? Danieli 7:7, 17, 18.

3. Je, Ufalme huo utaachiwa tena kwa wanadamu waharibikao wa taifa lingine lolote? Danieli 2:44. Ama Kristo ndiye atakayeuchukua utawala wa Ufalme huo? Danieli 7:13, 14.

4. Katika mfano ulioelezeza katika Injili ya Luka, je, Kristo aliupokea ufalme? Luka 19:11, 12. Je, maeleo haya yote, si kwamba yanahusu ufalme uleule mmoja, Ufalme wa Mungu?

5. Yesu anatoa MTIRIRIKO MWINGINE WA MATUKIO katika Marko 13 na Luka 21. Kabla haujaendelea zaidi, hakikisha unasoma maeneo yote ya sura hizi. Sasa ebu fungua Mathayo 24. Je, Yesu anaelezea kutokea kwa sauti kubwa mno itakayosikika angani? Mathayo 24:30-31. Je, Paulo naye alitaja kupulizwa kwa MLIO WA BARAGUMU/

TARUMBETA /PARAPANDA wakati wa kurudi kwa Kristo? 1 Wathesalonike 4:16.

6. Je, huo ndio wakati wa UFUFUO? 1 Wathesalonike 4:16-17. Ni baragumu/parapanda ipi itakayolia wakati tukio la ufufuo litakapotokea? 1 Wakorintho 15:52.

7. Sasa ebu jione katika Maandiko kile kitakachotoka wakati wa PARAPANDA YA MWISHO. Ufunuo 10:7 pamoja na 11:15. Je, huu ndio wakati wa kurudi kwa Kristo? Na wa ufufuo? Na wa kusimikwa kwa Ufalme? Hili linalezeza kwa ufasaha hasa ni lini Yesu atarejea.

MAELEZO: Katika Ufunuo 11:15-18, Yohana anafafanua tukio lilelile aliloliezeza Paulo katika Wakorintho wa 1. Hivyo tumeona kwamba KRISTO ATAREJEA WAKATI WA MLIO MKUU WA BARAGUMU KUBWA, ambayo itasikika kwa wote walioko katika dunia na wote walijuao hili watatambua kuwa huko ni kurudi kwa Kristo!

## JINSI Kristo Atakavyorudi

1. Je, Kristo atarejea kwa JINSI ILEILE KAMA ALIVYOONDOKA? Matendo 1:11. Je, Kristo aliondokaje? Matendo 1:9. Je, alichukuliwa hadi akapotelea mawinguni? Je, vilevile atarejea katika wingu? Je, Mathayo 24:27, 30, inaeleza nini juu ya hili? Je alipoondoka aliondokea kwenye Mlima wa Mizeituni? Matendo 1:12.

2. Ni nini KITATOKEA KWENYE SIKU ATAKAYOREJEA? Zekaria 14:4. Je, miguu yake itatua na kusimama kwenye MILIMA WA MIZEITUNI katika siku hiyo? "Siku" hapa inamaanisha kipindi kifupi cha muda- siku ya masaa 24. Na ni nani atakayetokea pamoja naye? Zekaria 14:5, maneno matatu ya mwisho.

3. Je, Kristo alipaa kutokea Mlima wa Mizeituni AKIONEKANA waziwazi? Matendo 1:9-11. Je, wote watamuona akija? Ufunuo 1:7. Je, hili sasa linaonyesha kwamba kutakuwa na kunyakuliwa kwa siri kwa watakatifu watoke katika dunia hii?

MAELEZO: Pale Yesu atakaporejea WAZIWAZI na katika utukufu mkuu (Mathayo 25:30-31); atasafiri akiwa na mng'ao na kasi ya RADII, mng'ao utakaoonekana kutoka mashariki hadi magharibi duniani kote, akiwakusanya wateule wake (Mathayo 24:27). Na hii ndiyo njia pekee iwezeshayo kila mtu duniani kote kuweza kumuona akirejea.

Yohana 14:19 hutumiwa kimakosa mara kwa mara katika kujaribu kuonyesha kwamba Yesu atakuja kwa siri na bila kuonekana. Aya hii haisemi kwamba ulimwengu HAUTAMUONA Yesu akirejea. Badala yake inasema kwamba watu waliokuwa wakiishi nyakati hizo – miaka 2000 iliyopita – wasingemuona tena kwa sababu alikuwa anaondoka na kurudi mbinguni. Lakini kwa habari ya kurejea kwake sehemu nyingi zimeeleza wote watamuona!

4. Zingatia 1 Wathesalonike 4:16-17. Ni wakati wa ISHARA gani ndipo Kristo atakaporejea? Je, kutakuwepo na MLIO WA SAUTI KUBWA ili kutangaza kurudi kwake ama atarejea

kwa siri?

5. Je, neno "sisi" lilitotajwa katika 1 Wathesalonike 4:17 linamaanisha yeyote yule ama ni watakatifu – ambao ndio watakaoa FUFULIWA ili kumlaki Kristo arudipo? Je, tangia hapo watakuwa na Kriso daima/siku zote? Aya ya 17. Je, 1 Wakorintho 15:51-52 inaithibitisha pointi iliyotangulia? Ni nani ndiye Mfalme wa Watakatifu? Ufunuo 15:3.

6. Je, MALAIKA WATAKATIFU nao pia WATASHUKA na Kristo pale ajapo? Marko 8:38. Pale Kristo alipokuja hapa duniani kwa mara ya kwanza, je alikuja akiwa na uwezo na nguvuzozote? Ama aliteswa, alidhihakiwa, na alinyanyaswa? Isaya 50:6; Yohana 19:1. Je, kuja kwake mara ya pili atakuja akiwa na NGUVU, UWEZO na UTUKUFU MKUU? Mathayo 24:30. Je, MAJESHI ya malaika yatafuatana naye? Ufunuo 19:14.

7. Sasa tunaona kwamba Kristo pamoja na majeshi ya malaika wake watashuka katika mawingu na kwamba watakatifu (wenye haki – wote walikufa na walio hai) watapaa juu kumlaki angani. Huku KUMLAKI KUTATEKELEZWA NAMNA GANI? Mathayo 24:27. Pale yeze pamoja na malaika wake watakapokuwa wakisafiri KWA KASI KATIKA DUNIA YOTE, ndipo WATAKATIFU toka kila sehemu watakapokuwa wakiungana na kuambatana naye na kudumu pamoja naye tangia hapo.

## TAARIFA HIZI KWA UFUPI

MUNGU ANAO MPANGO! Kupitia kwa manabii ametupa mfuatano wa matukio usiobadirikabadirika, utufikishao kwenye KURUDI KWA KRISTO.

NAMNA Kristo atakavyorejea ni jambo ambalao LIMEELEWEKA KIMAKOSA KWA KIASI KIKUBWA. Atarudi AKIONEKANA waziwazi kwa ulimwengu uliomkataa Mungu ili aje aulazimishe ulimwengu kuwa na amani. Atarejea MWANZONI mwa utawala wa MILLENNIA.

Imani ya uongo ya kwamba makanisa yanaweza kuleta utawala wa amani wa kimillenia kabla Kristo bado hajarejea ni jambo lisilowezekana na ni uzushi mtupu. Matukio ya ulimwengu yanathibitisha hivyo.

Watawala wa kimataifa kwa sasa wametambua kwamba tumaini pekee la kuuokoa ulimwengu dhidi ya kuijangamiza wenye ni kuundwa kwa SERKALI YA ULIMWENGU yenye uwezo mkubwa. Hata hivyo majoribio yote ya kutekeleza hilo yanakwama kutokana na kutokuaminiana, mashaka, ubinafisi, pamoja na chuki. Ukweli wazi ni kwamba MWANADAMU KILA MARA KASHINDWA – na ataendelea kushindwa kulifisia lengo hili.

ASILI YA MWANADAMU HAIJABDIRIKA.

Watu wangali wako tayari kumwaga damu ya wenzao ili tu wakidhi tamaa na matakwa yao. Je, watu wa dunia hii kiukweli wanaijua njia ya kuifisia amani? Mungu mwenyezi

akizungumzia juu ya mwanadamu aliyejaa dhambi kwa ujumla: "wala NJIA iletayo amani hawaijua" (Warumi 3:17). Tunasikia maneno mengi ya majigambo ya wanasiasa juu ya matumaini ya kufikia amani kupitia Umoja wa Mataifa – lakini matokeo yake yakusikitisha yanayathibitisha maneno yaliyovuvuviwa ya Paulo kwamba mtu wa mwilini kiujumla haijui njia ya kuifisia amani.

Historia ya mwanadamu ya majanga aliyojisababishia inapiga kelele kwamba katika kujaribu kujitawalamwenyewe mwanadamu amekuwa akijaribu kisichowezekana. Inaonyesha wazi kwamba akiwa yeze mwenye kama alivyoumbwa kwa sasa, mwanadamu hana nia SAHIHI wala uwezo wa KIAKILI wa kumwezesha kuumudu ulimwengu huu. Makanisa hayawesi kuutiisha ustaarabu wa dunia hii. Ni Kristo ndiye sharti arudi ili aje kuanzisha zama zilizoahidiwa za amani!

Ni kwa nini wanadamu wako katika ujinga juu ya swala muhimu kama hili leo?

Ni kwa sababu wako katika ujinga juu ya nabii zisizoidadi ambazo zinafunua kwa uwazi kwamba Mungu amepanga kwamba Kristo ndiye atakayeitawala dunia hii, atawafundisha kila mtu njia ya kuleta amani, na atamwonyesha kwamba hili litatokea baada ya mfuatano wa matukio fulani – na baada ya mwanadamu kuwa amepitia kipindi atakachojifunza kwa mateso ili aweze kutambua pasipo mashaka kwamba njia za mwanadamu pekee zinapeleka kwenye mauti (Methali 14:12).

ULIMWENGU HAUNA FURAHA leo. Ebu fuatilia tu yale yatokeayo kote duniani jinsi ilivyojaa majanga ya kutisha! Tafakari kuchinjwa kwa kiwango kikubwa kwa wanadamu kulikokuwa kumetabiriwa kungetokea hapo baadaye! Kristo alisema: "Nimekuja ili wawe na uzima [sasa na baadaye], na kwamba wawe nao TELE/ KWA KIWANGO KIKUBWA!" (Yohana 10:10).

WATU WATAKUWA NA FURAHA PALE KRISTO ATAKAPOREJEA KUJA KUTAWALA. Wataishi kwa maisha ya furaha yaliyo TELE! Chini ya uongozi wake mabadiriko muhimu yatafanyika ndani ya wanadamu ili wote waweze kufikia hali hii. "YESU [Mwokozi], . . . atawaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao!" (Mathayo 1:21).

# PENTEKOSTE, NDOTO, PAMOJA NA KARAMA ZA KIROHO



Kielelezo cha kisanaa cha kuonyesha ngazi ya ndoto ya Yakobo (Mwanzo 28:10-17)

Na Bob Thiel

Sikuu ya Pentekoste inaanza Juni 7 na kuendelea hadi machweo ya Juni 8 katika mwaka 2014.

Jione ya yafuatayo kutoka kwenye Sikuu ya Pentekoste ya kwanza baada ya kusulubiwa kwa Yesu na Kufufuka kwake:

1 Ilipowadia siku ya Pentekoste, walikuwa wote mahali pamoja. 2Ghafula sauti kama mvumo mkubwa wa upopo uliotoka mbinguni, ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. 3Zikatokea ndimi kama za moto zilizogawanyika na kukaa juu ya kila mmoja wao. 4Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia.

5Basi walikuwepo Yerusalem Wayahudi wanaomcha Mungu kutoka kila taifa chini ya mbingu. 6Waliposikia sauti hii, umati wa watu ulikusanyika pamoja wakistaajabu, kwa sababu kila mmoja wao aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. 7Wakiwa wameshangaa na kustaaajabu wakauliza, “Je, hawa wote wanaozungumza si Wagalilaya? 8Imekuwaje basi kila mmoja wetu anawasikia wakinena kwa lugha yake ya kuzaliwa? 9Warparathi, Wamedi, Waelami, wakazi wa Mesopotamia, Uyahudini, Kapadokia, Ponto na Asia, 10Frigia, Pamfilia, Misri na pande za Libya karibu na Kirene na wageni kutoka Rumi, 11(Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu sote tunawasikia watu hawa wakisema katika lugha zetu wenyewe, mambo makuu ya ajabu ya Mungu.” 12Wakiwa wameshangaa na kufadhaika wakaulizana, “Ni nini maana ya mambo haya?”

13Lakini wengine wakawadhihaki wakasema, “Hawa

wamelewa mvinyo!”

14Ndipo Petro akasimama pamoja na wale mitume kumi na moja, akainua sauti yake na kuhutubia ule umati wa watu, akasema: “Wayahudi wenzangu na ninyi nyote mkaao Yerusalem, jueni jambo hili mkanisikilize. 15Hakika watu hawa hawakulewa kama mnavyodhania, kwa kuwa sasa ni saa tatu asubuhi! 16Hawa hawakulewa, ila jambo hili ni lile lililotabiriwa na nabii Yoeli akisema,

17“Katika siku za mwisho, asema Bwana, nitamimina Roho wangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu na binti zetu watatabiri, vijana wenu wataona maono na wazee wenu wataota ndoto. 18Hata juu ya watumishi wangu nitamwaga Roho wangu, nao watatabiri”. 19Nami nitaonyesha maajabu mbinguni juu na ishara duniani chini, moto na mvuke wa moshi mnene. 20Jua litakuwa giza mwezi utakuwa mwekundu kama damu, kabla ya kuja siku ile kuu ya Bwana iliyo tukufu. 21Lakini ye yote atakayeliita jina la Bwana, ataokolewa.’

22“Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno haya nisemayo: Yesu wa Nazareti alikuwa mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu kwa miujiza, maajabu na ishara, ambayo Mungu alitenda mionganoni mwenu kwa kupitia yeye, kama ninyi wenyewe mjuavyo. 23Huyu mtu akiisha kutolewa kwa shauri la Mungu lilokusudiwa kwa kujua kwake Mungu tangu zamani, ninyi, kwa mikono ya watu wabaya, mlimwua kwa kumgongomea msalabani. 24Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu akamwondolea uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana yeye kushikiliwa na nguvu za mauti (Matendo 2:1-24).

Siku iliyotajwa hapo juu ya Pentekoste ilianza kwa miujiza. Wanafunzi walizungumza kwa lugha mpya ambapo watu wengine waliwasikia wakizungumza kwa lugha zao wenyewe za asili yao. Petro alisema kwamba Roho ya Mungu ilikuwa inamiminwa na kwamba baadhi ya wafuasi wangeota ndoto na wengine wangetoa unabii.

Kisha, katika Matendo 3:1-10, iliandikwa kwamba uponyaji wa kimiujiza ulifanyika. Wakati wengi wa Wakristo huamini kwamba Mungu aweza kuponya, wengi wamechanganyikiwa juu ya karama za kiroho kama vile ndoto, unabii, pamoaj na tafsiri.

## Vipi kuhusu ndoto, unabii, pamoja na karama zingine za kiroho?

Je, ndoto, tafsiri, na unabii zinayo nafasi yoyote katika kanisa la Kikristo leo? Je, haya yanayo nafasi yoyote kwa wahusiana na Kanisa la Continuing Church of God (ambalo halikuanza rasmi kama chombo kimoja hadi Disemba 28, 2012)?

Biblia inaonyesha kwamba Mungu mara kwa mara alitumia ndoto kupeleka ujumbe mbalimbali (Mwanzo 20:3-7, 28:10-17, 31:10-13, 31:24, 37:5-10, 40:5-18, 41:1-32; Hesabu 12:6; Waamuzi 7:13-15; 1 Wafalme 3:5-15; Danieli 2:3-45, 4:4-27, 7:1-28; Mathayo 1:20-25, 2:12, 2:13, 2:19, 2:22; Matendo 16:9).

Biblia inaonyesha kwamba Mungu mara kwa mara huchagua kufanya kazi na manabii kupidia katika ndoto:

6 "BWANA akasema, "Sikilizeni maneno yangu: "Akiwapo nabii wa BWANA miongan mwenu, nitajifuna kwake kwa maono, nitanena naye katika ndoto (Hesabu 12:6).

Jionee kwamba aya hiijuu inasema kwamba Mungu atazungumza na manabii wake katika ndoto. Fuatilia pia:

28 Mwache nabii aliye na ndoto aseme ndoto yake (Yeremia 23:28).

Miaka michache iliyopita niliota ndoto, ambayo pamoja na kwamba mwanzoni sikuweza kuilewa, kadri ilivyozi kutimizwa baada ya miaka kadhaa, nilianza kuilewa na kuamini kwamba ilikuwa imetoka kwa Mungu.

Wakati huo nilikuwa na miaka 50 (jambo linaloniweka katika kundi la 'wazee' kulingana na Hesabu 8:25; soma Yohana 8:57). Nabii Yeremia wakati fulani alishangazwa na ujumbe aliokuwa ameupokea na baadaye alifikia kuamini ulikuwa umetoka kwa Mungu (Yeremia 32:6-8), naye Mtume Petro angalau mara moja aliona maono ambayo yalimchanganya kuyaelewa (Matendo 10:9-17) hadi na yeye hapo baadaye (Matendo 11:5-17). Hili pia lilimpata Danieli (Danieli 8).

Katika ndoto yangu, kulionekana kama kuna mistari miwili ilio sambamba. Kiongozi wa kundi la Living Church of God (LCG) Roderick Meredith, alikuwa amesimama kwenye mstari wa juu na mimi nilikuwa nimesimama kwenye mstari ulio chini zaidi yake. Katika ndoto, nilikuwa naendelea kumuuta Bwana Meredith, lakini hakuonekana kuitika. Huko kutokuniitika, kwangu katika ndoto kulikuwa hakuna maana yoyote. Kisha baada ya kile kilichoonekana kuwa ni muda mrefu, mistari ile ikapishana kwa mstari wake kushuka chini na ule wa kwangu ukapanda juu!

Moja ya sababu iliyonisababisha nishindwe kuilewa ndoto hii wakati huo ni kwamba nilikuwa katika ukaribu fulani wa kimaongezi na Bwana Meredith kwa muda huo, hivyo maswala ya ndoto hiyo hayakuleta maana yoyote. Vilevile, kwa kuwa sikuwa na kusudi la kujitoa katika kanisa la Living Church of God wakati huo (na wala sikuwa na mipango ya kufungua kanisa tofauti), haikueleweka ndoto ilikuwa inaelezea nini. Sababu nyiningine iliyonifanya nisiwe na uhakika kuhusu ndoto hiyo kwa wakati huo ilikuwa kwamba sikuwa nimewekewa mikono kupokea upako wa Roho Takatifu kuwa mtumishi wa Mungu kwa wakati huo ukiachilia tu ule wa wakati wa kubatizwa.

Lakini maswala haya hatimaye yalibadirika. La kwanza, pasipo kutarajia niliwekewa mikono ili nipokee upako mara dufu wa Roho ya Mungu (soma 2 Wafalme 2:9) siku ya tarehe 15 Disemba, 2011 na Mchungaji wa LCG aliyeitwa Gaylyn Bonjour.

Zaidi ya hapo, kadri muda ulivyozi kwenda, Bwana Meredith alizidi kuwa mbali nami, akawa anashindwa kutunza ahadi mbalimbali alizozitoa kwangu, na hatimaye akaacha kabisa kuzungumza na mimi. Na nilipopokea barua kutoka kwake hapo 28/12/2012, ikawa wazi kwangu kwamba kulikuwa hakuna namna yoyote kwamba joho la Kifiladefia lingeweza kuwa

bado lingali kwake ama hata kwa viongozi wowote waliosalia katika LCG. Matukio haya yaliyojitekeza yalinionyesha kwamba ile ndoto ilikuwa ikitimizwa. Ndoto hii ilitoa ufanuzi wa kile ambacho kingetokea hapo baadaye na hilo limetimia.

Vilevile niliwahi kupata ndoto nyingine (ambayo sikumbuki vema ni lini, lakini ilikuwa kabla ya 2012) inayoendana na maono ya Isaya. Katika ndoto hiyo, ninakumbuka niliitikia wito kutoka kwa Mungu nikasema, "Niko hapa, nitume" (soma Isaya 6:8).

Kuhusiana na ndoto, Biblia pia inafundisha:

28 "Hata itakuwa, baada ya hayo, nitamimina Roho yangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto na vijana wenu wataona maono. 29 Hata juu ya watumishi wangu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile nitamimina Roho yangu (Yoeli 2:28-29).

28 Mungu ameweka katika kanisa, kwanza mitume, pili manabii, tatu walimu, kisha watenda miujiza, pia karama za kuponya, karama za masaidiano, karama za maongozi, aina mbalimbali za lugha. 29 Je, wote ni mitume? Je, wote ni manabii? Je, wote ni walimu? Je, wote wanafanya miujiza? 30 Je, wote wana karama ya kuponya? Je, wote hunena kwa lugha mpya? Je, wote wanatafsiri? (1 Wakorintho 12:28-30).

11 Yeye ndiye aliywewka wengine kuwa mitume, wengine kuwa manabii, wengine kuwa wainjilisti, wengine kuwa wachungaji na wengine kuwa walimu, 12 kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu kwa ajili ya kazi za huduma, ili kwamba mwili wa Kristo upate kujengwa. 13 mpaka sote tutakapoufikia umoja katika imani na katika kumjua sana Mwana wa Mungu na kuwa watu wazima kwa kufikia kipimo cha ukamilifu wa Kristo.

14 Illi tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwatupwa huku na huku na kuchukuliwa na kila upopo wa mafundisho kwa hila za watu, kwa ujanja, kwa kufuata njia zao za udanganyifu. 15 Badala yake, tukiambiana kweli kwa upendo, katika mambo yote tutakua, hata tumfikie Yeye aliye kichwa, yaani, Kristo. 16 Kutoka Kwake, mwili wote huunganishwa na kushikamanishwa pamoja kwa msaada wa kila kiungo, hukua na kujijenga wenyewe katika upendo, wakati kila kiungo kinafanya kazi yake (Waefeso 4:11-16).

Pamoja na kile ambacho Biblia inaeleza, makundi mengi ya Kanisa la Mungu yanaonekana hayakubaliani na kwamba wako manabii leo, na wala hayaonekani kukubaliana na kwamba Mungu nyakati zingine huzungumza kupidia katika karne hii ya 21-wengine, kwa bahati mbaya wanaonekana kuchukizwa na wazo kama hilo. Mojawapo ya sababu zilizoleta haya ni kwamba wale 'manabii' waliojiweka wenyewe mbali na kikundi cha Continuing Church of God mara nyngi wametabiri uongo.

Lakini hili halimaanishi kwamba Mungu huwa hatumii ndoto au hana yeoyote katika ofisi ya nabii. Biblia inaonyesha kwamba Mungu huweza kumimina upako mara dufu wa Roho yake (soma 2 Wafalme 2:9-15) na hili ni sawa na lile lililotendeka pale mtumishi mwenye upako aliponiombea na na kunipaka mafuta matakatifu mnamo Disemba 15, 2011.

Herbert W. Armstrong kuhusu Ndoto

Lakini kwanza, ebu na tuanzie hapa kwa kile ambacho marehemu Herbert W. Armstrong aliandika kuhusu ndoto:

Napaswa niseme hapa kwamba katika kadri ya nyakati 99,999 mionganoni mwa 100,000, pale watu wadhaniapo Mungu anaongea nao katika ndoto ama maono katika nyakati hizi na zama hizi, ni mafikra tupu, ama aina fulani ya kufikirika au kujidanganya mwenyewe. Nimefikia kuamini kwamba ndoto hii ilikuwa ni wito wa kiuwezo kutoka kwa Mungu kutokana na matukio yaliyoifuatia. (Kutoka kitabu: Autobiography of Herbert Armstrong, Toleo la I, sura ya 10).

Na hili liko sahihi. Ndoto zilizo nyingi hazitoki kwa Mungu, hata kama wahusika wanadhani zimetoka kwake. Ndoto kutoka kwa Mungu huonyeshwa kwamba ziko sahihi kulingana na matukio yatakayofuatia (japo si kwamba kwa vile tu ndoto imeishia kuwa ya kweli, hilo peke yake, haliithibitishi kwamba imetoka kwa Mungu kwa kuwa kunaweza kuwa na sababu zingine, soma Torati 13:1-5, lakini ni hakika Mungu mwenyewe wakati mwininge hutumia ndoto, Hesabu 12:6; Matendo 2:17-18).

Ijapokuwa wengi huzipuuza ndoto zote, wengi pia husahau kwamba Herbert W. Armstrong aliamini kwamba mkewe Loma Armstrong aliota ndoto kutoka kwa Mungu, japo ilimchukua miaka mingi kuupokea uhalali wake:

Ndani ya siku 30 au 60 baada ya ndoa yetu Mungu alizungumza na mke wangu katika kile ambacho yaonekana kilikuwa ni ndoto fasaha na isiyo ya kawaida, au ni katika maono — lakini ilikuwa ni baada ya miaka kadhaa baadaye kabla hatujafikia kuelewa dhahiri kwamba huu ulikuwa ni ujumbe toka kwa Mungu. (Armstrong H.W. Barua kwa Washirika na Watendakazi-Pamoja, Novemba 28, 1956; ona pia katika, Autobiography of Herbert Armstrong, Toleo la I, Sura ya 10).

Hivyo, hiyo ilikuwa ni ndoto kutoka kwa mwanamke ambayo ilitangulia mwanzo wa kanisa la Radio Church of God la kale ambalo Herbert W. Armstrong aliliongozoa.

## Je, Mungu Angetoa Ndoto kwa Mwanamke Mwingine?

Swali la kujiuliza ni je, kumekuweko na ndoto zozote kutoka kwa Mungu katika miaka ya hivi karibuni?

Ukiongezea juu ya ndoto zangu (ambazo zilionekana kupatana na Hesabu 12:6, Isaya 6:8 pamoja na Matendo 2:17), yaonekana pia kumekuwapo ndoto nyingine angalao moja inayohusiana na Kanisa la Continuing Church of God, ambayo ningependa niileezee kwa upana ambayo aliota mtu mwininge.

Pasipo mimi kujua hadi mwishoni mwa Septemba 2013, mwanamke aitwaye Fesilafai Fiso Leaana wa New Zealand aliota ndoto pale alipoenda kulala siku ya Disemba 8, 2012. Hapa nakuletea kile ambacho Fesilafai Fiso Leaana alichandika kuhusu ndoto yake:

Miezi kadhaa kabla ya ndoto yangu, mume wangu pamoja na mimi tuligundua uwepo wa mgongano katika mwenendo, kuhusu amri ya sabato katika kanisa la LCG, na tangia hapo tulianza kusali mara kwa mara tukimuomba Mungu atuongoze ambako ukweli uliko. Inaonekana Mungu ametujibu maombi yetu kuititia hii ndoto.

Ndoto ilianza kwa mimi nikiwa na ndugu wengine katika Bwana wa New Zealand wapatao 70 wa kanisa la Living Church of God, kisha ghafla kanisa la LCG likatoweka (nikabaki natafakari kwa mshangao LCG ilikuwa imeenda wapi?) na nikajikuta nimebaki nikiwa nimesimama na watu takriban 10 hivi, juu ya jengo lefu sana. Tulikuwa tumesimama juu kabisa ya jengo hilo, ambalo sikuweza kuona chini yake, kulikuwa hakuna jengo lingine, bali jengo hili pekee. Sikuweza kuona chini ya jengo hilo bali mawingu pekee chini ya jengo hilo na mawingu yakiwa yamelizunguka, kitu kilichofanya mlima mweupe wa kupendeza — mlima ambaa haukuwa na mwisho katika pande zake. Jengo ilikuwa karibu sana na mlima huo, kiasi niliweza kuona kileleni mwa mlima huo. Mlima wote ulikuwa ni mweupe na wa kupendeza sana. Ninakumbuka kwamba nilianza kujawa na furaha na amani. Lakini pia nikawa nawaza ni kwa namna gani tulifikasi juu ya jengo hilo na kustaajabu ni kwa nini kulikuwa hakuna majengo mengine pembedi mwake bali ilionekana kana kwamba mawingu ndio yaliyokuwa yanayaficha/yameyafunika majengo hayo mengine na nikahisi nimehifadhiwa au ilionekana kama niko kwenye sehemu salama. Nikaangalia kunizunguka na kulikuwa na hao watu kama kumi hivi tu, na mtu pekee niliyeweza kumtambua vema alikuwa ni Shirley ambaye alikuwa anaendelea na kazi kwa bidii, wale wengine takriban kumi walionekana wamekaa na wengine wamesimama tu hawafanyi lolote. Hivyo nikazunguka katika jengo hilo nikilitafuta kundi kubwa la LCG, lakini kila mara nilijikuta nimerudi na kumkuta Shirley akiwa katika kazi akifanya aina mbalimbali za kazi peke yake wakati wale wengine waliendelea ama kuketi ama kusimama pamoja nami pasipo kufannya lolote. Nikajiuliza ni kwa nini Shirley alikuwa akifanya kazi kwa bidii. Sikuweza kulipata/kuliona kanisa la LCG.

Kisha ghafla ujumbe ukaja katika fikra zangu: "Iko siri katika mlima huo". Na nikaonekana kujawa na furaha katika kulijua hilo, nilikuwa bado najisikia faraja na bado nikaendelea kuuona mlima mweupe wa kupendeza na nikawa natafakari kuhusu ile siri. Kisha nikauliza: "Siri hiyo ni nini?" Ndipo ule ujumbe ukasema, hakuna yeoyote aijuae siri hiyo kuhusu mlima bali ni wewe pekee ndiye umepokea ujumbe huu kwamba iko siri kuhusu mlima. Kisha nikauliza, 'hiyo siri kuhusu huu mlima ni ipi?' Nikapokea ujumbe ndani ya fikra zangu ulionambia kwamba: "siri kuhusu huo mlima ni Sanduku la Agano (Ark of the Covenant)". Kisha ndoto ghafla ikaisha kwa sababu niliamka kutoka usingizini. Na palepale, nikamwamsha mume wangu na kumwelezea ile ndoto, na nikamwambia mume wangu kuwa ilinikumbusha juu ya pale Mungu alipompatia Musa zile Amri Kumi juu ya mlima na ya kuwa mlima huo nao pia ulikuwa umefunikwa na mawingu.

Siku ileile baada ya ndoto yangu, tukiwa ibadani Bwana Penman alituonya tujihadhari na kile tunachokisoma kutoka kwenye kitabu cha Thiel, kwa sababu LCG hawakubaliani na mambo yote aliyoaandika katika kitabu hicho. Kutokana na hilo nikaliweka jina lako ndani ya moyo wangu kwa vile nilikuwa wakati huo sikuju wewe ni nani.

Kisha baada ya wiki tatu Shirley akawasiliana nami kuhusu maswala yako – kuondoka kwako kutoka kanisa la LCG. Shirley alikuwa amekusanya taarifa zako na yote yaliyokuwa yametukia huhusu wewe na akatupatia sisi waumini wote nakala ya mambo hayo, ambayo baadaye mimi na mume wangu tukaipitia kwa pamoja. Shirley alikazana mara kwa mara kusisitiza kwamba uongozi na usimamizi wa Kanisa la LCG ulikuwa umepotoka sawa na inavyothibitishwa na taarifa za matukio yako. Baada ya hapo ilitulazimu mimi na mume wangu tufanye maamuzi iwapo tutaendelea na Kanisa la LCG ama tuambatane na Bob Thiel (wewe) kufuatana na kwamba tayari, John na Kayla walikuwa wameshaamua kufuatana na wewe.

Tuliamua kuambatana na Bob Thiel na kisha tukaondoka katika kikao hicho lakini barua kutoka kwa Bwana Penman ikifuatiwa na kutembelewa na Mchungaji wa New Zealand, Bwana Paul walijaribu kuzuia kuondoka kwetu kwa kutuasa tusijitoe katika kanisa la LCG kwa kuambatana na wewe. Hili lilitufanya tutafakari kwa makini kabisa kuhusu uamuzi wetu.

Mume wangu pamoja na mimi tukiwa peke yetu, hapo ndipo mume wangu aliposema akiniambia: "Unakumbuka ndoto yako? Hiki ndicho ile ndoto yako inachomaanisha, kwamba tunatakiwa tuondoke katika kanisa hili na kuambatana na Shirley". Hapo ndipo tulipojua cha kufanya. Na ndoto hii ndiyo sababu wengi wetu tulioyo katika eneo la Kiwi tuliomo katika kanisa la CCOG tumejua kwamba tuko katika Kanisa sahihi, kwamba ni Mungu ndiye aliyetuambia tuambatane na kanisa hili. Tuliridhiana na Shirley pamoja na wengine kwamba tutaambatana na Bob Thiel na hapo ndipo mume wangu alipowasimulia ile ndoto kwa mara ya kwanza na kuwaambia kuwa ile ndoto ndiyo iliyopelekea mume wangu na mimi tuazimie kuja.

Akiwa hana maelezo kamili juu ya ndoto hiyo, Shirley ndipo alipoamua kufanya maombi kuhusu hiyo ndoto. Alimuomba Mungu ampe uelewa zaidi kuhusu hiyo ndoto. Kisha ndipo siku iliyoofuata alipokuwa akisoma kitabu cha Zaburi 25:14, AKASHTUSHWA pale aya hii ilipojaa katika fikra zake ikimkumbusha juu ya ile ndoto: "14Siri ya BWANA iko kwa wale wamchao, naye atawajulisha agano lake". (Email iliyyotumwa 9/29/2013).

Ndani ya wiki kadhaa baada ya ndoto hiyo, watu kumi katika New Zealand, akiwemo Shirley Gestro (aliyetajwa kama Shirley katika taarifa hapo juu) walianza kuhudhuria kwenye Kanisa jipya la Continuing Church of God.

Ki-Biblia, milima huweza kumaanisha serkali, utawala, mamlaka (Zaburi 30:7; Isaya 11:9; Danieli 2:35; Zekaria 4:7) na weupe kamili au usafi kama sufu (Isaya 1:18; Ufunuo 7:14, 19:14).

Mawingu yaliyozunguka mlima (ama hata yaliyoko katika kilele chake) yanaweza kuonyesha kutenganishwa—pengine utenganisho uwazuiao wengi wasiuone ukweli wote (soma Ayubu 22:14; Maombolezo 3:44) au utenganisho wa kuzuia kuutambua uongozi wa juu!

Ndoto hiyo yaonekana kuwa ilikuwa ni ishara ya kuthibitisha kwamba Joho la Kifiladefia lilikuwa limeondolewa kutoka kanisa la Living Church of God, na badala yake lilikuwa linahusika na mtu fulani ambaye sasa alikuwa anahusika na Sanduku la Agano. Kabla ya hiyo ndoto Fesilafai Fiso Leaana aliashiria kwamba alikuwa na matatizo na jinsi uongozi wa Kanisa la LCG liliyokuwa linaichukulia Sabato, na hilo ndilo lililokuwa moja wapo ya maswala niliyohusika nayo ndani ya majuma yaliyoambatana na kuanzishwa kwa Kanisa la Continuing Church of God.

Sasa, Mimi (Bob Thiel) sikuwa nimewahi kuisikia, wala kuitafakari ndoto hiyo, hadi Sikukuu ya Vibanda ya Septemba 2013 katika New Zealand (pale mke wangu Joyce pamoja nami tulipoenda huko kuhudhuria Sikukuu ya Vibanda ya mwaka 2013).

Ni kwa nini hili ni la kimsingi na muhimu?

Mnamo mwaka 2006, pale nilipoombwa nitoe mahubiri wakati wa Sikukuu ya Vibanda, fikra zilinjia kwamba sikuwa nakumbuka iwapo katika enzi za WCG, GCG, wala LCG kulikuwa na ye yote aliyekuwa amezingatia agizo lilioko katika Torati 31:10-13 kuhusu kuyasoma "Maneno ya Sheria" yaliyomo katika Kumbukumbu la Torati, kila baada ya miaka saba wakati wa Sikukuu ya Vibanda. Hivyo, pale fursa hii ya kuombwa nitoe mahubiri ilipojitokeza (kule Guatemala mwaka 2006), nilijaribu kupitia kitabu cha Sheria. Katika mwaka 2012, ikanijia akilini kwamba kwa vile hili liliagizwa lifanyike kila baada ya miaka saba, basi ilinipasa kufanya hivyo katika mwaka 2013 (ambao ulikuwa ni mwaka baada ya miaka saba), ila sikuwa na uhakika hili lilitakiwa lifanyikeje. Hata hivyo, mara baada ya Kanisa la Continuing Church of God kuanzishwa, nilielewa namna hili litakavyofanyika wakati wa Sikukuu ya Vibanda ya mwaka 2013.

Baada ya kuwa nimeanza kunukuru Torati 31:10-13 na kuwa nimeanza kukisoma Kitabu cha Sheria kwenye Sikukuu ya Vibanda kule New Zealand mwaka 2013, Fesilafai Fiso Leaana alinijia na akanielezea kuhusu ile ndoto. Tulijadiriana kuhusu baadhi ya vipengele vyake na kuhusu Sanduku la Agano,n.k. Na kama ilivyonekana, moja wapo ya vitu vilivyokuwa vikihifadhiwa katika Sanduku la Agano kilikuwa ndicho hicho "Kitabu cha Sheria" chenyewe (Torati 31:26), ambacho ndicho nilichokuwa nikikisoma na kukifundisha wakati wa Sikukuu hiyo ya vibanda. Huu ni ufunuo ambao, kibinadamu Fesilafai Leaana asingeliweza kuelewa. (Yapo pia maswala mengine yenye matokeo muhimu yahusianayo na Sanduku la Agano ambayo nitajaribu kuyaelezea hapo baadaye).

Matukio yaliyofuatia ndoto hii, matukio ambayo Fesilafai Leaana hangeweza kuyafikiria kwenye tarehe 8 au 9 Disemba 2012, ndiyo yaliyoithibitisha ndoto yake. Hakuwa anafununu yoyote kwamba Kanisa la Continuing Church of God lilikuwa linaenda kuanzishwa, na wakati huo nilikuwa bado sijaamua kwamba nianzishe hadi pale nilipopokea barua ya Disemba 28, 2012. Ndoto ya Fesilafai Leaana ni ushuhuda mwingine juu ya mwanzo

sahih, n.k. wa Kanisa la Continuing Church of God.

Ijapokuwa wengine wamechagua kutoamini taarifa zote kuhusu kwa nini na ni kwa namna gani Kanisa la Continuing Church of God lilianzishwa, kumbuka kwamba Biblia inafundisha:

16 ‘...kwa kinywa cha mashahidi wawili ama watatu kila neno litathibitika’ (Mathayo 18:16).

19 Usipokee shutuma dhidi ya mzee isipokuwa ikiwa zimeletwa na mashahidi wawili ama watatu (1 Timotheo 5:19).

Kwa ujumla, kwa kuwa Gaylyn Bonjour siku zote alielezea wazi kwamba alinitia mafuta kwa kuniombea nipewe ‘upako mara dufu’, kumekuwepo ushahidi wa pili kwa muda mrefu (ijapo watu mbalimbali wanamaoni yao katika kulifafanua hili)

Hata hivyo, pamoaj na ukweli kadhaa, ndoto kutoka kwa Fesilafai Leaana inaonekana kama pengine Mungu alikuwa amepanga kuifanya ieleweke kwa uwazi kwa Wanafiladefia wa kweli (walioko katika vikundi mbalimbali vyta makanisa ya Church of God) ili waweze kuelewa kwamba Joho kiukweli lilikuwa limehamishiwa sehemu nyingine.

Vilevile nilipokea ndoto kutoka kwa mtu ahusianaye na Kanisa la Continuing Church of God kule Africa ambayo ninaichukulia kuwa inawezekana kuwa na umuhimu, na iwapo baadhi ya maswala yanayoihusu yakiidhirisha, ninakusudia nayo kuwaeleza habari zake pia.

Ni dhahiri, baadhi watazipuuzia ndoto pamoja na uthibitisho wake kama ushahidi maalum juu ya swala lolote ambalo hawataki kuliamini.

## Zijaribu Roho, Lakini Uwe Tayari Kuamini

Biblia inafundisha, “zijaribuni roho, ikiwa zimetokana na Mungu” (1 Yohana 4:1). Memba wa zamani wa Bodi ya kanisa la Global Church of God (GCG), ambaye siye sehemu ya Kanisa la Continuing Church of God, aliandika yafuatayo mwishoni mwa mwaka 2013 (Wino mweusi ni wake):

Pale tunapohitaji kujua kile ambacho kinaenda kutokea, Mungu atatuonyesha kupitia mafunuo ya moja kwa moja na kupitia Maandiko sahihi kwa wakati sahihi.

“Hakika Bwana Mungu hatafanya lolote, kabla kwanza hajawafunulia watumishi wake manabii siri yake” (Amosi 3:7).

Agano Jipyota lote liko namna hii...

1 Kor. 14:29-32 “29 Manabii wawili au watatu wanene na wengine wapime yale yasemwayo. 30 Kama mtu ye yote aliyeketi karibu, akipata ufunuo, basi yule wa kwanza na anyamaze. 31 Kwa maana wote mnawezwa kutoa unabii mmoja baada ya mwingine ili kila mtu apate kufundishwa na kutiwa moyo. 32 Roho za manabii zinawatii manabii”.

1 Kor. 14:37-39 “37 Kama mtu ye yote akidhani kwamba yeye ni nabii, au ana karama za rohoni, basi na akubali kwamba haya ninayoandika ni agizo kutoka kwa Bwana. 38 Kama mtu akipuuza jambo hili yeye mwenyewe atapuuzwa. 39 Kwa hiyo ndugu zangu, takeni sana kutoa unabii na msikataze watu kusema kwa lugha...

1 Yoh. 4:1-2 “Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho mwone kama zimetoka kwa Mungu, kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea ulimwenguni. 2 Hivi ndivyo mnavyoweza kutambua Roho wa Mungu: Kila roho inayokubali kwamba Yesu Kristo amekuwa katika mwili yatoka kwa Mungu”.

Tambua: Endapo kusingkuwa na manabii wa kweli, kusingkuwa na haja ya “kuzipima/kuzijaribu roho zao”—kwa sababu kila nabii angekuwa ni “nabii wa uongo”. Lakini kwa vile wapo wote, manabii wa kweli na manabii wa uongo, tunahitaji “kuzijaribu hizo roho”...

Wengi wamesema, “Iwapo Mungu angali akiinua manabii katika kanisa, wako wapi?” Kanisa langu—hata dhehebu langu lote—halimtambui yeyote kuwa ni nabii”. Hata viongozi wetu wa kitaifa hawamtambui yeyote pia. Hiyo ni kwamba “shughuli zinaendelea kama kawaida”, lakini ijapo kwa swala la manabii! Ni muhimu tukumbuke kwamba Mungu huwatuma manabii waje kuzungumza ujumbe wake na kazi yake, ambayo mara kwa mara hupingana na kusudi la viongozi wa kisiasa ama wa kidini...

Karama ya unabii haifungamani na uchunguzi wa kipimo cha ki-electronic, kukosekana kwa mtando, vitendo vyatupi, mbano wa sheria ama tathmini za kidini. Hufanya kazi katika lugha yoyote, mila ama desturi. Hufanya kazi pasipo kujali mataifa mengine ama makanisa yanafanya nini - (Na Edwards N. Hitaji la Manabii zaidi kuliko Unabii. Shepherd’s Voice, Mwaka 2013).

Ndiyo, kwa sababu kiongozi wa kundi hamtambui nabii, hilo halimaanishi kwamba huyo nabii si wa kweli. Makala hii hapo juu pia ilinukuru Maandiko kadhaa yathibitishayo hili.

Lakini andiko moja ambalo halikunukuriwa ambalo wote wanatakiwa kulizingatia ni hili lifuatalo:

41 Mtu ye yote anayempokea nabii kwa kuwa ni nabii, atapokea thawabu ya nabii..... (Mathayo 10:41).

Hivyo, watu wanatakiwa wazijaribu roho (1 Yohana 4:1) na wamkubali nabii kulingana na uthibitisho wa neno lake kama Yesu alivyoelekeza. Watu wanatakiwa “wayachunguze Maandiko” ili waone ikiwa mambo haya ndivyo yalivyo (Matendo 17:11).

Wengi hawaamini kwamba Mungu angetumia Roho yake kuzungumza kupitia manabii leo. (Fahamu, si kwa vile ninasema ama ninaongea kitu fulani HAIMAANISHI nafanya hivyo kama nabii. Sharti niwe ninasoma Maandiko kwa ufasaha ama ninatoa ujumbe uliotoka moja kwa moja kwa Mungu, ambao kikawaida nitautambulisha hivyo, vinginevyo ninaweza na nitafanya makosa. Manabii katika Biblia kusema kweli walitumia mda mchache tu katika maisha yao wakitoa unabii na kiujumla

walikuwa wakijishughulisha na kufundisha Biblia, isipokuwa pale tu walipokuwa na ajira zingine).

Wengi wanatarajia waone ishara za kimiujiza (Mathayo 12:38; 1 Wafalme 19:11-12), lakini ukweli ni kwamba Mungu hafanyi hivyo kila wakati (Mathayo 12:39-42; 1 Wafalme 19:12-14).

Je, wewe waweza kuamini?

## Vipi Kuhusu Tafsiri?

Wengine wameeleza kwamba mtu anatakiwa awe ama ni mchungaji aliyewekewa mikono au mwinjiliti au yuko kwenye kofia nyingine ifananayo na hizi ndipo atakapoweza kutafsiri ndoto na/ama ujumbe mwingle kuteka kwa Mungu.

Lakini kulingana na Biblia haihitajiki iwe hivyo.

Yosefu mashuhuri katika kitabu cha Mwanzo alikuwa ni mtafasiri wa ndoto. Kuhusiana na utafasiri wake wa ndoto za mnyweshaji na mwokaji, nafasi ya Yosefu ilikuwa ni mfungwa tu (Mwanzo 40:1-22). Biblia haielezi kwamba Yosefu alikuwa na wadhifa wa aina yoyote ya kiroho alipofanya hivyo.

Danieli naye pia alikuwa ni mtafasiri wa ndoto. Alikuwa ni mateka na wadhifa wake waweza kuwa ulikuwa ni mshauri kwa kiongozi mmoja ama wengi wa serkali (Danieli 1:3-7). Kwa taarifa yako, niliteuliwa na kiongozi mkuu wa LCG (Mwinjilisti Roderick C. Meredith, kuwa mshauri wa Wainjilisti wa kanisa la hilo hapo mwaka 2005. Kuzungumza kiroho, wadhifa huo haukuwa duni kuliko wadhifa wowote ambao Danieli alikuwa nao wakati anaelezwa kuwa alikuwa mtafasiri ndoto (Danieli 2:1-45).

Zaidi, Agano la Kale liko wazi kabisa kwamba mtu hahitaji awe na wadhifa maalum ndipo aweze kuwa mtafasiri ndoto. Fuatilia yafuatayo:

13Gideoni alifika wakati huo huo kukiwa na mtu mmoja aliye kuwa anamweleza mwenzake ndoto yake, akisema, "Niliota ndoto, tazama mkate wa shayiri ulioviringana ulianguka katika kambi moja ya Wamidiani, ukaipiga na ikaanguka nao ukaipindua juu chini na hema ikaporomoka chini."

14Rafiki yake akamjibu, "Habari hii si kitu kingine zaidi ya upanga wa Gideoni mwana wa Yoashi, . Mungu amewatia Wamidiani na jeshi lote mkononi mwake."

15Gideoni alipoisikia hiyo ndoto na tafsiri yake, akamwabudu Mungu. Akarudi kwenye kambi ya Israeli na kusema, "Inukeni! BWANA amelitia jeshi la Wamidiani mkononi mwenu" (Waamuzi 7:13-15).

Neno 'rafiki' siyo rasmi, lakini limetumika kuonyesha kuwa huyo rafiki yake alikuwa ni "Mtafasiri" ndoto.

Zaidi, katika Agano Jipy, mke wa Pilato anaonyeshwa kuwa aliota ndoto na akapewa tafsiri yake ambayo Biblia yaonekana haikutaka kuiweka wazi (Mathayo 27:19). Haonekani kuwa alikuwa na wadhifa wowote wa kibiblia na inawezekana kabisa kwamba hata alikuwa ni mpagani.

Kwa kuongezea, wakati Agano Jipy halitaji zaidi ya mtafasiri wa ndoto lilikuwa na jina jingine kwa watu hawa, linazungumzia juu ya watafasiri wa ndimi/lugha. Fuatilia kile ambacho Mtume Paulo alichandika:

27Kama mtu ye yote akinena kwa lugha, basi waseme watu wawili au watatu si zaidi, mmoja baada ya mwingle na lazima awepo mtu wa kutafsiri. 28Lakini kama hakuna mtu ye yote wa kutafsiri, hao watu na wanyamaze kimya kanisani na wanene na nafsi zao wenywewe na Mungu (1 Wakorintho 14:27-28).

Hapa Paulo anawaandikia Wakristo walioongoka. Hivyo, ninaamini kwamba Agano Jipy linaruhusu yeyote aliye na Roho Takatifu ya Mungu kutafsiri endapo watajisikia wanaongozwa kimakini kufanya hivyo. Wote mimi na Solomona Leaana (mume wa Fesilafai Fiso Leaana) aliyeitafasiri ndoto nilioyelezea katika makala hii tulibatizwa kwa usahihi na tukawekewa mikono kupokea ujazo wa Roho Takatifu. Alikuwa ni Solomona Leaana ambaye ndiye aliitafasiri ndoto ya mke wake akiifanua kwa usahihi kwamba ilikuwa ikielekeza kwangu na kwa kanisa la Continuing Church of God, hivyo haikuwa mimi ambaye mwanzoni nilifanya hivyo. Kumbuka Yesu alisema kwamba: "Kwa vinywa vya mashahidi wawili ama watatu kila neno litathibitika" (Mathayo 18:16).

Wakati mtafasiri anaweza kabisa kukosea, Maandiko yako wazi na hayaonyeshi kama inahitajika mtu awe na wadhifa fulani ndipo aweze kuwa mtafasiri sahihi.

## Vipi Kuhusu Karama Zingine za Kiroho?

Biblia inafundisha kuhusu karama zingine za kiroho, kama vile kupambanua roho, inayowenza kuwa inahusiana na kutafasiri:

9Haya ndiyo maombi yangu kwamba upendo wenu uongezeke zaidi na zaidi katika maarifa na ufahamu wote, 10ili mpate kutambua yale yaliyo mema, mkawe safi, wasio na hatia hadi siku ya Kristo, 11mkiwa mmejawa na matunda ya haki yapatikanayo kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa za Mungu (Wafilipi 1:9-11).

Tambua kwamba Paulo alihuisha kuwa na haki na upendo wa kweli, elimu sahihi, pamoja na kupambambanua kuliko sawa. Hizi ni karama (vipawa ama zawadi) muhimu za Roho (soma 1 Wakorintho 12:1-11).

Angalia pia yafuatayo:

8Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, 9si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. 10Kwa maana sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili tupate kutenda matendo mema, ambayo Mungu alitangulia kuyaandaa tupate kuishi katika hayo (Waefeso 2:8-10).

Si tu kwamba tunahitaji karama/zawadi ya imani ihusianayo na wokovu, tunahitaji pia wokovu ili tuweze kuishi katika njia ya Kikristo.

Mtume Paulo alizidi kufundisha:

1 Fuateni upendo na kutaka sana karama za roho... 12 Vivyo hivyo na ninyi. Kwa kuwa mnatamani kuwa na karama za rohoni, jitahidini kuzidi sana katika karama kwa ajili ya kulijenga kanisa (1 Wakorintho 14:1, 12).

Zaidi akazidi kuandika kuhusu aina mbalimbali za karama/zawadi za kiroho, huku akitoa tahadhari:

1 Basi ndugu zangu, kuhusu karama za rohoni, sitaki mkose kufahamu.....

4Basi kuna aina mbali mbali za karama, lakini Roho ni yule yule. 5Pia kuna huduma za aina mbalimbali, lakini Bwana ni yule yule. 6Kisha kuna tofauti za kutenda kazi, lakini ni Mungu yule yule atendaye kazi zote kwa watu wote.

7Basi kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa faida ya wote. 8Maana mtu mmoja kwa Roho hupewa neno la hekima na mwingine neno la maarifa kwa Roho huyo huyo. 9Mtu mwingine imani kwa huyo Roho na mwingine karama za kuponya. 10Kwa mwingine matendo ya miujiza, kwa mwingine unabii kwa mwingine kupambanua roho, kwa mwingine aina mbali mbali za lugha, kwa mwingine tafsiri za lugha. 11Haya yote hufanywa na huyo huyo Roho mmoja, Roho naye humgawia kila mtu, kama apendavyo mwenyewe (1 Wakorintho 12:1,4-11).

22Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, 23upole, kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria. 24Wote walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na tamaa zake. 25Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, basi na tuenende kwa Roho. 26Tusijisifu bure, tukichokozana na kuoneana vivu (Wagalatia 5:22-26).

Wakristo wa kweli wanayo mojawapo ama zaidi mionganoni mwa karama hizi za Roho. Na wakati mwingine, huwa hatuwezi kujitambua hadi baadaye juu ya ni nini ndizo karama za kiroho ama uwezo. Lakini Wakristo wanapaswa "kukua katika neema na kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo" (2 Petro 3:18), na hiyo elimu (kumjua) ni moja wapo ya zawadi za kiroho (soma 1 Wakorintho 2:10-14). Sisi sote tunapaswa tuwe na upendo, furaha, amani, hekima, imani, n.k.

Fahamu, hata hivyo kwamba, wakati Mtume Paulo anafundisha kwamba sote tutamani karama zilizo muhimu, ni upendo ndio wenye faida:

12:31 Basi tamanini sana karama zilizo kuu. Nami nitawaonyesha njia iliyo bora zaidi.

13: 1 Hata kama nitasema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa kengele inayolialia au toazi livumalo. 2Ningekuwa na karama ya unabii na kujua siri zote na maarifa yote, hata kama nina imani kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, mimi si kitu. 3Kama nikitoa mali yote niliyo nayo na kama nikijitolea mwili wangu uchomwe moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu.

4Upendo huvumilia, upendo hufadhili, upendo hauoni vivu, hauna majivuno. Upendo hauna kiburi. 5Haukosi kuwa na adabu. Upendo hautafuti mambo yake, haukasiriki upesi, hauweki kumbukumbu ya mabaya. 6Upendo haufurahii mabaya bali hufurahi pamoja na kweli. 7Upendo huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahimili yote.


8Upendo haushindwi kamwe.....

13Basi sasa, yanadumu mambo haya matatu: Imani, tumaini na upendo. Lakini lililo kuu mionganoni mwa haya matatu ni upendo (1 Wakorintho 12:31; 13:1-8, 13).

Upendo ndiyo karama ya kiroho muhimu zaidi tunayoweza kuidhihirisha na kuiendeleza.

Wakati wa haya majira ya Pentekoste, tafakari kwamba Mungu yu angali akiwa kwenye Kiti chake cha Enzi, bado angali akimimina Roho yake, na sisi sote tunahitaji kuudhihirisha zaidi upendo wa Mungu. Ikiwemo kuyapenda maneno yake kwa kiwango kitoshacho kutuwezesha tuwe na imani ya kuusadiki ukweli kumhusu yeeye pamoaja na kuhusu karama zake za kiroho na kutembea kama Wakristo.

# JE, UNAJISUKUMA TU “UKIVUMILIA HADI MWISHO?”



(Mchoro na Everkinetics)

Na Richard A. Wiedenheft

*Baadhi katika Kanisa la Mungu kiujumla wamekusudia “kung’ang’ana tu” hadi Kristo arejee. Kwa kuonekana, wana “VUMILIA hadi mwisho” (Math. 24:13) – lakini si kwa namna ambayo Kristo alikusudia. Je, wewe nawe unayafanya makosa yao?*

TAFAKARI nyakati za nyuma punde kabla hujakutana kwa mara ya kwanza na ujumbe uliokuwa ukihubiriwa na Kanisa la Mungu. Yawezekana wakati huo maisha yako yalikuwa yamefikia kuwa ni ya kukatisha tamaa na yasiyo na mwelekeo. Ulikuwa na matatizo na mashaka. Uliona kuna kutokuwa na haki na kuwepo kwa maovu kote kukuzungukako. Pengine hata ulijiliza, “haya yote yana maana gani?” Kitu fulani kilikuwa kinapelea!

Na baadaye ukaja msisimko na kuchalenjiwa na ukweli wa Mungu. Ndani yake ukaona majibu kwa mashaka mengi yaliyokuwa yanaumiza, ufumbuzi kwa matatizo - sahihi, chanya, kanuni zitekelezikazo ziwezazo kuyafanya maisha yako yawe yenye maana, yenye furaha na yaliyotoshelezwa.

Ndipo ukaikamata njia ya Mungu kwa shauku na ukaziweka kanuni hizo za maisha katika njia zako – ukiwa tayari kuachana na mambo uliyokuwa unayapenda, pengine hata ajira yako, rafiki zako, na hata familia yako. Lakini hili lilikuwa na thamani ya kukuwezesha uwe tayari kujitoa mhanga kwa sababu maisha yako sasa yalipata maana sahihi na mwelekeo bora - ukiwa pia umepewa ahadi ya kuupata uzima wa milele. Ukajaa msukumo kwamba Mungu huuita “upendo wa kwanza” kwa ukweli wake.

## Mazoe ya Maisha ya Kikristo

Kadri siku, majuma na miezi ilivoyozidi kuyoyoma, ikatokea, ukagundua kwamba bado ulikuwa ndiye yuleyule, kwamba

maisha bado yalikuwa yanaleta mkanganyiko, kukatishwa tamaa pamoja na maumivu ya moyo. Hata kama u Mkristo aliyeongoka na kubadirika, uliendelea kupambana na majoribu na mitihani, ambayo baadhi yake ilikuwa mizito mno na ya kuchosha.

Na ndipo “upendo wako wa kwanza” ukaanza kupungua, msisimko wako wa awali wa kama mtoto sasa ukapambana na hali ya kiutu uzima ya kutambua kwamba njia ya Mungu si kama vile uganga ama suluhisho la kimiujiza kwa matatizo yote – kwamba inahitajika juhudu kubwa kwa upande wako.

Je, sasa wewe u mmoja wa wale ambao kwa ujumla “wanangojea tu” – ukiyavumilia matatizo na mapungufu yako – ukitaraji kwamba kwa namna fulani, pale Kristo atakapotokea kwenye mawingu, mwelekeo wako wote wa kimawazo ghafla utabadirishwa? Je, unautarajia Ufalme wa Mungu kukuletea “furaha ya ghafla?”

Wapendwa, msidanganyike. Mungu hatayamaliza matatizo yenu yote, majoribu na mitihani kwa ajili yetu pale tutakapokuwa tunapaa kumlaki Kristo mawinguni – tunatakiwa tuwe tukifanya jitihada kupambana na kuyashinda muda huu, kwa jitihada zetu wenyewe zilizozidishwa na kufanywa timilifu kwa msaada wa kiroho wa Mungu!

Mungu kaahidi maisha ya milele ya kiroho pamoja na kutawala katika Ufalme wake kwa wale tu ambao katika maisha haya wamejipatia tabia ya haki ya kiroho – wale waishio kwa upendo, shangwe, amani, furaha pamoja na kushinda na kuyatatura matatizo sasa hivi!

## Watu wa Mungu wanatakiwa kuwa wenye furaha

Yesu alifafanua kwa wanafunzi wake kwamba yule aliye mwaminifu katika machache ndiye anaweza kuwa mwaminifu katika mengi pia (Luka 16:10). Endapo tutajifunza hapa na sasa kuishi maisha yaliyojaa furaha, na yenye malengo maalum, tukaweza kudhibiti na kushinda matatizo yetu, Mungu atajua tunaweza kuwa wenye furaha kwa milele yote katika Ufalme wake.

Katika Yohana 10:10 Kristo aliwaambia Mafarisayo: “Mimi nimekuja ili wawe na uzima, na kisha wawe nao tele”. Mungu alikusudia maisha yetu ya kimwili yawe yenye kuridhisha kwa kiwango kikubwa – siyo lazima yowe yamejaa utajiri na mali za kidunia, bali yajae upendo, shangwe, amani na furaha.

“Upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi . . .” ni mionganii mwa matunda ya Roho ya Mungu (Gal. 5:22-23). Tambua kwamba upendo, furaha pamoja na amani ndiyo yaliyotangulia kwenye orodha hii. Haya yanahuusu kazi za kiroho ambazo ndizo Mungu anatupima kupitia kwazo.

Je ni kweli tunaweza kudhihirisha upendo, furaha, na amani iwapo tunakaa na “kungoja muda ufile tu”? Kwa dhahiri hapana. Kuandamana na mapungufu yetu na kuruhusu mazingira yaliyo chini ya uwezao wetu yatupeleke huku na kule - tukitaraji kwamba Kristo atarejea kabla uvumilivu wetu haujakoma – siyo njia ya kutupeleka kwenye amani na furaha!

Pale Kristo arudipo anataka awakute watumishi wake "wanafanya hivyo" (Math. 24:46) – wanajibidisha na kupambana katika kufanya mabadiriko ya udhaifu wao wenyewe; kiujumla wakiwa wanatatu matatizo – si kwamba wanaangalia "nyakati pekee", huku wakiendelea kuishi na mapungufu yao – siyo wawe wakimtegemea mwagine awasukume kwenda kwenye kuyashinda. Anatarajia aje akute ndani yetu kuna furaha izidiyo kuongezeka pamoja na malengo yajayo pale tu panapokuwepo kukua kiroho.

Jitathmini.

Je, unaweza kusema kwamba tangia ulipoingizwa kwenye Kanisa la Mungu umebarikiwa sana – na kwamba unaendelea kubarikiwa zaidi na zaidi kiroho muda wote?

Iwapo siyo, basi fahamu kuna jambo lenye mapungufu.

Endapo haujisikii kuwa aliyebarikiwa sana na mwenye furaha – na anayezidi kuwa hivyo kadri muda unavyozidi kupita, yawezekana unaweza kuwa "umeikosa mashua"!

## Majaribu, Ndiyo! Huzuni, hapana!

Ni dhahiri Mungu aliahidi majaribu na dhiki kwa Wakristo wa kweli. Yeyote atakayeishi maisha ya kimungu atarajie nyakati ngumu.

Lakini hata katika wakati wa kuyakabiri majaribu, Mkristo hatakiwi kuwa mwenye huzuni na aliye changanyikiwa. Yakobo aliagiza, "Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha tupu mnapopatwa na majaribu mbalimbali, 3kwa sababu mnajua ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi" (Yakobo 1:2-3).

Hakuna janga ama kikwazo kionekanacho kutufanya tupige kelele kwa shangwe – angalau ni vigumu katika hali ya kimwili. Lakini tumeagizwa na Mwumbaji wetu tufurahie kiujumla kuhusu uimara amba jaribu linaweza kutuletea. Tunaweza kuwa na maono na matarajio ya kujua kwamba Mungu anadhibiti mambo yote, akiruhusu tatizo pale tu ajuapo hatimaye litatuletea baraka ya kiroho.

Majaribu yaweza kuwa machungu mno; lakini haimaanishi yatuharibie kuridhika kwetu na furaha tulio nayo katika kujua kwamba tunapitia sasa mafunzo ya namna ya kuishi ili baadaye tuweze kutawala milele pamoja na Kristo.

Hakuna chochote kinatakiwa kiyafunike maono yetu juu ya lengo letu. Hivyo, hakuna kiwezacho kuharibu furaha yetu! Kristo aliwaasa wanafunzi wake: ". . . msifurahi kwa kuwa pepo wachafu wanawatii" (ama kwa ajili ya uwezo wowote wa kufanya miujiza mlionao) – "bali furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa mbinguni" (Luka 10:20). Hilo ndilo sababu yetu ya kuwa na furaha kubwa, pasipo kujali mazingira yetu ya kimwili.

## Uwe Aliyeongoka kwa Kiwango Kikubwa

Ingawa baraka za muda za kimwili za maisha haya zinaweza kuongezea furaha yetu, hatutakiwi kuruhusu kutokuwa nazo ama shauku ya kuzipata iharibu ama kuondoa furaha yetu.

Kusiwepo na kujaribu kuyafanya maisha yetu na furaha yetu zitegemee vitu ambavyo vyawenza kuondolewa kwetu kwa urahisi, tusiachie hilo lifaulu.

Lakini kufaulu kuzihamisha fikra zetu zisijikite kwenye vitu vya kimwili vya ulimwengu huu, sharti tuwe tumeongoka kwa kiwango kikubwa – sharti tujibidishe kujiondolea tabia, tamaa, na matarajio yetu ya maisha ya kimwili. Sharti tuelewe na kudharau umwili tunaouona ndani ya fikra zetu wenyewe. Ni sharti tuwe tayari kupokea kusahihishwa na kukili udhaifu wetu na mapungufu.

Tunatakiwa tumuombe Mungu ili atuonyeshe makosa na mapungufu yetu, atusahihishe katika huruma yake; na pia tunatakiwa tuwaombe Watumishi wa Mungu watusaidie tuweze kuona pale tunapotakiwa kubadirika.

Kukiri makosa na kupokea kusahihishwa, kisha kujibidisha kushinda, sharti liwe ndilo mapambano yetu ya kilasiku- tukijuwa kwamba tunafaulu kwa ajili ya lengo la milele ambalo ndilo msingi wa furaha yetu. Tukiwa na kusudi hili la kiroho miyoni mwetu, tutaweza kushukuru kwa kiwango kikubwa kwa kila baraka za kimwili ambazo Mungu ametujalia na tutaweza kuzitumia kikamilifu. Dhambi pamoja na huzuni huja kutokana na matumizi mabaya ama kutomshirikisha Mungu- bali furaha, amani na shangwe huja kutokana na uelewa sahihi pamoja na matumizi ya vyote ambavyo Mungu ameviumba.

Furahia ladha ya chakula kitamu; sisimuka kwa muziki mzuri; vutiwa na ushirikiano unaoupata kutoka kwa wanafamilia wengine wa Kanisa la Mungu; shukuru kutokana na utukufu wa viumbe vya Mungu. Katika kiwango sahihi burudishwa na yote ambayo yanatokana na uumbaji wa Mungu wa kimwili, lakini siku zote utafute kwanza Ufalme wake (Math. 6:33).

## Yatattue Matatizo Yako

Kama wakristo wa kweli, kwa kweli tunatakiwa tuyatattue matatizo ya maisha haya. Usifikiri ama kusema, "Siwezi kufanya mambo kwa namna nyingine. Hivi ndivyo mimi nilivyo," au, "siwezi kabisa kujizua pale hali inapokuwa hivi" – wala usijiachie kuanguka katika hali ya kutofanya lolote.

Wengi wetu tunaridhiswa mno na nafasi ya pili – tukiwa kwenye ndoa ambayo hairidhishi kwa kiwango kitakiwacho, tukiwa wqenye watoto amba si watifu kikamilifu. Tunahama kutoka ajira moja hadi nyingine pasipo kuwa na mwelekeo. Tunayaruhusu mazingira kuyaendesha maisha yetu. Tunateleza kutoka mshahara mmoja hadi mwagine tukiwa tu tunajaribu kupata malipo yatakayotuwezesha tusizame kwenye maji. Tunaruhusu maumbile ya miili yetu kubakia manene sana, au makondefu kuptita kiwango, au yakiwi katika maumivu, wakati hilo liko ndani ya uwezo wetu kusahihishwa hali hiyo – endapo tu tutaweka jitihada kujiondoa katika hali hiyo.

Je, unaboresha na kutumia fikra zako, ukipanua mipaka yako ya kiufahamu, ukijifunza, fani ambazo hapo awali ulizipuuzia ama hukuwa na fursa nazo? Ama pia, pengine tayari una upenzi na mambo mengi mno na hivyo wahitaji kupunguza baadhi yake na kuanza kujikita zaidi katika fani maalum.

Tukitambua, kuna vikwazo kwa yale tuwezayo kuyabadirisha katika maisha haya – lakini sasa je, tunajibidisha kubadirika kwa kiwango sahihi? Ni ukweli kwamba mabadiriko siku zote huchosha, husumbua, na ni bugudha, lakini kiukweli je, tunayapima kulingana na tunavyotarajiwa kwa ajili ya shangwe ijayo?

Je unayatatu na kuyashinda matatizo-ukiyaweka nyuma yako kuwa yamemalizika na kupita? Ama unajihuisha na shindano jepesi la uvumilivu?

### **Tafakari yaliyo Chanya**

Kawaida ya wanadamu wengi ni kuangalia na kuona upande wa mapungufu wa mambo zaidi. Hailishi wewe ni nani, siku zote unaweza kukutana na kitu cha kukukatisha tamaa mbele yako iwapo utataku kuwa hivyo. Kila siku kuna shida na matatizo ulimwenguni, katika taifa lako, katika kila jamii. Kuna maumivu na kuumwa kichwa, kuvunjwa moyo na kukatishwa tamaa katika maisha yetu ya kila siku.

Bali kitu kimoja ni hakika: kuwazia na kulalamika kuhusu matatizo haya, kuyatafakari bila kikomo, kukosa furaha kwa ajili yake na kulalama, hakutaya fanya yaondoke.

Hivyo sasa ni nini tunatakiwa tufanye?

Tunahitaji kujifunza kuyaweka matatizo yetu katika mikono ya Mungu kuitia maombi na kutafakari upande wa chanya wa maisha yetu na njia yake. Sisi mionganini mwa watu wote ndio tujuuo sisi ni nani – tunajua ni wapi tuendako. Tunayo ahadi njema kwamba: “. . . Mungu hutenda kazi pamoja na wote wampendao . . .” (Rum. 8:28). Mbele yetu lipo lengo kuu kuliko yote ambayo mwanadamu anaweza kuwazia – Kusudi lilioahidiwa la kuingia kwenye familia ya Mungu na kuishi humo milele.

Wapendwa, hebu na tuwazie zaidi yaliyo chanya!

Ebu na tuidake tena nguvu na furaha ya awali tulioipokea pale tulipoanza kutembea katika njia ya maisha ya Mungu.

Kumbuka, maisha haya ya kimwili ni chuo na ni majoribio kwa ajili ya maisha ya kiroho ya milele katika familia tukufu ya Mungu. Furaha ya milele itatolewa kwa wale tu ambao watajifunza kuwa na furaha ya kweli hapa na sasa!

Mwanzioni ilichapishwa kama “ Je, unajisukuma tu katika “kuvumilia hadi Mwisho?”, gazeti la Good News, July – September 1973, Kurasa 24-25.

## **EVANS OCHIENG NA KANISA LA CONTINUING CHURCH OF GOD**



*Na Evans Ochieng Kisiengo.*

Mimi nilizaliwa katika familia ya Prisila Oloo na Christopher Kisiengo. Wazazi wangu walikuwa ni waumini wa Kanisa la Kikatholiki waliokuwa wakishika Jumapili. Hili ndilo dhehebu nilipokulia kwa vile ndilo pekee lililokuwepo katika eneo letu. Kitu cha ajabu ni kwamba mimi sikuwahi kubatizwa katika hiyo imani ya Ukatholiki!

Nilijaribu kutaka kubatizwa mara kadhaa pale dada yangu mkubwa pamoja na rafiki zangu walipokuwa wakienda kubatizwa, lakini kuna kitu fulani ambacho siku zote kilizua nisibatizwe. Siwezi kueleza ni kwa nini, maana yaonekana kulikuwepo na kitu nisichokielewa ambacho ndicho kilizua nisibatizwe.

### **Baada ya kusikia Mahubiri na Maandiko Fulani, Nikawa Mpentekoste**

Hatimaye, nilikutana na mhubiri fulani wa Kipentekoste alipokuwa akifundisha juu ya ubatizo, akisisitiza kwamba ubatizo wa kweli ni lazima ufanyike tu ndani ya mto wa maji mengi au ziwa, si kwa maji kidogo ndani ya bilauri au chombo; nilistaajabu kwani alielezea jinsi Yesu alivyobatizwa ndani ya mto na si kwa kunyonyiziwa maji kwenye uso au kichwani.

Ndipo akasoma kutoka Maandiko yafuatayo: 1 Yohana 2:6: (Yeyote asemaye kuwa yeye ni Mkristo, inampasa aishi na kuenenda sawa na Kristo alivyoenenda). Zaburi 119:105 (105Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga katika njia yangu). Zaburi 119:106: (106Nimeapa na nimethibitisha,

kwamba nitafuata sheria zako za haki). Nilishtushwa niliposikia maandiko haya yote na tangia hapo nikageuzea moyo wangu kwa kuuacha Ukatholiki na kuamua kuwa Mpentekoste, ambako baadaye nilibatizwa kwenye maji mengi. Hili lisababisha mtafaruku mkubwa baina yangu na wazazi wangu, lakini katika yote haya, nilikuwa na furaha ya kwamba mimi nimekifanya kile

ambacho Yesu alikifanya.

Nilijaribu kuongea nao juu ya huu ubatizo unaoagizwa na Biblia lakini hawakuweza kunisikiliza kwa sababu aina hii ya ubatizo ilikuwa kinyume kabisa na jinsi walivyozea katika Ukatholiki. Kule kwenye Ukatholiki, hatukuwa tunaruhusiwa kuisoma Biblia, na tulifundishwa kwamba endapo tutaisoma tunaweza kuugua na hata kufariki.

Hivyo kutohana na hilo nilikuwa mwoga sana wa kuisoma Biblia, maana tulikuwa tumeelezwa kwamba ni mapadre (wachungaji) pekee ndio wanaruhusiwa kuisoma Biblia. Kutohana na hili, tulikuwa tukitembea gizani tu kwa kutokujua kile ambacho kilikuwa kimeandikwa katika Biblia. Tulichokuwa tukifuata ilikuwa ni maelekezo kutoka kwa mapadre peke yake. Vilevile tulikuwa haturuhusiwi kusoma kitabu chochote kutoka dhehebu lingine lolote isipokuwa Katholiki tu. Hivyo tulikuwa katika giza nene kwa kuwa hatukuweza kujua kile kilichokuwemo ndani ya Biblia.

Pale nilipojunga na Upentekoste, nikawa huru kuisoma Biblia. Na nilifundishwa kwamba ninapaswa kuongozwa na Biblia kwa kuwa ndio ilioandikwa kwa pumzi ya Mungu na hivyo Maandiko yote yaliongozwa na BABA MWENYEZI wa JUU (MUNGU MWENYE UWEZO) (2 Petro 1:201:-Kwa maana hakuna unabii wowote uliomo katika Maandiko ambaa uliandikwa kwa mawazo ya nabii mwenyewe. Ilikuwa ni Roho Takatifu ndani yao iliowapa ujumbe wa kweli kutoka kwa Mungu). Na huu unabii unasaadia katuongoza, katuonya na kutufundisha (2 Timotheo 3:16). Biblia yote ilitolewa kwetu kwa uvuvio wa Mungu na inafaa kwa kutufundisha kile kilicho kweli na kutufanya tutambue kile kisicho sahihi katika maisha yetu; inatutia nguvu na kutusaidia tuweze kufanya kile ambacho ni sahihi).

## Kisha Nikajifunza kuhusu Sabato

Nikawa nimefanyika Kiongozi wa Vijana wa Kipentekoste na nikiwa katika wadhifa huo, nilikuwa nikiisoma Biblia kila siku. Kilamara nilipokuwa najifunza Biblia, niligundua kwamba Biblia inatuagiza tuishike Sabato na siyo Jumapili, kwa kuwa ni sehemu ya Amri Kumi za Mungu:

8 Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. 9 Kwa siku sita utafanya kazi zako zote, 10 lakini siku ya saba ni Sabato kwa BWANA Mungu wako. Siku hiyo hutafanya kazi yo yote, wewe wala mwana wako au binti yako, wala mtumishi wako wa kiume au wa kike wala wanyama wako, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. 11 Kwa kuwa kwa siku sita, BWANA aliumba mbingu na nchi, bahari na vyote vilivymo ndani yake, lakini akapumzika siku ya saba. Kwa hiyo BWANA akaibariki siku ya Sabato na kuifanya takatifu (Kutoka 20:8-11).

Na pia ni ishara kati ya Mungu na wanadamu:

“12Pia niliwapa Sabato zangu kama ishara kati yangu nao, ili wapate kujua kuwa Mimi BWANA niliwafanya kuwa watakatifu” Ezekiel 20:12.

Hata ingawa nilikuwa nikijifunza juu ya Sabato ya Mungu bado nilikuwa nikiishika Jumapili lakini huku nikiwa na mashaka mengi,

kwani nilipowauliza wachungaji wangu maswali juu ya Sabato, walikuwa wakinipa majibu yasiyotosheleza nao walikuwa hata tarayi kupambana na mimi wakinichukulia kama mtu aliyekuwa akileta mgawanyiko katika kanisa lao.

Watu wengi walikubaliana nami na kuyapokea mafundisho juu ya Sabato lakini mbele ya mchungaji, wengi waliniacha na kuambatana naye kwa ajili tu ya woga. Hivyo hilo lilikuwa ni tatizo kubwa kwangu hadi siku moja ya Sabato asubuhi, nikafanya uamuzi katika nafsi yangu kutafuta mahali ambako wale waliokuwa wakishika Sabato ya Mungu walikuwa wakikutana.

## Baada ya Mchungaji wa Kipentekoste Kupingana na Sabato, Niliambatana na Wa-S.D.A.

Nikiwa njiani kwenda kupatafuta, nilikutana na waumini wa Ki-Seventh Day Adventist (SDA), wakienda kuhuduria ibada ya siku ya Sabato. Nilipozungumza nao juu ya ni siku ipi waliyokuwa wakiishika, waliniyeza kwamba walikuwa wakishika Sabato. Tangia hapo mimi pia nikawa muumini wa dhehebu la SDA.

Mwanzioni, nilishawishika kuamini kwamba walikuwa ni kanisa la kweli la Mungu, kwa kuwa tu walikuwa wakishika Sabato. Nilidumu ndani ya U-SDA hadi nikafikia kuwa Mhubiri azungukaye akifundisha kila sehemu. Siku moja tulienda kufungua Shule mpya ya Sabato, ambako mimi ndiye nilikuwa nimekaribishwa kuongoza mahubiri. Ilikuwa ni siku ambayo wengi waliyafurahia mahubiri yangu na wengi wakaamua kuijunga na imani hiyo ya Ki-SDA na siku hiyo dhehebu la SDA lilipata mafanikio makubwa sana.

## Ndipo Nikakutana na Mafundisho ya Kanisa la Worldwide Church of God ya Kale

Ikiwa ni saa za jioni tukiwa kwenye kujifunza Biblia, pasipo sisi kufahamu kumbe mionganini mwetu kulikuwa na mtu ambaye alikuwa mtendakazi na Mungu katika Kanisa la WORLDWIDE CHURCH OF GOD. Mtu huyu akaanza kupingana na mafundisho yetu kama vile:

1. Namna tulivyoishika Pasaka! Katika kanisa la SDA tulikuwa tukiifanya Pasaka mara 4 kwa mwaka. Lakini Biblia inafundisha Pasaka ifanyike mara moja tu kila mwaka (Mambo ya Walawi 23:5).
2. Ni kwa nini sisi (katika kanisa la SDA) tulikuwa tukihubiri juu ya kwenda mbinguni baada ya ufufuo kwa miaka 1000? Biblia inasema hakuna kwenda mbinguni kwa miaka 1000 bali Kristo ndiye atakayekuwa duniani kuja kutawala dunia kwa miaka 1000 (Yohana 7:33-34):

“33 Yesu akasema, ‘Mimi bado niko pamoja nanyi kwa kitambo kidogo, kisha nitarudi Kwake Yeye aliyenituma. 34 Mtanitafuta, lakini hamtaniona, nami niliko, ninyi hamwezi kuja’”.

Baadaye aliwaambia tena katika Yohana 8:21-24:

"21Yesu akawaambia tena, "Ninaenda zangu, nanyi mtanitafuta, lakini mtakufa katika dhambi zenu. Niendako ninyi hamwezi kuja." 22Ndipo wale Wayahudi wakasema, "Je, atajua? Je, hii ndiyo sababu amesema, 'Niendako Mimi ninyi hamwezi kuja?' 23Akawaambia, "Ninyi mmetoka chini, mimi nimetoka juu. Ninyi ni wa ulimwengu huu, mimi si wa ulimwengu huu. 24Nilwaambia kuwa mtakufa katika dhambi zenu, kwa maana msipoamini ya kwamba 'Mimi Ndiye,' mtakufa katika dhambi zenu'."

Tunakuta katiak Ufunuo 11:15 kwamba:

"15Yule malaika wa saba akaipiga tarumbeta yake, pakawa na sauti kubwa mbinguni iliyosema: "Ufalme wa ulimwengu umekuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atatawala milele na milele".

Soma pia: Ufunuo. 5:10, Danieli 7:26-28, n.k.

3. Na vipi kuhusu Sikuu Takatifu saba zilizoamuliwa na Mungu ambazo kanisa la SDA halizishiki? Law. 23. Mtu huyu alikuwa na vijitabu mkononi mwake. Na kwa kuwa nilikuwa ninamashaka ikiwa alikuwa anaafuata Biblia, nikavipokea hivyo vitabu ili niweze kuvisoma. Vitabu hivi viliitwa: 1. "God's Holy Days or Pagans Holidays? – yaani, ( Ni Sikuu Takatifu za Mungu ama ni mapumziko ya Kipagani?); kitabu kingine kiliitwa: "The Gospel of the Kingdom" – yaani, (Injili ya Ufalme) vyote vikiwa viliandikwa na Armstrong.

Hivyo ndivyo nilivyoitwa kuingia kwenye Kanisa la Mungu. Katika Kanisa laMungu ndipo palipo na ukweli kamili na "lililo nguzo na msingi kweli" (1 Timotheo 3:14).

## Nikawa Mchungaji

Nilibatizwa katika WCG ambako nilibaki hadi pale mchungaji Tkach alipoleta mafundisho potofu katika Kanisa la Mungu. Huo ndio muda nilipoamua kujitoa toka WCG.

Ilichukua muda kadhaa kabla hatujajiunga na kundi lolote. Baadaye tukapata mawasiliano ya anuani ya kundi la United Church of God (UCG) na tukawaandikia. Walimtuma Mchungaji Batholomew wa South Africa aliyejuka kukutana nasi hapa Kenya. Tukajiunga na UCG na mwaka huo tukaishika Sikuu ya Vibanda pamoja nao hapa Kenya ambapo walimtuma Mchungaji George De Lap kutoka Scotland pamoja na Nail Baker kutoka South Africa. Punde baada ya Sikuu Batholomew akaja tena Kenya akiwa na taarifa za masikitiko kwamba UCG ilikuwa imegawanyika, hivyo kila mtu anapaswa aangalie ni wapi atahitaji kujunga. Ikatukia pale nilipoamua nikisoma kitabu kiitwacho: "The Ten Commandments" cha Dr. Roderick Meredith. Ndipo nikaamua mimi mwenyewe nijiunge pale alipo Meredith.

Kwa sababu nilijua kwamba kulingana na kitabu alichokiandika, asingeliweza kufuata mafundisho potofu ya Tkach. Hii ndiyo sababu nilijunga na Global Church of God (GCG). Tukaishika Sikuu ya Vibanda tukiwa na GCG mwaka huo.

Lakini kwa mara nyingine, baada ya Sikuu hiyo tukapokea

habari kwamba GCG nayo ilikuwa imegawanyika. Larry Salyer akiwa na wenzake wameenda njia yao na Dr. Meredith na wenzake nao wameenda njia nyingine. Kusema kweli ilikuwa ni habari ya kusikitisha. Katika wakati huo, niliamua kujunga na Living Church of God (LCG) aliyokuwa nayo Dr. Meredith.

Katika LCG nilisimamia vikundi vitano tofauti hadi ilipofikia wakaamua kutaka kuniwekea mikono ili niwe Shemasi. Mpango huo ulipokuwa umekamilika, mchungaji wetu wa Kenya akafanya kosa kubwa, ambalo hakulitubia. Hivyo sikuweza kukubali kuwekewa mikono na mtu kama huyo. Nilikataa swala hilo pale Mchungaji Dr. Winnail alipokuja Kenya kuamua tatizo la huyu mchungaji wa Kenya na mke wake pamoja na mwanamke mwingle kanisani. Nikaamua kujitoa toka LCG kutokana na mambo mabaya ambayo huyu mtu wa Kenya alikuwa akiyatenda.

Baadaye, niliteuliwa kuwa Mwakilishi wa kundi la COG IN TRUTH. Tukiwa na Mchungaji Bill Goff, tukashiriki katika COG IN TRUTH. Aliona namna kundi hili lilivyokuwa likininyanya katika kazi. Na akaamua kunisiaidia kifedha katika kila safari zangu za kikazi. Baadaye yeche pia aliamua kujitoa katika kundi la COG IN TRUTH. Hatimaye, sisi pia tuliamua kujitoa na tukaanzisha kazi ya Mungu pamoja naye. Hadi sasa bado tunapendana na kuheshimiana baina yetu naye. Ni mtu ambaye ni mnyenyeketu na hujitoa kwa muda na mali zake katika kumtumikia Mungu. Ninamshukuru sana kwa kujitoa kwake. Niliwekewa mikono na yeche kuwa mchungaji.

Nimekuwa nikintumikia Mungu kama mchungaji katika Kenya kwa miaka 10.

Katika mwaka 2013, niliwasiliana na Mchungaji Dr. Bob Thiel wa Kanisa la Continuing Church of God (CCOG). Nilimjua tangia tukiwa pamoja enzi za Global na baadaye Living Church of God. Nilivutiwa na mwamko wake katika kazi ya Mungu anayofanya katika CCOG. Niliwasiliana naye na kutaka Munguidie kujua kazi aliyokuwa akiifanya ndani ya Continuing Church of God.

Baada ya kuyapitia machapisho mengi ya kanisa la CCOG, tukibadirishana naye email nyingi, ikiwemo pia kukutana na wengine katika kanisa hili, na hatimaye kuwa na maongezi na Dr. Thiel, nilimuomba niweze kuwa Mwakilishi wa Continuing Church of God hapa kama Mchungaji.

Kwa sasa ninasimamia makundi 20 ya kikanisa yaliyoko Kenya pamoja na jingine la Tanzania nikifanya hivyo kama Mchungaji wa Continuing Church of God. Wako pia wengine kule Tanzania ambaa ninatarajia kukutana nao ambaa nao ni washirika wa kundi la Continuing Church of God.

Taarifa za Mchapishaji: Kulingana na tabia ya Mchungaji wa LCG kipindi kile,inanibidi nieleze kwamba hata nami nilisikia juu ya taarifa hizo na nikalifanya maombi tatizo hilo, lakini katika muda huo sikuwa nimeamini iwapo mimi (ama LCG) tulikuw na ukweli wote kamili juu ya hilo (Nilikuja kuelewa zaidi juu ya swala hilo hapo baadaye, kitu kilichothibitisha lile nililokuwa nimelisikia). Ninakubaliana na uamuzi wa Evans Ochieng kukataa kuwekewa mikono wakati ule na naelewa ni kwa nini alijitoa toka LCG kipindi hicho. Wengine pia katika kanisa hilo wamekuwa na matatizo ya kitabia, jambo ambalo lilinifanya niondoke LCG pale nilipoamua hivyo.

# Kuitekeleza Mathayo 24:14 Pamoja na Mathayo 28:19-20



*Website ya Kanisa la Continuing Church of God: [www.ccog.org](http://www.ccog.org)  
Website ya Taarifa za Unabii wa Biblia za Kilasiku: [www.cogwriter.com](http://www.cogwriter.com)*

**CCOG.ASIA:** Hii ni Website ilengayo wasomaji kutoka Asia. Inazo makala katika lugha ya Kichina cha Mandarin pia na katika Kiingereza pamoja na lugha zingine za Kiasia.

**CCOG.IN:** Hii ni Website inayolenga wale walio wa asili ya kihindi.

**CCOG.EU:** Hii ni Website kwa wale wa Ulaya. Inazo makala katika lugha nyingi za Ulaya.

**CDLIDD.ES:** Hii ni website ya Continuing Church of God katika lugha ya Kihispania.

**PNIND.PH:** Hii ni Website kwa ajili ya wale wa Ufilipino ama wenye asili yao.



***Chaneli ya Habari za Unabii wa Biblia***  
[www.youtube.com/BibleNewsProphecy](https://www.youtube.com/BibleNewsProphecy)

***Chaneli ya kanisa la ContinuingCOG***  
[www.youtube.com/continuingcog](https://www.youtube.com/continuingcog)

---

Mchungaji Mwandumizi wa Continuing Church of God ni mgeni mwalikwa mara kwa mara kwenye radio, akitumia radio kuwafikia wasikilizaji wa maeneo mengi.

Kanisa la Continuing Church of God pia hutumia majarida pamoja na magazeti ya kielectronic, vitabu na barua za kila juma kwa waumini wake katika nkutekeleza Mathayo 24:14 pamoja na Mathayo 28:19—20

